

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

- | | |
|---------------------------------------|--|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwanii. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvumi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28. Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi/Jimbo la Mpandae.
31. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32. Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34. Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35. Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40. Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad

Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita - Tarehe 22 Mei, 2015

(Kikao kilanza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuweka mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamti ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar 2015/2016.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 60

Wimbi la Uingiaji wa Watu Kiholela Zanzibar

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: (Kny. Mhe. Salim Abdalla Hamad) - Aliuliza:

Kwa sababu Serikali inaelewa wazi kuwa hapa Zanzibar uingiaji wa watu unaongezeka kila uchao na unasababisha matatizo ya kiuchumi na hata kiusalama kutokana na uhuru wa kuingia bila ya pasipoti, kwa wale wanaolazimika na hilo.

Je, Serikali haioni kuwa kwa kujiiamarisha kiuchumi, kudumisha usalama wetu na kwa kudumisha utamaduni, mila na desturi zetu wakati umefika wa kuiangalia vizuri hali hii na kubadilisha utaratibu huu hatarishi uliopo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad Mwakilishi wa Mtambwe swali lake namba 60 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali haijaruhusu wale wanaolazimika kuingia na Pasipoti nchini, ambao ni raia wa kigeni kuingia bila ya Pasipoti na tutaendelea kulisimamia hilo kwa mujibu wa Sheria ziliopo na zile za Kimataifa, ili wale wote wanaowajibika kuingia na paspoti wanafanya hivyo.

Mhe. Spika, hata hivyo Serikali inaendelea kuimarisha shughuli ulinzi na usalama pamoja na kuhakikisha wageni wanaoingia nchini wanafuata sheria na taratibu za nchi ili kuona wageni hao wanasaidia shughuli za kuimarisha uchumi, kudumisha amani na usalama wetu pamoja na kuendeleza utamaduni mila na desturi zetu.

Mhe. Spika, naomba nitanabahishe kuwa vyuo vyetu nya ulinzi na usalama vipo macho kwa wageni na wale wote wenye nia ya kudhoofisha ulinzi, usalama na uchumi wetu. Hivyo hakuna hali hatarishi ikiwa wageni wanaoingia nchini wanafuata taratibu na sheria kwani sheria zimeveka kutulinda. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, ninashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa uingiaji wa watu Zanzibar unaongezeka siku hadi siku na kwa kuwa kuna baadhi ya nyakati kunakuwa na milio ya risasi isiyotarajiwa katika maeneo ya biashara hapa Zanzibar, kunajenga hofu kwamba kwa utamaduni wetu wa Zanzibar wa upendo, amani na utilivu, inawezekana kwamba wanaofanya vitendo hivi ni wale ambao hawafuati utamaduni wetu wa kizanzibar. Je, Ofisi ina mpango gani wa kufanya operation maalum ya kuwatambua wahamiaji haramu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nipokee ushauri wa Mhe. Mwakilishi kwa ajili ya kufanya *operation* maalum, hata hivyo hivi sasa Idara ya Uhamiaji Zanzibar inachukua hatua kufanya *operation* kutafuta wageni wanaoishi nchini bila ya kufuata taratibu na sheria zilizowekwa. Kwa hivyo tutaendelea kulisimamia hili ili kuhakikisha wale wote wanaoishi nchini bila ya kufuata taratibu wanatia mbaroni na hatua za kisheria zinachukuliwa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri pale naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ardhi ya nchi yetu ni ndogo sana na kutokana na udogo huo ndio maana muasisi wa nchi hii alianzisha utaratibu maalum wa kutoa *permission* kwa kila asiyekuwa Mzanzibari kuingia hapa na kujulikana alipo na lini ataondoka. Sasa kwa sababu utaratibu ule

umeondolewa na kwa sababu nchi yetu sasa inaonekana kuingiliwa na wageni wengi mno wasiokuwa Wazanzibari halisi. Je, Mhe. Waziri haoni kuja haja sasa ya kuufufua ule utaratibu ili tuweze kuwajua Wazanzibari ni wepi na wasiokuwa Wazanzibari ni wepi.

Pili, mpaka hivi sasa wale ambao wamo katika nchi hii ambao si wazanzibari halisi wamefikia idadi gani. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nchi yetu kama alivyosema ni ndogo na kwa kila hali inahitaji udhibiti wa kuchukua hatua ili wale ambao hawafati taratibu za kisheria wasiweze kukaa nchini.

Mhe. Spika, uzanzibari ni sifa inayotokana na kuwa Mtanzania, kwa hivyo wale wote walioitimiza masharti ya kuwa Wazanzibari hawa wote ni Wazanzibari halisi na wana haki ya kuishi Zanzibar. Lakini Mhe. Spika, ningependa nitanabahishe kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Watanzania wote wana haki kuishi mahala popote katika upande wowote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo kwa wageni wale ambao hawana haki hiyo Idara ya Uhamiaji itaendelea kuchukua hatua, ili wale wote wanaokaa nchini wawe ni wale ambao wamekaa kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Mhe. Spika, tumefungua milango yetu kwa ajili ya uwekezaji na kwa njia moja au nyengine maendeleo makubwa yamepatikana na mafanikio makubwa ya kijamii na kiuchumi yamepatikana kutokana na kuanzisha utaratibu wa kuanzisha vitega uchumi nchini. Kwa vyovyyote itakavyokuwa unapoanzisha utaratibu huo utapata wageni wengi, wageni ambao wakikaa hapa sio tu watatusaidia kupata mazingira ya kujiongezea kipato cha kiuchumi, lakini pia wanao ujuzi fulani ambao kuja nao nchini katika suala zima la kitega uchumi na husaidia kutaalamisha wananchi wetu. Kwa hivyo wageni wakati mwengine inakuza soko, inakuza uchumi, cha msingi ni kufuata taratibu za sheria za nchi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ninashukuru sana, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri tena kwa utulivu sana kweli kweli na tumeyafahamu. Mimi nina swalii dogo tu la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa sababu Zanzibar ni nchi na kwa sababu Katiba inaeleza kuwa Zanzibar ni mionganii mwa nchi mbili zilizoleta muungano huu wa Tanzania inahitaji kuwa na haki zake za kinchi pamoja na watu wake. Kwa sababu sheria imeeleza kuwa mtu yoyote anayetoka upande wa pili wa Muungano na ikiwa ni

Mtanzania na akiweza kuishi kwa mfululizo kwa miaka 15 hapa moja kwa moja ni njia ya kumpatia Uzanzibari lakini Wazanzibari wapo pamoja na nchi yao.

Kwa mtindo huo na kwa sababu Mtanzania anayo haki ya kuishi popote ukiangalia mazingira ya Zanzibar hivi sasa yalivyo naona Uzanzibari wetu unaingia katika hali ambayo mwisho itakuwa hatuna maamuzi kwa Wazanzibari kutokana na kuwa tutakuwa tuna watu wengi sana ambao wanatoka upande wa pili wa muungano.

Sasa ili kuweza kudumisha uhuru wetu, utamaduni wetu, silka zetu na kuweza kuijiendeshea nchi yetu wenyewe hatuoni kuwa tusiache tu watu wakaja wanavyotaka kiasi ya kutozidi kwa idadi wakaja kutuharibia mambo yetu tuweke utaratibu ambao ikifika kiwnago hicho kwa sababu ya udogo wa nchi yetu iko haja ya kutafuta utaratibu mwengine hiyo ni moja.

Pili, kwa sababu tumeshuhudia kuwa wenzetu wanaoingia hapa na ni haki yao kuingia lakini kwa sababu ya kuwa ni Watanzania kuna mambo ambayo si ya kisheria wala si ya kihaki ya kupatiwa vitambulisho vya kupiga kura jambo ambalo linavuruga kweli kweli haki yetu ya Mzanzibari kwa kifungu nambari 7(1) na (2) ukurasa wa 3 Katiba, je, Mhe. Waziri haoni iko haja sasa ya kutoa taaluma hasa kuwa pamoja na kuwa Mzanzibari, Mtanzania anaweza akaishi popote lakini, si kila Mtanzania mwenye haki sawa sawa na Mzanzibari Zanzibar kabla ya kuwa na programu yake kamili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu uingiaji nchini hasa alivyokusudia kwa wenzetu kutoka Tanzania Bara. Kama kisiwa kwa vyovyyote vile uigiaji hauwezi kuwa mkubwa kama watakavyoingia watu kutoka Kisiwani kwenda Bara na ushahidi wa wasi upo. Mhe. Spika, kwamba sisi Wazanzibari tulioko Bara ni wengi zaidi kuliko Wabara walioko Zanzibar. Kwa hivyo unapochukua hatua zozote zile za kubagua unajibagua mwenyewe. Sote uelewe kwamba kwa kiasi kikubwa sisi Wazanzibari tuko Tanzania Bara tunafanya shughuli zetu bila ya kubughudhiwa na vivyo hivyo wenzetu walioko Tanzania Bara wana haki ya kufanya shughuli zao Zanzibar bila ya kubughudhiwa.

Mhe. Spika, ni utaratibu wa tu wa mpango kuna nchi ndogo kama vile Singapore, Dubai, ni ndogo lakini zina wageni wengi kuliko wenyewe ndani ya nchi lakini zina manufaa makubwa kimaendeleo. Kinachotakiwa tusiwe na mawazo ya nyuma, tusonge mbele kufikiria zaidi wageni wetu wawe ni sehemu ya uzalishaji na mapato makubwa yaye katika nchi yetu.

Hata Uingereza ni nchi ndogo sana lakini kiutaratibu ni namna gani unajipanga ili wageni wanaoingia nchini wanakuwa ni sehemu na chachu ya uzalishaji na kuongeza mapato ya nchi. Kwa hivyo cha msingi hapa ni namna gani tutajipanga

kama Wazanzibari. Katika ulimwengu wa leo wa intergration huna namna ya kuepuwa wageni ndio hali halisi watu wanakwenda kwa kuishi licha ya kinchi, kikanda iko kimataifa na kadhalika. Kwa hivyo huwezi kujigawa ukawa nje ya ulimwengu. Labda uichukuwe Zanzibar ukaijenge mbinguni huko ambapo ni jambo haliwezekani. Madhali ni kisiwa watu wataingia na watu watakuwepo.

Kuhusu vitambulisho vya Mzanzibar, vitambulisho vya Mzanzibari vina taratibu zake kisheria, kama mtu amepewa kitambulisho kinyume na utaratibuwa kisheria hatua zichukuliwe ni kosa hairuhusiwi, wanaopewa ni wale ambao wanafata utaratibu wa kisheria.

Nam. 28

Kuhamasishwa kwa Wazanzibari Wanaoishi Nje Kuunga Mkono Juhudi za Serikali

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:

Kwa kuwa wananchi wa nchi mbali mbali wanaoishi nje ya nchi zao (Diaspora) huwa wanatoa mchango mkubwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi zao. Na kwa kuwa Zanzibar Diaspora wametawanyika sana ulimwenguni kote. Na kwa kuwa tayari katika Serikali lipo Dawati maalum la Diaspora. Na kwa kuwa na wao wanamoyo wa kuchangia maendeleo ya nchi yao.

Ni lini Serikali kuititia Dawati la Diaspora watapita katika nchi kadhaa Duniani kuwashamasisha Wazanzibari wanaoishi nje kuunga mkono juhudhi za Serikali pamoja na kuchangia katika suala zima la Uhifadhi wa Mazingira, ambayo yanazidi kuathirika siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi swali lake Nam. 28 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, watendaji wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje tayari wamefanya ziara katika nchi mbali mbali na kukutana na Wanzanzibari wanaoishi huko. Nchi hizo ni pamoja Uingereza, Marekani, Brazil, UAE, Oman na Denmark. Aidha, Viongozi Wakuu wetu wote wanapofanya ziara nje ya nchi hupata nafasi ya maalum ya kukutana na wazanzibari hao wanaoishi nchi za nje au *Diaspora* Zanzibar na Watanzania kwa ujumla.

Mhe. Spika, lengo la ziara hizo ni kuwashajiisha Wanadiaspora kuchangia maendeleo ya Zanzibar kwa kuzijumuisha sekta zote za Kiuchumi, Kijamii na Sekta Mtambuka ikiwemo uhifadhi wa mazingira. Naomba Mhe. Spika, nitoe shukurani maalum kwa Wazanzibar hawa wanaoishi na kufanya kazi nchi za nje, kwa kweli wameonesha uzalendo wao kivitendo kwa kuchangia katika maendeleo ya nchi yao ikiwa ni pamoja na kuangalia jamaa na ndugu zao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ya kujibu swali la msingi nimuombe kumuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza. Kwa kuwa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi idadi yao inaongezeka siku hadi siku serikali imefanya utafiti gani kujua wako wangapi. Hilo moja.

Pili, kwa kuwa Zanzibar inakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo uhaba wa madawati ya skuli, vifaa vyaa mahospitali hasa maabara serikali kwa nini haijatumia Wazanzibari hao wanaoishi nje ya nchi kukabiliana na tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba sasa kwa muhtasari nilitarajia suala la takwimu kwa hiyo nilijiandaa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013 katika ziara tulizofanya Wazanzibari tuliowaorodhesha Oman ni 374, kwa upande wan nchi za Falme za Kiarabu mwaka 2012 tuliorodhesha Wazanzibar wapatao 85, na kwa upande wa Brazil mwaka 2014 tuliorodhesha idadi ya Wazanzibari 11. Upande wa Marekani mwaka 2012 tuliorodhesha Wazanzibari 170, na upande wa Uingereza mwaka 2013 tuliorodhesha Wazanzibar wapato 220, upande wa Denmark kwa mwaka 2013/2015 tuliorodhesha Wazanzibari 33, India tulijitahidi lakini hatukupata hasa takwimu, tunaendelea nazo.

Mhe. Spika, idadi hii ni Wazanzibari waliowahi kutembelewa na Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Diaspora, idadi kamili ya Wazanzibari wote wanaoishi nje ya Zanzibar itajulikana kama alivyoshauri Mhe. Mwakilishi baada ya kufanya utafiti wa kina utakaotoa takwimu halisi na uwezo wao kiuchumi, hadhi na kiwango cha ujuzi kwa kila mwanadiaspora atakayejirodhesha.

Kwa upande wa misaada wanayotoa au wanavyochangia ni kweli ipo haja kubwa na kama nilivyosema wameshajionesha kivitendo katika kuchangia vifaa vyaa skuli na hata hospitali.

Nitatoa mfano Skuli ya Shaurimoyo mwaka 2014 walipata msaada wa vifaa vyaa elimu kutoka kwa Wazanzibari wanaoishi nchi za *Scandinavian*. Vile vile kwa upande wa hospitali ya zamani ya Kijiji cha Mahonda Mzanzibari maarufu Dkt.

Ame Shumetah na gurupu yake wameifufua ile hospitali ya Mahonda na kuanza kutoa huduma bora za afya pamoja na vifaa nya kisasa katika hospitali hiyo mwaka jana.

Halikadhalika umoja wa Wazanzibari wanaoishi Marekani Mhe. Spika, nao walitoa msaada wa kompyuta na *laptop* kiwango cha kontena moja la futi 40, wao waliwapa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kusambaza katika skuli zenye mahitaji hayo.

Pia Wazanzibari wanaoishi Canada Mhe. Spika wao wameleta walimu wa kujitolea kutoka nje ya nchi kwa lengo la kusomesha sayansi na lugha ya Kiingereza katika Skuli ya Unguja kuu tokea mwaka 2013 mpaka hii leo wanaendelea. Kwa hiyo, kama nilivyosema lazima tuwapongeze michango kama hii Mhe. Spika imeanza kutiririka kwa wingi kabisa. Ahsante.

Nam. 8

Ujenzi wa Barabara ya Matale – Chanjaani kwa Kiwango cha Lami

Mhe. Abdalla Juma Abdalla (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Kwa kuwa miradi mingi ya barabara za ndani imefanywa Kisiwani Pemba (*feeder roads*) na kwa kuwa barabara ya Pujini hadi leo hii hajijengwa pamoja na umuhimu wake kwa wananchi katika Wilaya nzima ya Chake Chake, kwani husaidia sana kwa kusafirisha mazao muhimu kama vile ndizi, nyanya, mahindi pamoja na mihogo kutoka Pujini, Matale hadi katika soko la Qatar.

Je, ni lini serikali itajenga barabara hii katika kiwango cha lami na hatimae kuweza kujenga daraja katika mto chuchuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, matarajio yetu Halmashauri ya Wilaya ya Chake-Chake wataona umuhimu wa baraabra hiyo kwa ajili ya kulinda na kuweza kusafirisha mazao ili kufika sokoni mapema na kwa wakati. Aidha, kwa upande wa aina ya ujenzi utaenda hatua baada ya hatua kutoka kiwango cha kifusi na hatimae kiwango cha lami.

Mhe. Spika, barabara aliyoitaja Mhe. Mwakilishi ni mionganoni mwa barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Chake-Chake na kwa bahati nzuri mwaka huu wa bajeti kupitia Mfuko wa Barabara tayari tumetengeneza utaratibu maalum wa kuweza kufikisha fedha katika Wizara ya Tawala za Mikoa hasa katika Halmashauri, ili kuweza kuweka umuhimu na kipaumbele katika maeneo husika kwa kuzingatia miradi kama hii ya barabara katika maeneo yaliyokusudiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali madogo tu ya nyongeza.

Kwa kuwa suala la uchakavu wa barabara linagusa wananchi moja kwa moja na wakati mwengine kuwa chanzo cha mafuriko, serikali imejipanga viyi kushughulikia barabara za ndani yaani *feeder road* hasa ukizingatia mwaka huu na kipindi tulichokuwa nacho cha mvua kubwa za kunyesha.

Hilo moja na ikiwemo vile vile barabara ya Jambiani ambayo Mhe. Naibu Waziri kwa kilio kikubwa kwa wananchi wa Jambiani. Kwa kuwa waathirika wakubwa ni wananchi serikali ina mpango gani wa kuwapunguzia wananchi maumivu kutokana na gharama kubwa ya *road license* iliyopandishwa na serikali ukizingatia barabara yenyewe serikali kwa muda mrefu hazishughulikii.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, samahani naomba hili swalii lake la pili arejee taratibu ili niweze kumsikia vizuri na niweze kumfahamu alichokusudia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swalii la pili ni kwamba Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa waathirika wakubwa ni wananchi serikali ina mpango gani wa kuwapunguzia wananchi maumivu kutokana na gharama serikali iliyopandisha kuhusu charge za *road license*, ukizingatia serikali barabara nyingi haiziangalii hasa za ndani ikiwemo ya Mhe. Thuwayba ya Fuoni na alizotaja Mhe. Saleh Nassor Juma na vile vile ikiwemo barabara ya Jambiani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia taasisi yake ya Mfuko wa Barabara jukumu kubwa na la msingi na wajibu wao taasisi hii ya mfuko wa barabara ni kuhakikisha kwamba barabara zetu zote zilizojengwa zinatunzwa na kuwa endelevu.

Kwa hiyo, kama kutatokea athari yoyote ni wajibu wa serikali kwa kupitia mfuko huu kuweza kufanya matengenezo. Kuna baadhi ya matengenezo yanaweza yakawa madogo, kuna baadhi ya matengenezo yanaweza yakawa ya muda mrefu. Na kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kuwa tunatoka katika kipindi

cha mvua kuna maeneo mengi ambayo yameathirika, tayari serikali kwa kupitia mfuko wa barabara kuna baadhi ya kazi ambazo tumeona kwa kufanya tu taasisi yetu ya serikali ya Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara haitokidhi.

Tayari tumefanya zabuni na kuweza kupata wakandarasi wa nje ya serikali ili kuona kwamba tunapunguza muda katika kurekebisha barabara zile, ili wananchi waliokusudiwa kupata huduma nzuri za matumizi ya barabara waweze kupata kama yalivyo malengo ya serikali.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara za ndani nyingi takriban huwa zinashughulikiwa na Mbunge na Mwakilishi wa eneo husika. Na kwa kuwa kiwango cha utengenezaji wa barabara hizi kwa Mbunge na Mwakilishi ni kiwango cha kifusi, kutohana na uwezo mdogo walionao, na kwa kuwa barabara za eneo la Chambani kama vile Kwamtora, Uktutini, Kiembeni/Matele, Kiembeni/Mapape na kadhalika katika msimu uliopita zilitiwa kifusi kwa kiwango kizuri.

Lakini kifusi hiki kimebururwa na maji ya mvua za Masika zilizonyesha hivi juzi. Je, Mheshimiwa wizara yako ina mpango gani wa kuziendeleza barabara hizi ambazo zinatengenezo la Mbunge la Mwakilishi ili kuwapunguzia wananchi hawa matatizo ya usafiri kufika katika barabara kuu. Ahsante.

Mhe. Spika: Suala limekuwa na mtawanyiko mkubwa na mchanganyiko pamoja na hili saidia majibu kama yapo karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza naomba nimpe pongezi Mhe. Mwakilishi kwa kushirikiana na Mhe. Mbunge wake kama wanaweza kujenga barabara kwa kiwango cha kifusi katika maeneo hayo ya wananchi. Lakini kama yalivyo maelezo yake kwamba kinachowakwaza kwamba washindwe kujenga kwa kiwango cha lami katika maeneo haya, barabara ziliuwepo jimboni kwao ndicho hicho hicho kinachoikwaza serikali kushindwa kujenga kwa kiwango cha lami katika maeneo hayo ambayo tumeyataja.

Wajibu wa serikali ni kuona kwamba tunakamilisha hii miradi mikubwa ya kuunganisha barabara zetu kubwa, maeneo yote ya Mikoa kwa Mikoa, Wilaya kwa Wilaya tufike katika ngazi ya jimbo maeneo ya Mijini, baadae tutakwenda maeneo yote hayo. Lakini inategemea hali ya uchumi na mimi nimuhakikishie tu kama kuna maeneo ambayo yameathirika vibaya serikali kwa kupitia Halmashauri, tutahakikisha kwamba tunakwenda kutoa kila aina ya msaada ili kuweza kuunganisha daraja hilo la kuweza kuunganisha watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu ya pili.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, mimi kwanza niipongeze serikali kwa hatua ilizozichukua kutengeneza barabara hizi ndogo *feeder road* ikiwemo barabara ya kutoka Mzambarautakao mpaka Mchangamdogo, kutoka Kitambuu mpaka Kambini Kichokochwe, Mheshimiwa kuna utaratibu gani barabara ile ili kudumu kwa muda mrefu. Kwa sababu katika kipindi hiki cha mvua zote zimeshaanza kuharibika, serikali ina utaratibu gani kuweza kuzidumisha tukatumia kwa muda mrefu. Hilo moja.

- b) Kwa sababu barabara kutoka Wete kuititia njia kongwe mpaka Chake-Chake imechimbika vibaya sana na ni hatari kweli kweli hata kwa maisha ya wananchi wanaosafiri barabara ile, kila siku na kila siku tunaambiwa kuna mkandarasi anatafutwa sijui, mipango gani lakini mpaka leo hajakamilika. Barabara ile hasa nataka utueleze Mheshimiwa kuna utaratibu gani unaofikiwa hatua ya kuweza kujenga au malengo ya baadae kuweza kujenga, naomba kujua.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la mwisho kwamba barabara ya Wete hii tayari tuko katika taratibu za mwisho za kukamilisha zabuni ili tuweze kujenga na mradi huu ni mkubwa tukisema kama tutajenga wenyewe kilomita zaidi ya 22 tutachelewa muda mrefu.

Mradi huu unategemea wafadhili ambapo tayari mfadhili mmoja tayari ameshatuthibitishia upatikanaji wa fedha na mfadhili wa pili nae tayari yuko katika harakati za kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha na imani yetu tukikamilisha taratibu za zabuni ujenzi utaanza mara moja.

Nikuombe tu Mhe. Mwakilishi wewe pamoja na wananchi tuendelee kufanya subra madhumuni ya serikali ni kuona kwamba tunajenga mradi huu uwe mradi mzuri na ukamilike kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa.

Mhe. Spika, suala la pili anaulizia kwamba ujenzi wa barabara kukinyesha mvua kifusi kinaondoka. Ni kweli ujenzi wa barabara kwa kiwango cha kifusi unategemea mambo mawili. La kwanza ni maumbile ya ardhi husika lakini la pili aina ya kifusi ambacho kimetumika. Kuna baadhi ya maeneo, maeneo ya karibu yanayohusika hayana kifusi kizuri. Kwa hiyo, ukichukua kifusi ambacho ni chepesi cha jasi ikinyesha mvua kitaondoka.

Pia yapo maeneo ambayo ardhi maumbile yake ni ya udongo kwa hiyo inahitaji kifusi maalum kiwezwe kuwekwa vizuri *layer* isipungue mbili ama tatu ndio kiweze kudumu kwa mudara mrefu. Lakini yapo baadhi ya maeneo ambapo barabara zimejengwa kwa kiwango cha kifusi zimekaa zaidi ya miaka mitatu.

Mfano, Makunduchi, Cheju yapo baadhi ya maeneo kama haya ambapo tumeweza kujenga kwa kiwango cha kifusi na imekaa vizuri.

Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi pengine hayo maeneo umeyaona yalikuwa na athari hizo ya maumbile ya ardhi ama kifusi kilichotumika hakikuwa muafaka katika eneo hilo. Kwa hiyo, matarajio yetu kama tutapata kifusi muafaka kwa eneo na hali ya ardhi au maumbile ya ardhi yatakuwa na hili basi barabara ya kifusi inaweza kudumu. Lakini malengo ya barabara ya kifusi ni kwa muda baadae unapata uwezo kujenga kwa kiwango cha lami. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 25

Tatizo la Umiliki wa Ardhi Katika Eneo Liliopo Kwareni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Kwa kuwa Taasisi binafasi ya Istiqama wanayohati miliki ya umiliki wa ardhi katika eneo liliopo Kwareni Makaani. Na kwa kuwa taasisi hiyo tayari imeanza kuitumia ardhi hiyo kwa kuanza kujenga jengo moja la kisasa kwa ajili ya shule. Na kwa kuwa sehemu hiyo hiyo, inayomilikiwa na Taasisi hiyo vile vile wamepewa Kampuni ya Ujenzi ya *MECCO* na tayari wameanza kuweka Mashine (*Crusher*) na wameanza kuchimbua kifusi pamoja na kupasua miamba kunakoathiri sana jengo la mmiliki wa kwanza.

- (a) Je, ni nani mmiliki halali wa ardhi hiyo.
- (b) Kama serikali imetoea umiliki wa watu wawili katika ardhi moja huko si kuzigombanisha taasisi hizo mbili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, enneo la Kwareni Makaani lilitolewa kwa taasisi ya Istiqama mwaka 2009. Baadae serikali iliamua kuwafutia eneo hilo kwa sababu yakutokuliendeleza pia kutaka kutumia eneo hilo kwa matumizi mengine. Baada ya kupata *notice* ya uftutaji taasisi ya Istiqama ilipeleka kesi Mahakamani na hadi sasa hivi serikali inasubiria maamuzi ya Mahakama.

- (a) Mhe. Spika, kwa vile hati haijafutwa bado mmiliki halali ni Istiqama. Pamoja na kwamba mmiliki huyo hatoweza kufanya chochote katika eneo hilo kuwa shauri hilo lipo Mahakamani.
- (b) Mhe. Spika, serikali haijatoa umiliki wa eneo hilo kwa taasisi mbili. Aidha, Kampuni ya *MECCO* iliomba serikali kupatiwa sehemu ya kuchimba mawe magumu kwa ajili ya maendeleo ya ujenzi wa barabara katika Kisiwani cha Pemba. Hivyo hadi hivi sasa serikali haijatoa hati nyengine ndani ya eneo hilo husika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwanza nimpe pole kwa kuumwa karibu siku tatu nne hatujamuona hapa waziri wake dhamana akawa anajibu maswali ya wananchi, naomba kuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza. Kigezo gani mllichokitumia kufutia Istiqama na sheria zenu za ardhi nafikiri mkakaa na wanasheria wenu mkayazingatia kwanza kabla ya kumfutia mniamwita yule mtu ndipo mniamfutia, kigezo gani au baada ya kumfutia mmempa eneo jengine au hana haki mwananchi huyo. Hilo moja.

La pili, kwa kuwa dunia hivi sasa inapigania sana hifadhi ya mazingira kwa nini maeneo hayo yanapochimbwa vifusi hadi leo hii yanaendelea kubaki bila kuchukuliwa hatua ya kuyahifadhi na badala yake kuchimbwa vifusi katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, unapopewa ardhi kuna muda maalum unaotakiwa uwe umeshaiendeleza. Kusema kweli hatua iliyotaka kuchukuliwa katika ardhi hii palikuwa hapajaendelezwa, ardhi ni kubwa na ilikuwa imejengwa banda la mabatisio nyumba ya kisasa kama alivyosema msemajji.

Kwa hivyo, ikaonekana kwamba hii ardhi hajaitumia hivyo hapo keshafanya kosa kwa sababu tayari anayo ardhi mkononi kwa muda wa miaka sita hajaiendeleza wakati miezi 30 imeshavuka katika miaka sita. Hilo ni moja.

La pili, hifadhi ya mazingira. Hifadhi ya mazingira sio kwamba Idara ya Mazingira inakataza kutafuta mawe magumu mwahala isipokuwa inataku ufile katika kiwango maalum katika kuchimba kwako, usiende chini sana. Sasa *MECCO* wamepewa kazi ya kujenga barabara, Baraza hili lilikuwa likilalamika sana juu ya habari ya barabara zile za Pemba kwamba hazijajengwa, sasa wao wakaona mawe magumu kwa ajili ya kutengeneza kokoto za barabara ile yanapatikana Vitongoji mahala ambapo tangu zamani palikuwa pakifanywa shughuli hiyo.

Kwa hivyo, wakaomba kwenda kuvunja yale mawe magumu pale wapate kokoto nzuri kwa ajili ya kwenda kutengeneza ile barabara. Serikali ikaona sio jambo baya na hapa ndio serikali ilipogutuka kuona kwamba hii ardhi imekaa bila ya kutumiwa.

Huyu bwana sasa akataka iwe tunanunua mawe, sasa hapo ndipo ulipokuja wasiwasi tunajenga barabara kwa matumizi ya wananchi halafu tukanunue kwake, sisi hatukumpa ardhi ile kwamba auze mawe tumempa ardhi ajenge, hicho anachotaka kujenga hajakijenga anataka atuu zie mawe, ndio sababu tukaona huyu bwana sasa hivi anaanza kututawala kabisa katika ardhi yetu wenyewe tununue kitu wenyewe wakati ardhi ni mali ya serikali.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kama nimemfahamu vizuri Mhe. Waziri amesema kuwa Kampuni ya *MECCO* iliomba ruhusa ya kwenda kutumia mawei kwa sababu watapata kokoto ngumu na mawe hayo yaliikuwa yanafaa kwa kazi hiyo. Lakini kwa sababu swali mama linasema kuwa taasisi hiyo vile vile wamepewa Kampuni ya Ujenzi ya *MECCO* na tayari wameshaanza kuweka mashine (*crusher*) wameshaanza kuchimbua kifusi pamoja na kupasua miamba, kunakoathiri sana jengo la mmiliki huyo.

Kwa hiyo, kwa sababu suala mama linasema kuna kupasua miamba na kuchukua kifusi wakati waziri hakutia neno kifusi. Je, ni yupi msema kweli, ni mwenye swali ambaye yuko katika mazingira yale au Mhe. Waziri aliyejibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, hiyo sehemu mimi naijua pamoja na kuwa siishi kule, mara nyingi ninapofanya uamuzi huwa ninajaribu kufuatilia. Kwa hivyo, ninachokisema ni hakika, pale mahala *crusher* ilikuwepo zamani na kwa bahati nzuri mimi nilisimamia ujenzi wa Uwanja wa Gombani *crusher* ilikuwepo pale, niliikuta mimi iko pale na nikatakiwa niitengeneze wakati mimi ni Waziri wa Habari nikaitengeneza *crusher* ile na tukapasua mawe, tukatengeneza kokoto kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Gombani ambaa sasa hivi tayari unatumika vizuri tu. Ujenzi wa Uwanja wa Gombani na huyo alitaka kwa nia hiyo hiyo.

Kwa hivyo, naeleza ile hali halisi, sikusudii kumsuta Mheshimiwa kwa sababu kumsuta Mheshimiwa ni kosa mana ni Mheshimiwa nimeeleza hali ninayoijua.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

TAARIFA

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwanza kumkaribisha Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kusoma bajeti.

Mhe. Spika, bajeti hii tuna utaratibu mpya wa *PBB* kama tulivyoiona na kama tulivyoanza jana, na tulielezwa kwamba utaratibu huu mpya ambao wengi kwetu sisi ni wageni, katika uwasilishaji wake utakuwa una mambo matatu.

Kwanza utakuwa una malengo, lakini pili kutakuwa kuna kitu programu, lakini mambo hayo mawili yatasaidiwa sana na kuwa na zile *activities*. Programu ni mafungu tumeyaona, malengo tumeyaona yamo kwenye kitabu hiki, lakini bahati mbaya sana Mhe. Spika, kwamba jana tulipitisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili bila ya kujua ule mnyambuliko wa zile shughuli zenyewe kimafungu.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba katika utaratibu huu ni sawa na kutufungia ngulai, kwa sababu tunapitisha fungu wakati tukijua hatujui fungu lile mnyambuliko wake utakuwa ni upi na Baraza lako baadae liridhie hilo.

Sasa kwa kuwa jana tulifanya hivyo basi naomba sasa Baraza lako tujipe fursa ili sisi Wajumbe ambao hatumo kwenye Kamati tuweze kuweza kujua *activities* za kila fungu zinazowasilishwa katika Baraza hili, ili tuwatendee wananchi haki katika matumizi ya fedha zao. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Sawa kabisa Mhe. Omar Ali Shehe na suala hili tulikubaliana mpaka kwenye semina ambapo kwa bahati mbaya baadhi yetu wengi tulikuwa hatukuweza kuhudhuria kwa sababu maalum. Sasa tulichokubaliana ni kwamba zile *list of activities* kwa kila wizara inapowasilisha hotuba yake basi zitakuwa zinatolewa, hazitatolewa kwa wote, lakini kutakuwa na *copy* ambazo yule ambaye anataka ku-refere mapema anaweza akapata. Jana suala hilo pia tulilizingatia na nikaambiwa kwamba leo hizo *activities* kwa kila wizara ambayo itakuwa inawasilisha hoja yake itakuwa zinawekwa, ili Waheshimiwa Wajumbe wapate kuzipitia.

Sasa naelewa kwamba ofisi ya katibu itaandaa utaratibu ili *activities* hizo zinazohusiana na *programme* na *sub programm* mbali mbali zitakuwa zipo ili Wajumbe wapate kuzipitia na waweze kujuwa na kutambua huo mnyambuliko wa mambo mbali mbali yanayohusiana na *sub programme* na *programme* zenyewe.

Kwa hiyo, ofisi ya katibu ishughulike na hilo na nadhani pengine pahala muwafaka itakuwa pale pale kwa watendaji hapo nyuma ili Wajumbe tuweze kufanya *reference* ya hizo *activities* kwa kila *programme* na *sub program*. Kwa hiyo, ofisi ya katibu ifanye hiyo kazi.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili, kuchangia na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kukutana kwa lengo la kujadili hotuba hii ya OMKR.

Namuomba Mwenyenzi Mungu atuwezeshe kukamilisha vizuri miaka mitano ya awamu hii ya saba tukimalizia uwasilishaji wa hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuwa karibu nasi kwa muda wote katika utendaji wa kazi za ofisi yetu. Hakika ukaribu wake huo tunauthamini sana maana umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kuwashudumia wananchi bila ya hofu na kwa mafanikio.

Mhe. Spika, vile vile sina budi kuwapongeza viongozi wetu wa kitaifa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa jitihada zao za kumsaidia Mhe. Rais katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, natoa shukurani na pongezi maalumu kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa uongozi wake imara. Miongozo na ushauri wake anaotupa katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa masuala mtambuka yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais umekuwa ni chachu kwa mafanikio tuliyoyapata. Kwa niaba ya wafanyakazi wote

wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, tunaahidi kuendelea kushirikiana naye ili kuleta maendeleo kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa namna ya kipekee naomba nikupongeze wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako wakiwemo Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza vyema.

Mhe. Spika, namshukuru Mwenyeekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Hamza Hassan Juma, pamoja na wajumbe wote wa kamati yake kwa kushirikiana nasi bega kwa bega katika kuhakikisha tunafanikisha utekelezaji wa malengo ya ofisi yetu. Naishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Hesabu za Serikali chini ya Mwenyeekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa mashirikiano mema na ofisi yetu.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu kwa mashirikiano yao ya dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa ofisi yetu tukiwa ndani ya Baraza na hata katika majimbo yao. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie uchaguzi wa salama na atuwezeshe kukutana tena katika awamu ijayo. Aidha, nachukua nafasi hii kuwatakiwa wote mafanikio mema katika uchaguzi unaokuja.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu. Vile vile napenda kuwashukuru kwa dhati Afisa Mdhamsini wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa juhud, bidii na ustahamilivu mkubwa katika kutekeleza majukumu yao ya kazi na kuleta ufanisi na tija kwa taifa letu.

Mhe. Spika, katika mvua zinazoendelea za masika za mwaka huu ndani ya nchi yetu, mwanzoni mwa mwezi wa Mei tumeshuhudia mvua katika kiwango kikubwa ambacho hakijawahi kutokea kwa miongo ya hivi karibuni.

Mhe. Spika, mvua hizo zimesababisha maafa mbali mbali yakiwemo kupoteza maisha kwa wananchi wetu na uharibifu wa makaazi na miundombinu uliotokana na mafuriko katika maeneo mbalimbali ya visiwa yetu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru viongozi na wananchi wote kwa jumla kwa mashirikiano waliyoonesha katika kukabiliana na maafa hayo. Aidha, naomba nitoe mkono wa pole kwa wafiwa na waathirika wote, nawaomba wawe na moyo wa subira katika mtihani huo na kufahamu kuwa hiyo ni kazi ya *Allah*.

Serikali itaendelea kuwa pamoja na wananchi katika kukabiliana na changamoto hizo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais napenda kutoa mkono wa pole kwako Mhe. Spika na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, familia pamoja na wananchi wa Jimbo la Magomeni kwa kuondokewa na Mwakilishi wao mpendwa marehemu Salmin Awadh Salmin. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi. Amin.

MALENGO MAKUU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kusimamia na kuratibu Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, mipango, sera na utafiti, uendeshaji na utumishi, masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, masuala ya watu wenye ulemavu, udhibiti wa dawa za kulevyta na muitiko wa taifa wa kupambana na UKIMWI. Katika kutimiza jukumu hili, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imekuwa na malengo makuu yafuatayo:-

1. Kuratibu na kusimamia shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuratibu mipango, sera na utafiti unaohusiana na maeneo ya majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
3. Kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira na kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi.
4. Kuimarisha na kutetea uzingatiaji wa haki na fursa sawa kwa watu wenye Ulemavu ndani ya jamii.
5. Kuratibu na kudhibiti usafirishaji, uingizwaji, matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevyta.
6. Kuratibu mwitiko wa taifa juu ya kinga dhidi ya UKIMWI na kupunguza athari kwa jamii.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatekeleza majukumu yake kupitia taasisi zifuatizo:-

1. Ofisi ya Faragha
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
4. Idara ya Mazingira
5. Idara ya Watu wenye Ulemavu
6. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba
7. Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta
8. Tume ya UKIMWI

Mhe. Spika, kufuatia kupitishwa na kusainiwa kwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2015, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2015/2016 inategemea kuwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (*Zanzibar Environmental Management Authority – ZEMA*) ili kuongeza nguvu katika utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa mazingira, Zanzibar.

MUHTASARI WA MAFANIKO NA CHANGAMOTO ZA OMKR KWA MIAKA MITANO (5)

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeanzishwa mwaka 2010 mara baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2010. Tokea kuanzishwa kwake, pamoja na kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, pia ilijikita katika kutayarisha nyenzo ambazo zitasaidia kufanya kazi kitaalamu na kwa ufanisi zaidi kwa miaka kadhaa ijayo.

Mhe. Spika, kwa kuwa kipindi cha miaka mitano kimepita tokea kuanzishwa kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na hasa kwa vile tunamaliza bajeti ya awamu hii, naomba nieleze kwa muhtasari baadhi ya mafanikio ya msingi yaliyopatikana na ofisi yetu.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeweza kuratibu kwa ufanisi mkubwa shughuli za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais zikiwemo safari za ndani na nje ya nchi ambapo miongozo kwa taasisi mbali mbali imetolewa ikiwa ni sehemu ya kuyatafutia ufumbuzi matatizo ya kijamii pamoja na kufanikisha usimamizi wa masuala yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Aidha, uratibu wa mikutano kati ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mabalizi waliopo nchini, viongozi wa nchi na mashirika mbali mbali ya kimataifa ulifanyika kwa ufanisi mkubwa ambapo pamoja na mambo mengine mikutano hiyo imekuza mahusiano kati ya Zanzibar na nchi au mashirika hayo.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo, Ofisi ya Faragha imekuwa na changamoto ya msingi iliyodumu ndani ya kipindi cha miaka mitano ambayo ni kukoseka kwa makaazi rasmi ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais huko Dar-es-Salaam. Hali hiyo imemlazimisha kufikia hoteli, jambo ambalo limepelekea kuwa na gharama zaidi.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeandaa Mpango Mkakati kwa kipindi cha 2014 – 2020 na Mpango Mkuu wa Utafiti kwa kipindi kama hicho kwa masuala yanayoratibiwa na ofisi yetu. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pia imeandaa muongozo wa uzingatiaji pamoja na mfumo wa ufuatilaji na tathmini kwa mambo mtambuka yanayosimamiwa na ofisi yetu.

Mhe. Spika, ni jukumu la taasisi na wadau wengine kuutumia muongozo huo na mingine ya kisekta iliyoandaliwa katika kuhakikisha mambo mtambuka yakiwemo ya mazingira, masuala ya Watu wenyewe Ulemavu na UKIMWI yanazingatiwa katika mipango yao mbali mbali.

Mhe. Spika, katika sekta ya mazingira, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeandaa sera ya mazingira ya mwaka 2013, Mkakati wa Zanzibar wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa mwaka 2014, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015, Mkakati wa Mawasiliano ya Mazingira, Mkakati wa Mawasiliano wa Mabadiliko ya Tabianchi, Muongozo wa Uzingatiaji wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa sekta mbalimbali pamoja na kanuni za mifuko ya plastiki na maliasili zisizorejesheka. Jumla ya Tathmini 71 za Athari za Kimazingira zimefanyika na kutolewa yeti vya mazingira kwa miradi hiyo.

Aidha, wananchi 8,000 wa kijiji cha Nungwi wamepatiwa maji safi na salama ambao kwa muda mrefu maji yao yalikuwa na chumvi-chumvi kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Spika, mafanikio mengine katika sekta ya mazingira ni kukua kwa uelewa wa masuala ya mazingira katika jamii ambapo kamati, vikundi na asasi zisizokuwa za Kiserikali mbalimbali zimeundwa ndani ya jamii kwa lengo la kusaidia usimamizi wa mazingira nchini. Aidha, kupungua kwa matumizi ya mifuko ya plastiki ndani ya Zanzibar ni mafanikio ya kupigiwa mfano yaliyofikiwa na Afisi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado sekta ya mazingira inakabiliwa na changamoto za kuwepo kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika, katika masuala ya Watu wenyewe Ulemavu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeweza kufanya usajili wa Watu wenyewe Ulemavu katika Mikoa yote mitano ambao utaiwezesha Serikali kuwatambua walipo pamoja na kuzingatia mahitaji yao katika mipango ya maendeleo.

Aidha, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeanzisha Mfuko wa Watu wenyewe Ulemavu kwa lengo la kudumisha utoaji wa huduma kwa watu hao, kuandaa rasimu ya sera ya Watu wenyewe Ulemavu ambayo inatarajiwa kuwasilishwa Serikalini hivi karibuni. Aidha, watu 281 wenyewe ulemavu wamepatiwa visaidizi na dawa ili pamoja na mambo mengine kurahisisha shughuli zao za kimaisha.

Mhe. Spika, pamoja na juhudhi hizo, Serikali inakabiliwa na changamoto za kuwepo kwa udhalilishaji kwa Watu wenyewe Ulemavu hasa wenyewe ulemavu wa akili pamoja

na baadhi ya wadau na jamii kutozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu katika mipango yao.

Mhe. Spika, katika sekta ya UKIMWI, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imetayarisha Mkakati wa Pili wa Taifa wa Ukimwi Zanzibar kwa kipindi cha 2011 – 2016 na Sheria ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI ya mwaka 2013. Sheria hii itaondoa unyanyapaa pamoja na kuimarisha haki za binadamu kwa kuwalinda walioambukizwa na wasioambukizwa na Virusi vya Ukimwi. Aidha, Tume imeandaa Mkakati wa Utafutaji wa Rasilimali kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa shughuli za UKIMWI.

Mhe. Spika, pamoja na juhudhi hizo ambapo pia kumekuwa na kupungua kwa unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU, sekta hii ya UKIMWI inakabiliwa na changamoto ya kupungua kwa upatikanaji wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo hali inayokwaza juhudhi za mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mhe. Spika, katika kushughulikia tatizo la dawa za kulevyta, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imefanya mapitio ya Sheria ya Udhhibitwa Dawa za Kulevyta ya mwaka 2009 ambayo yamepelekea kuundwa kwa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhhibitwa Dawa za Kulevyta. Aidha, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeandaa muongozo kwa ajili ya uanzishwaji wa nyumba za makaazi ya vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevyta. Hivi sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa wanaotumia dawa za kulevyta ambacho kinahitajika sana katika kukabiliana na tatizo la dawa hizo hapa nchini.

Mhe. Spika, pamoja na kuimarika kwa mashirikiano mionganoni mwa taasisi wadau katika suala la udhibiti wa dawa za kulevyta, bado Serikali inakabiliwa na changamoto za kuwepo kwa uingizwaji na usambazwaji wa dawa hizo unaopelekea kuendelea kwa matumizi yake hapa Zanzibar.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA OMKR KWA MWAKA 2014/2015

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Spika, Afisi ya Faragha ina jukumu la kuratibu shughuli za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Afisi ya Faragha ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuimarisha mazingira ya kazi katika kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2015, Afisi ya Faragha imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyopanga:-

Mhe. Spika, katika kuimarisha mashirikiano ya kijamii na kiuchumi, Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais amefanya ziara 4 za nje. Aidha, ziara mbali mbali za ndani ya nchi zilifanyika na ripoti za ziara hizo kuwasilishwa sehemu husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kwa upande wa ziara za ndani miongozo mbali mbali imetolewa kwa taasisi na jamii zilizo tembelewa.

Mhe. Spika, wageni 25 kutoka nje ya nchi walipata kuonana na Mhe. Makamu wa Kwanza na kubadilishana mawazo juu ya mambo mbali mbali yanayohusu uchumi, kijamii na mazingira. Vile vile, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ameonana na wageni wa ndani na kubadilishana mawazo juu ya mambo mbali mbali ya kijamii na ushauri wa mambo hayo umetolewa. Sambamba na hayo, katika kusaidia shughuli za kiuchumi na kimaendeleo Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais amesaidia jumuiya na vikundi vya jamii.

Mhe. Spika, katika kukuza mawasiliano na upatikanaji wa taarifa kuhusiana na utekelezaji wa shughuli za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, jumla ya kalenda 2,000 za mwaka 2015 zenye ujumbe mbali mbali zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Ununuzi wa vifaa mbalimbali vya habari umefanyika na kuongeza utoaji wa habari za Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mazingira ya kazi na ya wafanyakazi wa Afisi ya Faragha, matengenezo madogo ya Afisi ya faragha na nyumbani kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais yamefanyika. Vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya afisini na nyumbani vimenunuliwa.

Mhe. Spika, Afisi ya Faragha kwa mwaka wa fedha 2014/15 ilikadiria kutumia T.Shs.411,150,000/- kwa kuendeshea kazi. Hadi kufikia Machi, 2015 ilikwisha kuingiziwa T. Shs.143,902,500/- sawa na asilimia 35.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo; kuratibu shughuli za utafiti pamoja na kufuatilia na kutathmini utekelezaji kwa taasisi zote zilizo chini ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kujenga uwezo wa utafiti kwa watendaji 20 na kufanya tafiti tatu katika maeneo ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka ya Afisi.
3. Kuratibu shughuli za sera, mipango na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2015 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyopanga:-

Mhe. Spika, mafunzo ya utafiti ya siku tano kwa wafanyakazi wa Afisi yalitolewa. Mafunzo hayo yaliwashirikisha watendaji 30 kutoka Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na yalilenga kuwawezesha watendaji kutumia matokeo ya utafiti katika kupanga na kufuatilia mipango ya kila siku.

Mhe. Spika, utafiti wa kimazingira unaohusu masuala ya athari na kiwango cha uingizaji wa vifaa chakavu vya umeme na elektroniki yaani *E-waste* umefanyika na ripoti yake itawasilishwa kwa wadau hivi karibuni.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha sekta zinazingatia masuala mtambuka yanayosimamiwa na Afisi yetu ndani ya mipango yao ya kimaendeleo, mafunzo ya siku tatu ya wakufunzi yalitolewa. Mafunzo hayo yalihusu utekelezaji wa muongozo wa mambo mtambuka ulioandaliwa na Afisi na kuwashirikisha watendaji 25 kutoka katika sekta mbali mbali za serikali.

Mhe. Spika, taarifa mbali mbali za utekelezaji za robo mwaka na za mwaka zimeandaliliwa na kuwasilishwa sehemu husika ikiwemo Tume ya Mipango, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Fedha na taasisi nyengine kila ilipohitajika.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2014/15 iliidhinishiwa kutumia T. Shs. 146,065,000/- kwa kuendeshea kazi. Hadi kufikia Machi, 2015 ilikwisha kuingiziwa T. Shs. 51,819,000/- sawa na asilimia 35.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliratibu utekelezaji wa miradi (2) ya maendeleo kama ifuatayo:-

- a) Mradi wa kujenga Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kwa mwaka wa fedha 2014/15 ulilenga kukamilisha ujenzi wa sehemu ya chini, hadi kufikia Machi 2015 ujenzi wa msingi pamoja na uwekaji wa jamvi umekamilika.

Mhe. Spika, mradi huu kwa mwaka wa fedha 2014/15 uliidhinishiwa kutumia T.Shs.1,400,000,000/-. Hadi kufikia Machi, 2015 ilikwisha kuingiziwa T. Shs. 250,000,000/- sawa na asilimia 18.

b) Mradi wa kujenga uwezo wa utekelezaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo *UNDP* kuititia programu ya *UNDAP*. Mradi huu unatekelezwa kuititia malengo saba ambapo malengo manne kati ya hayo yanatekelezwa na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Malengo hayo ni:-

- i. Kuhakikisha masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi yanaingizwa katika mipango ya maendeleo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa MKUZA II.
- ii. Kutayarisha Mkakati wa Zanzibar wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na kusaidia utekelezaji wake.
- iii. Kuimarisha muundo wa kitaasisi kwa ajili ya kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi.
- iv. Kukuza kiwango cha upatikanaji wa taarifa na uelewa juu ya athari za mabadiliko na mikakati ya kukabiliana nayo mionganoni mwa jamii na Taasisi za Serikali.

Mhe. Spika, malengo mengine matatu ya mradi huu yanatekelezwa kuititia Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Aidha, jumuiya ya Maendeleo ya Jamii na Uhifadhi wa Mazingira Zanzibar *CODECOZ* nayo inashiriki katika utekelezaji wa mradi huu kwenye lengo moja la kukuza kiwango cha upatikanaji wa taarifa na uelewa juu ya athari za mabadiliko na mikakati ya kukabiliana nayo mionganoni mwa jamii na taasisi za Serikali.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2015 Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuititia mradi huu imeweza kutekeleza yafuatayo:-

Mhe. Spika, rasimu za mipango kazi ya kisekta ya kuzingatia mabadiliko ya tabianchi zimetayarishwa. Sekta zilizohusika na utayarishaji huo ni Uvuvi, Miundombinu, Utalii na Kilimo.

Mhe. Spika, hekta 30 za mikandaa zimepandwa katika maeneo sita ya Unguja na Pemba. Maeneo hayo ni Kiongwe, Mafufuni na Kisakasaka kwa Unguja na Ndagoni, Wambaa na Pujini kwa Pemba.

Mhe. Spika, ripoti ya ukusanyaji wa taarifa za msingi za kutayarisha mpango wa jamii wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi imetayarishwa na inategemewa kuwasilishwa kwenye vikao vya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mapitio na kuridhiwa.

Mhe. Spika, hatua za utayarishaji wa Mpango kazi wa Utekelezaji Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi zimeshaaza na utayarishaji wa mpango huo unategemewa kumalizika mwezi Januari, 2016 kwa hatua za uhamasishaji wa nyenzo za utekelezaji.

Mhe. Spika, watendaji wawili kutoka Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais waliwezesha kuhudhuria mukutano wa 20 wa Dunia wa mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Lima, Peru na mashirikiano ya wadau mbalimbali wa mabadiliko ya tabianchi wa nje ya nchi yameongezeka.

Mhe. Spika, vipindi 6 vya elimu ya athari mabadiliko ya tabianchi vilitayarishwa na kurushwa kuptitia redio jamii za Micheweni, Makunduchi na Tumbatu. Uelewa wa jamii juu ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi umeongezeka.

Mhe. Spika, Wajumbe 5 kutoka Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Idara ya Ushirika na Asasi ya kiraia ya wamepatiwa safari ya kimasomo huko Arusha Tanzania Bara kujifunza utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya jamii ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 mradi huu ulidhinishiwa kutumia T.Shs.577,500,000/. Hadi kufikia Machi, 2015 mradi ulikwisha kuingiziwa T.Shs 245,620,000/- sawa na asilimia 43.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji na utumishi zikiwemo sheria na kanuni za utumishi, mafunzo, maslahi na maendeleo ya wafanyakazi.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia, kukuza na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kuleta ufanisi.
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2015, Idara imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyopanga:-

Mhe. Spika, katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi vifaa mbali mbali vimenunuliwa pamoja na huduma mbali mbali za ofisi zimetolewa.

Mhe. Spika, katika kushiriki mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, wafanyakazi 23 wamewezeshwa kushiriki katika mikutano ya ndani kwa ajili ya kufuutilia wa shughuli za Ofisi (Pemba, Dar-es-Salaam na Dodoma) na 9 wamewezeshwa kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa nje ya nchi (Kenya, Malaysia, Qatar, Lima na Singapore). Safari hizi zimeongeza mahusiano na washirika wa maendeleo.

Mhe. Spika, taarifa mbali mbali zinazohusiana na majukumu ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais zimetolewa kupitia vyombo vyya habari na mitandao ya kijamii, makala 2 zenye maudhui yanayohusu mabadiliko ya tabianchi na sheria ya mazingira zimetolewa katika gazeti la Zanzibar Leo. Aidha, filamu fundishi 2 kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi moja ikiwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiengereza zinazohusu mabadilko ya tabianchi zimetayarishwa.

Mhe. Spika, wafanyakazi 33 wamesaidiwa gharama za ada na vifaa na kupatiwa fursa za mafunzo katika ngazi za Cheti, Stashahada, Shahada ya kwanza na ya pili, pamoja na shahada ya uzamili katika fani tofauti (Angalia Kiambatanisho Nam. 1).

Mhe. Spika, katika kusimamia ufanisi wa utendaji wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, vikao viwili vyya kamati ya uongozi vimekaa na kujadili rasimu ya sera ya watu wenye ulemavu, mkakati wa mawasiliano ya mabadiliko ya tabianchi pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji wa kazi za maabara ya utalii zinazotekeliza na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Aidha, kikao kimoja cha zabuni kilichojadili kumpata mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha marekebisho ya tabia kimefanyika. Vilevile, ripoti ya fedha ya mwaka 2013/2014 imetayarishwa na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa kutumia TZS 1,610,084,000/-. Kati ya fedha hizo, TZS 320,084,000/- kwa ajili ya matumizi mengineyo, na TZS 1,290,100,000/- kwa ajili

ya mishahara. Hadi kufikia Machi, 2015 Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilikwisha kuingiziwa TZS 1,110,748,833/- zikiwemo TZS 173,444,933/- kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 54, na TZS 937,303,900/- kwa mishahara ambazo ni sawa na asilimia 73.

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ndio Idara pekee iliyoingiziwa fedha zaidi ya asilimia 50 kwa vile kazi zake nyingi zinajumuisha kuzihudumia Idara zote ikiwemo mafunzo kwa wafanyakazi wote, huduma za jingo na utekelezaji na usimamizi wa vikao vyote kwa misingi ya utawala bora.

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kukusanya na kuhifadhi taarifa za kimazingira, kutoa taarifa za kimazingira ili ziweze kusaidia katika kutayarisha na kutekeleza mipango na miradi ya kimaendeleo, kufuatilia mwenendo wa hali ya kimazingira, kukabiliana na matatizo ya kimazingira, kuhamasisha wadau kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira pamoja na kutoa elimu ya mazingira kwa jamii. Aidha, Idara hii pia inajukumu la kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Mazingira ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Mazingira.
2. Kusimamia uingizwaji wa masuala ya mazingira katika miradi ya maendeleo.
3. Kukuza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2015, Idara ya Mazingira imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyopanga:-

Mhe. Spika, jumla ya operesheni 33 za uzuaijti matumizi ya mifuko ya plastiki zimefanyika (Angalia Kiambatanisho Nam. 2). Katika operesheni hizo, watu 23 wamekamatwa na kupelekwa mahakamani na kutozwa faini ya jumla ya TZS 3,170,000/. Aidha, wastani wa kilo 759 za mifuko ya plastiki zimekamatwa na kuweza kuangamizwa. Vile vile jumla ya operesheni ishirini na saba zimefanyika Unguja na Pemba za kuwakamata wanaovuna na kusafarisha kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015 imepitisha na Baraza lako Tukufu katika kipindi hichi cha mwaka 2014/2015. Ninapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kuipitisha sheria hiyo. Ni imani yetu ya Ofisi yetu kuwa sheria hiyo itasaidia sana kupunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira uliopo hivi na

kuongeza ufanisi wa kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Aidha, naomba pia nichukue nafasi hii kuliarifu Baraza lako kuwa Mhe. Rais ameshaisaini sheria hiyo.

Mhe. Spika, jumla ya miradi kumi na tatu imefanyiwa tathmini ya athari za kimazingira na kijamii na tayari ripoti za tathmini hizo zimefanyiwa mapitio ya wadau kwa uratibu wa Idara ya Mazingira. Kufuatia mapitio hayo miradi yote imepatiwa vyeti vya kuhifadhi mazingira na imetakiwa kuendelea na utekelezaji kwa kufuata masharti yaliyotolewa. **Tafadhali angalia kiambatisho Na. 3.**

Mhe. Spika, mafunzo ya aina mbili ya tathmini ya athari za kimazingira yamefanyika. Mafunzo hayo yaliwashirikisha watu arobaini kutoka taasisi mbali mbali za Kiserikali na zisizokiserikali ambayo yameongeza ujuzi na ufhamu wa tathmini ya athari za kimazingira na usimamizi na ufuatiliaji wa tathmini hizo.

Mhe. Spika, jumla ya vipindi kumi na tatu vimetayarishwa na kurushwa kupitia ZBC redio na TV. Vipindi kumi vya redio vilihu matumizi ya majimbo sanifu, vipindi viwili umuhimu wa umeme wa juu, vipindi viwili marufuku ya mifuko plastiki, vipindi mmomonyoko wa fukwe na vipindi viwili Kanuni za maliasili zisizorejesheka na matumizi endelevu ya maliasili zisizorejesheka. Aidha, vipindi viwili vya TV vinavyohusu matumizi ya majiko sanifu na umeme wa juu vimerushwa hewani.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mazingira iliidhinishiwa kutumia Shs.113,284,000/= kwa ajili ya kuendesha kazi hadi kufikia Machi, 2015 Idara ya Mazingira ilikwishaingiziwa Shs.44,274,000/= sawa na asilimia 39.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Ofisi ya Makamu wa Kwanza Rais iliidhinishiwa kukusanya Shs.10,500,000/= kupitia Idara ya Mazingira. Fedha hizi zinatokana na ada ya uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na vyeti vya mazingira. Kazi ambayo inategemea idadi ya miradi inayowasilishwa kutoka Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi au miradi ya maendeleo ambayo inastahili kufanyiwa tathmini hadi kufikia Machi, 2015, jumla ya Shs.8,700,000/= zimekusanywa ambayo ni sawa na asilimia 83.

Idara ya Watu Wenyewe Ulemavu

Mhe. Spika, Idara ya Watu Wenyewe Ulemavu ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia masuala mbali mbali yanayohusu watu wenye ulemavu ili kuhakikisha ujumuishwaji katika shughuli zote za kimaendeleo zikiwemo za kiuchumi na kijamii.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Watu Wenye Ulemavu ilitaka kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa sheria, Kanuni, miongozo kwa watu wenye ulemavu
- Kusimamia haki na fursa sawa na ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu
- Kuanzisha programu ya Makuzi ya awali ya maendeleo ya mtoto.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2015 Idara ya Watu Wenye Ulemavu imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Spika, rasimu ya sera ya watu ulemavu imeandaliwa na taratibu za kukamilisha rasimu mpango wa kazi kwa ajili ya utekelezaji wa sera hiyo zinaendelea ili kwa pamoja ziweze kuwasilishwa Serikalini. Mhe. Spika, kikao kimoja cha Baraza la Watu Wenye Ulemavu kimefanyika kujadili taarifa mbali mbali zinazohusiana na maendeleo na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, kikao kimoja cha Maafisa Waratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu kimefanyika. Kikao hichi utekelezaji wa masuala ya watu wenye ulemavu katika sekta mbali mbali ulijadiliwa. Vile vile mafunzo juu ya uwezeshaji wa watu wenye ulemavu na mkataba wa kimataifa wa haki na fursa za watu wenye ulemavu yametolewa kwa Maafisa Waratibu kumi na nne wa Wizara na Waratibu wa kumi wa Jumuiya zinazoshughulika na masuala ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, ziara kumi zimefanywa katika taasisi za Serikali na za binafsi kwa lengo la kuhamasisha masuala ya watu wenye ulemavu na kuzungumzia ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu katika sekta hizo. Vile vile safari moja imefanywa nchini Kenya na nne ndani ya nchi kwa lengo la kukuza mashirikiano juu ya utekelezaji wa programu zinazohusu masuala ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, waandishi wa habari ishirini wamepatia elimu na kujengewa uelewa juu ya masuala ya makuzi ya awali ya maendeleo ya mtoto mwenye ulemavu.

Mhe. Spika, mafunzo ya usimamizi wa fedha na uongozi kwa viongozi thalathini tano wa Jumuiya za watu wenye ulemavu yametolewa kwa lengo za kuzijengea uwezo na kuleta ufanisi katika kazi. Watu wenye ulemavu mia mbili na ishirini na tano wamepatiwa visaidizi vya aina mbali mbali ili pamoja na mambo mengine kuweza kurahisisha shughuli zao za kimaisha. **Tafadhali angalia Kiambatanisho Na 5 .**

Mhe. Spika, sambamba na hayo siku ya kimataifa ya watu wenye ulemavu imeadhimishwa ambapo maandhimisho ya mwaka huu yamefanyika Kisiwani Pemba kwa kufanyika shughuli mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuielimisha jamii juu ya haja ya kuzingatia haki za watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2014/2015, iliidhinishiwa kutumia jumla Shs.278,442,000/= kwa kuendesha kazi hadi kufikia Machi, 2015 ilikwisha kuingiziwa Shs.100,724,500,000/= sawa na asilimia 36.

Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi Kuu Pemba ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi
- Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi
- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza Rais Pemba
- Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2015 Ofisi Kuu Pemba imeweza kuyatekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia.

Mhe. Spika, ziara zote za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais huko Pemba na ziara mbili za Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa zimeratibiwa. Ziara hizo zimeweza kuishauri Ofisi juu ya utekelezaji wa majukumu yake pamoja na kukagua shughuli mbali mbali zinazofanywa na jamii.

Mhe. Spika, katika jitihada za kupunguza athari na uharibu wa mazingira, ziara nane za ukaguzi zimefanywa kwenye maeneo yanayotumika kwa uchukuaji wa maliasili zisizorejesha kama vile mchanga, mawe na kifusi.

Maeneo yaliyokaguliwa ni Ging'ingi, Mwambe, Mkanyageni, Kiongoni, Ole, Pujini, Uwandaji na Mvumoni Tunduuwa.

Mhe. Spika, katika kuwajenga uwezo wafanyakazi gharama za mafunzo ya usimamizi wa mazingira zimelipiwa kwa mfanyakazi mmoja anayesoma katika Chuo Kikuu cha Dodoma ngazi ya shahada ya pili. (**Angalia Kiambatanisho**

Nam. 1). Hatua hiyo ni sehemu ya jitihada za kukuza na kuimarisha ufanisi za kiutendaji.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi jengo la Idara ya Mazingira Pemba limeezekwa. Ofisi Kuu imeweza kununua gari na vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2014/2015, iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shs.369,575,000/. Kati ya fedha hizo Shs.159,575,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shs.210,000,000/= kwa ajili ya mishahara hadi kufikia Machi, Ofisi Kuu Pemba imeingiziwa Shs.251,169,450/= zikiwemo Shs.77,100,000/= sawa na asilimia 48 kwa matumizi mengineyo na Shs.174,069,450/= kwa mishahara ambazo ni sawa na asilimia 83.

Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta

Mhe. Spika, Tume ya Taifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta ina jukumu la kuratibu mapambano dhini ya matumizi, biashara na usafirishaji wa dawa za kulevyta kwa kushirikiana na wadau mbali mbali, kutoa huduma kwa jamii juu ya athari za dawa kulevyta na kutoa huduma za tiba na ushauri nasaha kwa watumiaji wa dawa za kulevyta.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Kitaifa Kuratibu na Udhibiti wa Dawa Kulevyta ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kupunguza matumizi ya dawa za kulevyta
- Kupunguza usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevyta
- Kuweka mazingira bora ya kazi pamoja na kuleta ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevyta

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2015 Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia.

Mhe. Spika, jumla ya vipindi viwili vyta redio zimerushwa kupitia ZBC redio kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya athari ya dawa za kulevyta. Ziara za utoaji taaluma kuhusu athari za dawa kulevyta zimefanywa kwenye skuli arobaini na mbili ambapo wanafunzi elfu mbili, mia nane na sita walipatia taaluma hiyo.

Vile vile ziara kama hizo zimefanyika katika Shehia thalathini Unguja na Pemba. Aidha, nyumba 10 za makaazi wa vijana walioacha dawa za kulevyta zimepatiwa ruzuku (**Angalia Kiambatanisho Nam.7**) ambapo viongozi wa nyumba hizo walifanyiwa mikutano na kupewa taaluma juu ya ugawaji wa vifaa vyta kutendea

kazi viliviyotoka Taasisi ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (*UNODC*).

Mhe. Spika, katika kupunguza usafirishaji na usambazaji wa dawa kulevya Tume imetoa mafunzo ya sheria ya kulevya kwa taasisi za Serikali na Unguja na Pemba zikiwemo Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, Mahakama, Mamlaka ya Viwanja vyta Ndege, Bandari, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Bodi ya Mapato Zanzibar na Taasisi na Kupambana na Kuzuiwa Rushwa.

Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kujadili changamoto za kesi za dawa kulevya na kuimarisha mahusiano ya kisekta. Mhe. Spika, mkakati wa pamoja kati ya viongozi wa Tume, Wilaya, Shehia na wadau wengine juu ya kudhibiti uingizwaji, usambazaji na matumizi ya dawa kulevya katika Shehia umeandalisha na utekelezaji wake umepelekea kuvunjwa kwa vijiwe na kusambaratishwa kwa maeneo yanayofanyiwa biashara ya dawa kulevya yaliomo kwenye Shehia husika na kuunda Kamati za Udhibiti wa Dawa za Kulevya za Shehia hizo.

Pia kikao kimoja kimefanyika ili kutathmini na kujadili changamoto na mafanikio mbali mbali yaliyojitezea katika kufanikisha kazi ya uratibu na udhibitiwa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, wafanyakazi watano wamepatiwa mafunzo ya mfupi ya utunzaji wa kumbukumbu na mfanyakazi amelipiwa sehemu ya gharama za mafunzo ya utawala shahada ya pili.

Mhe. Spika, Tume ya Kitaifa Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2014/2015 iliidhinishiwa kutumia jumla Shs.364,000,000/= kati ya fedha hizo Shs.220,000,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shs.144,000,000/- kwa ajili ya mishahara hadi kufikia Machi, 2015 Tume ilikwisha kuingiziwa Shs.269,920,950/= zikiwemo Shs.162,138,000/= kwa matumizi mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 74 na Shs.107,782,950/= kwa mishahara ambayo ni sawa na asilimia 75.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Spika, majukumu makuu ya Tume ya Ukimwi ni kuhakikisha kwamba sera na mikakati ya taifa ya kupiga vita Ukimwi zinatayarishwa na kutekelezwa, kutafuta raslimali zitakazotumika katika utekelezaji wa mutitiko wa kitaifa wa kupambana na Ukimwi, kuimarisha uwezo wa wadau katika kufanya kazi programu za Ukimwi na kuratibu shughuli zao, kushajihisha utoaji wa huduma za tiba na matunzo kwa watu walioathirika na kuathiriwa, kufuatilia na kutathmini

umakini na ufanisi wa utekelezaji wa mikakati, sera na muitiko wa kitaifa na kutoa taarifa zote zinahusiana na Ukimwi.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Ukimwi ilipanga kutekeleza malengo yafutayo:-

Kuongoza, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mkakati wa pili wa kitaifa wa Ukimwi kwa wadau wote, kuimarisha ubora wa taarifa zinazokusanywa pamoja na kufuatilia matumizi ya taarifa zinazotokana na utuutiliaji tathmini na utafiti wa programu za Ukimwi na pia kutoa miongozo na kuratibu masuala ya habari, utetezi na mawasiliano kuhusu Ukimwi ili kuchochea mabadiliko ya tabia katika jamii na makundi maalum. Na pia kuongoza pamoja na kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi wa Tume kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu wa masuala ya Ukimwi.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2015 Tume ya Ukimwi imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia.

Mhe. Spika, katika kukuza mawasiliano na habari, nakala 5,000 za Toleo la 18 na nakala 5,000 la 19 la Jarida la JIHADHARI lenye ujumbe tofauti wa mapambano dhidi ya Ukimwi vimechapishwa na kuweza kusambazwa kwa wadau mbali mbali.

Mhe. Spika, katika kutekeleza Mkakati wa Pili wa Taifa wa Ukimwi, Tume imeiwezesha kifedha Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto kwa ajili ya kutayarisha Mpango wa Utekelezaji wa miaka miwili (2015-2016) ambao utawawezesha kutekeleza programu ya kuzuia udhalilishaji wa kijinsia (*Gender Based Violence*).

Mhe. Spika, jumla ya watu 756 walio katika makundi maalum wameweza kufikiwa na kupatiwa ushauri nasaha wanaotumia dawa kulevyta, watu 6 wanaotumia dawa za kulevyta kwa njia ya kujidunga, 389 dada poa na 19 kaka poa. Miongoni mwao 138 waliweza kupima virusi vya Ukimwi ambapo watano kati yao waligundulika kuishi na virusi vya Ukimwi, watu 62 walipatiwa rufaa na kupelekwa katika vituo vya tiba kwa uchunguzi zaidi.

Mhe. Spika, jumla ya vipeperushi 4,200 vimechapishwa na kusambazwa kwa walifikiwa kupitia mikutano 16 iliyofanyika Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Zanzibar tumeungana na nchi nyengine duniani kuadhiminisha siku ya Ukimwi ambayo tarehe 1 Disemba, ya kila mwaka. Maadhimisho hayo yalifanyika kijiji cha Machomane, Wilaya ya Chake-Chake Pemba ambapo shughuli mbali

mbali za kilele zilifanyika ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha jamii juu ya mapambano dhidi ya Ukimwi.

Mhe. Spika, wafanyakazi watano wamelipiwa gharama za masomo katika ngazi ya shahada ya pili na stashahada katika fani tofauti. Wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya ufuatiliaji na tathmini. Aidha, safari 6 za ndani za ufuatiliaji zimefanyika ambazo zimeongeza uratibu na ufanisi wa kazi za Tume.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Ukimwi iliidhinishiwa kutumia jumla Shs.811,000,000/-, kati ya fedha hizo Shs.533,208,700/- kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shs.277,791,300/- kwa ajili ya mishahara, hadi kufikia Machi, 2015 Tume ya Ukimwi ilikwisha kuingiziwa jumla ya Shs.503,194,400/- Kati ya hizo Shs.258,789,946/- sawa na asilimia 49 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shs.244,404,454/- sawa na asilimia 88 kwa ajili ya mishahara.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Ukimwi ilitekeleza kazi mbali mbali zilizopatiwa fedha na washirika wa maendeleo. Fedha hizo ni kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (*UNFPA*), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*). Shughuli zilizotekelawa kupitia fedha hizo ni kama zifuatazo:-

(a) Utekelezaji wa kazi zilizofadhiliwa na *UNFPA*

Mhe. Spika, mikutano miwili ya wadau wa sheria kutoka taasisi mbali mbali imefanyika kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutetea masuala ya mapambano juu ya udhalilishaji wa kijinsia na kukinga maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi na kuangalia mapungufu yaliyoopo kiutekelezaji, kutoa mapendekezo na kuwezesha matumizi mazuri ya sheria zilizopo.

Mhe. Spika, katika kupunguza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, Tume imefanya mikutano minne kwa viongozi wa Dini yenye jumla washiriki 80 ambapo walihamasishwa juu ya mbinu bora za kukinga na kudhibiti maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa vijana pamoja na kupunguza vitendo vya ubakaji na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Spika, katika kufanya uhamasishaji ndani ya jamii juu ya kupinga vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto na kuimarisha mapambano dhidi ya Ukimwi, maagizo 19 yalifanyika katika Shehia 19 Unguja na Pemba.

Kwa Unguja Shehia hizo 10 ni Bumbwini, Kiongwe, Makufuni, Nyamanzi, Pwanimchangani, Ungujuakuu-kaebona, Kiwengwa, Mpapa, Chukwani, Ungujuakuu-tindini na Mbuzini.

Kwa Pemba ni Shehia 9 ni Wambaa, Wesha, Chumbageni, Pujini, Dodoo, Chachani, Bopwe, Mchangamdogo, Mzambarauni, Pujini-kibaridi.

Jumla ya wananchi wa 1,592 kutoka Shehia 10 za Unguja walifikiwa na jumla ya wananchi 2,250 kutoka Shehia 9 za Pemba wameweza kufikiwa. Kati ya hao wanaume ni 900 na wanawake 1,350.

Mhe. Spika, katika kuwasaidia watu wanaoishi na virusi nya UKIMWI, vikundi vitano (3 Unguja 2 Pemba) nya ujasiriamali nya wanawake wanaoishi na virusi nya UKIMWI, vimepatiwa fedha na misaada mbali mbali kwa ajili ya kuijendeleza (Angalia Kiambatanisho Nam. 8).

Mhe. Spika, jumuiya ya ZAYEDESA imepatiwa msaada wa kuimarisha kituo cha huduma rafiki cha vijana kilichoko Mkoani Pemba. Baada ya kuimarishwa kituo hicho, Jumuiya hiyo imeweza kuwatumia waelimishaji rika wake na kuwafikia watu 17 walio katika makundi maalum (dada poa 11, kaka poa 3 na watumiaji wa dawa za kulevyta 3).

Mhe. Spika, kuitia mikusanyiko ya kidini yenyenye lengo la kuimarisha maadili mema na kurekebisha tabia, ili kuweza kujikinga na maambukizo mapya ya UKIMWI, pamoja na kupunguza vitendo nya unyanyasaji wa kijinsia, Tume imeiwezesha Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) kufanya ziara 9 (5 Unguja na 4 Pemba) za uhamasishaji ambapo wanashelia 270 Unguja na 214 kwa Pemba waliweza kufikiwa.

Mhe. Spika, Vilevile vipindi 5 nya redio (3 ZBC na 2 redio Adhana) vilitayarishwa na kurushwa hewani, kwa ajili ya kutoa elimu ya mwitiko wa taifa wa mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mhe. Spika, mikutano 2 ya uratibu (1 Unguja na 1 Pemba) iliyowashirikisha viongozi wa dini, (kiislamu na kikiristo) iliyolenga kukemea vitendo nya udhalilishaji na unyanyasaji ilifanyika. Jumla ya viongozi wa kidini 50 (25 Unguja na 25 Pemba) walishiriki.

Mhe. Spika, shehia 20 (Unguja 9, Pemba 11) zinazotekeleza mpango shirikishi wa kuziwezesha jamii (*community capacity enhancement*) zimefanyiwa ufuatiliaji. Shehia hizo kwa Pemba ni Kiwani, Makombeni, Michezani, Chonga, Vitongoji, Nawara, Kiuyu Kigongoni, Msuka, Tumbe Mashariki, Tumbe Magharibi na

Kizimbani. Kwa upande wa Unguja Shehia hizo ni Tumbatu Jongowe, Tumbatu Uvivini, Tumbatu Gomani, Kiboje, Mkwajuni, Koani, Malindi, Mlandege na Nungwi.

a) Utekelezaji wa kazi zilizofadhiliwa na UNDP

Mhe. Spika, mikutano mmoja wenyewe washiriki 40 kutoka kamati za UKIMWI za shehia, sekta kuu za serikali, taasisi za kisheria, taasisi za kiraia, makundi maalum na taasisi za watu wenyewe ulemavu, ulifanyika Pemba kwa lengo la kuhakikisha ufanisi katika kuongeza uwezo wa programu za habari utetezi na mawasiliano kwa kuchochea mabadiliko ya tabia katika masuala ya UKIMWI.

Mhe. Spika, mikutano miwili ya uratibu imeandaliwa (1 Unguja na 1 Pemba). Jumla ya washiriki 40 (20 Unguja na 20 Pemba) walishiriki katika mikutano hiyo ambao ni waratibu wa shughuli za UKIMWI katika ngazi za wilaya, sekta kuu za serikali, jumuiya na sekta binafsi katika mapambano dhidi ya UKIMWI (ABCZ), Jumuiya ya Watu wanaoishi na VVU, taasisi za kiraia, mtandao wa waelimishaji rika katika makundi maalum.

b) Utekelezaji wa kazi zilizofadhiliwa na UNICEF

Mhe. Spika, Tume ya UKIMWI ilifanya ziara za kuwapitia wadau wanaofanyakazi na makundi maalum, kwa lengo la kutambua shughuli wanazofanya na changamoto wanazokabiliana nazo na kusaidia kupata ufumbuzi. Miiongoni mwa taasisi zilizotembelewa ni pamoja na kanisa la Anglicana, nyumba ya wanawake ya makaazi ya vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevyta, watu waliokuwa wakitumia dawa za kulevyta na wamepata nafuu (*Zanzibar recovery community*), mtandao wa watu walio katika makundi maalumu (*Key Population Network*), mokusanyiko wa vijana wa Zanzibar kwa ajili ya kupambana na UKIMWI (*Zanzibar Youth Forum*), na Jumuiya ya Kidini ya mapambano dhidi ya UKIMWI (*ZEYADA*). Aidha, mikutano wa robo mwaka kwa wadau wanaofanyakazi na makundi maalum ulifanywa na kutathmini mafanikio na changamoto mbali mbali wanazokabiliana nazo na namna wanavyozitatua.

Mhe. Spika, zoezi la kuzitambua na kuzifanya uhakiki asasi za kiraia zinazowalenga vijana katika maeneo ya UKIMWI na Afya ya uzazi limefanyika kwa Unguja na Pemba. Jumla ya asasi za kiraia 68 (Unguja 51, Pemba 17) zimetambuliwa na kati ya hizo asasi 36 tu ndio zimeonekana kuwa na uwezo wa kufanyakazi kitaalamu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume ya UKIMWI iliidhinishiwa kutumia jumla ya TZS 1,369,000,000/- kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Hadi kufikia Machi, 2015 Tume ya UKIMWI ilikwisha kuingiziwa TZS 633,427,500/- sawa na asilimia 46.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume ya UKIMWI iliidhinishiwa kutumia TZS 50,000,000/- ikiwa ni mchango wa serikali katika kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2015 hakuna fedha zilizopatikana.

MALENGO YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS, KWA MWAKA 2015/2016

Mhe. Spika, kama ilivyokwishaelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, serikali inaendelea kutekeleza mageuzi ya mfumo wa bajeti, kutoka katika bajeti inayotumia vifungu (*line item*) kwenda katika mfumo unaotumia programu (*Program Based Budget – PBB*).

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2015/2016, inakusudia kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kupitia Programu kuu saba (7) zifuatazo:-

- A. Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya tabianchi;
- B. Programu ya Usimamizi wa masuala ya Watu wenye Ulemavu;
- C. Programu ya Mipango na Utawala;
- D. Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevyा;
- E. Programu ya Mipango na Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu; Udhibiti wa Dawa za Kulevyा;
- F. Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI; na
- G. Programu ya Mipango na Utawala wa Tume ya UKIMWI (Angalia Kiambatanisho Nam. 9).

A. PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Mhe. Spika, programu hii itatekelezwa kupitia programu ndogo mbili (2) na matarajio yake ya muda mrefu ni kuimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

A.1. Programu ndogo ya Usimamizi wa Mazingira

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kufikia mazingira endelevu ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kuendeleza mazingira endelevu kwa jamii pamoja na kukuza uelewa wa jamii juu ya usimamizi wa mazingira.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na idadi ya kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira itakayotayarishwa; idadi ya mikutano ya kimataifa ya mazingira itakayohudhuriwa; idadi ya miradi ya wahisani itakayoanzishwa; idadi ya misaada ya kitaalamu itakayopatikana; idadi ya operesheni za kimazingira zitakazofanywa; idadi ya ziara za ufuutiliaji na ukaguzi wa kimazingira zitakazofanywa; idadi ya miradi itakayokaguliwa; idadi ya miradi itakayofanyiwa tathmini ya athari za kimazingira; idadi ya miradi itakayofanyiwa ukaguzi wa kimazingira; idadi ya vipindi vya radio na vipindi vya TV vitakavyorushwa; idadi ya vipeperushi na vijarida vilivyotayarishwa na kusambazwa; pamoja na idadi ya mikutano ya uhamasishaji itakayofanyika

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo ya Usimamizi wa Mazingira utafanywa kwa pamoja kati ya Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (*Zanzibar Environmental Management Authority – ZEMA*).

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 174,076,000/- kutoka Serikalini.

A.2. Programu ndogo ya Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuratibu na kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kutayarisha nyenzo na mipango ya usimamizi, kuratibu mikutano ya usimamizi, kujenga uwezo wa wadau, kukuza uelewa juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuzisaidia jamii katika kukabiliiana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na kuwepo kwa mpango kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko ya tabianchi utakaotayarishwa, kuwepo kwa utaratibu maalumu wa kifedha kwa ajili ya kugharamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi utakaoandaliwa, kuwepo kwa mfumo wa utayarishaji wa mipango wa kijamii ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi utakaotayarishwa, idadi ya maeneo yaliyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi yatakayoendelezwa, idadi ya taasisi zitakazosaidiwa kuingiza mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwenye programu za taasisi hizo, idadi ya taasisi zitakazosaidiwa kuanzisha vitengo vya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwenye taasisi hizo, idadi ya mikutano ya Kamati za mabadiliko ya tabianchi itakayofanyika, idadi ya wafanyakazi watakaosaidiwa kushiriki mafunzo mafupi na mikutano ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi, idadi ya mikutano, vipeperushi na programu za TV na redio za kuelimisha jamii na wadau juu ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi zitakazotayarishwa na idadi ya majiko sanifu yatakayotengenezwa na kutumika.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo ya Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi utafanywa na Idara ya Mazingira, Wizara ya Kilimo na Maliasili kuitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, Wizara Fedha kuitia Idara ya Fedha za Nje, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuitia Idara ya Nishati na Madini na Jumuiya ya Maendeleo ya Jamii na Uhifadhi wa Mazingira Zanzibar (*Community Development and Environmental Conservation in Zanzibar CODECOZ*) na utaratibiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla **ya TZS 450,000,000/-** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya TZS 624,076,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Kati ya hizo TZS 174,076,000/- kutoka Serikalini na TZS 450,000,000/- kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

B. PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, programu hii itatekelezwa kuitia programu ndogo moja (1) na matarajio yake ya muda mrefu ni kuimarisha ujumuishaji wa mahitaji ya Watu wenye Ulemavu katika Sera, Sheria na Mipango mbali mbali.

B.1. Programu ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuhakikisha upatikanaji wa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kutetea ujumuishwaji wa Watu wenye Ulemavu; kukuza uelewa wa jamii juu ya masuala ya watu wenye ulemavu pamoja na uwezeshaji wa Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na sheria itakayofanyiwa mapitio; idadi ya nakala za sheria zitakazo chapishwa na kusambazwa; idadi ya miongozo na kanuni zitakazotayarishwa; idadi ya mikutano ya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu; idadi ya mikutano ya waratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu; idadi ya vipindi vya radio na vipindi vya TV; idadi ya mikutano ya uhamasishaji; idadi ya Watu wenye Ulemavu waliopatiwa visaidizi na dawa; idadi ya jumuiya za Watu wenye Ulemavu zitakazosaidiwa; pamoja na idadi ya vikundi vya ujasiriamali vya Watu wenye Ulemavu vitakavyosaidiwa.

Mhe. Spika, programu hii ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 155,460,000/- kutoka Serikalini, na utekelezaji wake utafanywa na Idara ya Watu wenye Ulemavu. Hivyo, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya TZS 155,460,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii.

C. PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA

Mhe. Spika, programu hii itatekelezwa kuititia programu ndogo tatu (3) na matarajio yake ya muda mrefu ni kuimarisha ufanisi na ubora katika utoaji wa huduma katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

C.1. Programu ndogo ya Uongozi na Utawala

Mhe. Spika, programu hii ina lengo kuu la kuratibu shughuli za uongozi na rasilimali watu, ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi na uongozi; kuisaidia jamii katika kazi za maendeleo pamoja kuongeza uelewa wa jamii juu ya masuala yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii yatapimwa kutokana na asilimia ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi; idadi ya wafanyakazi waliopatiwa mafunzo; asilimia ya mahudhurio kazini; idadi ya wafanyakazi waliopatiwa stahiki; idadi ya vikundi vilivyopatiwa msaada; idadi ya mikutano na waandishi wa habari (*press conference*) na idadi ya vipindi vyta redio na vipindi vyta TV.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo ya Uongozi na Utawala utafanywa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Ofisi ya Faragha.

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 2,051,997,000/- kutoka Serikalini.

C.2. Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, programu hii lengo kuu ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Sera, Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini kwa masuala yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kuimarisha mfumo wa upatikanaji taarifa na kuzisambaza kwa wadau; kuratibu masuala mtambuka yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; na kutayarisha sera, mipango na bajeti za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na idadi ya tafiti zitakazofanywa; idadi ya nakala za ripoti za utafiti zitakazochapishwa; idadi ya mikutano ya kuwasilisha taarifa za utafiti kwa wadau; idadi ya taasisi zenyne mpango wa kujumuisha mambo mtambuka; idadi ya mikutano ya uratibu wa masuala mtambuka; idadi ya mikutano ya ufuutiliaji na tathmini; hotuba ya bajeti na Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*) itakayotayarishwa; na idadi ya nakala za sera ya Watu wenye Ulemavu zitakazochapishwa.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti utafanywa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadirwa kutumia jumla ya TZS 93,719,000/- kutoka Serikalini.

C.3. Programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba

Mhe. Spika, programu hii lengo lake kuu ni kuratibu shughuli za uongozi, rasilimali watu na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba ambapo huduma zinazotarajijiwa kutolewa ni uimarishaji wa ufanisi wa utendaji kazi na uongozi pamoja na kuratibu, kufuatilia na kukuza mashirikiano kwa masuala ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na asilimia ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi; idadi ya wafanyakazi watakaopatiwa mafunzo; asilimia ya mahudhurio kazini; idadi ya wafanyakazi watakaopatiwa stahiki; na idadi ya ziara za vijijini (*field visits*) zitakazofanywa kufuatilia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo utafanywa na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadirwa kutumia jumla ya TZS 448,148,000/- kutoka serikalini.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya TZS 2,593,864,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii ya Mipango na Utawala wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

D. PROGRAMU YA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, programu hii itatekelezwa kuititia programu ndogo mbili (2) na matarajio yake ya muda mrefu ni kuiwezesha jamii kuwa huru na athari ya dawa za kulevya.

D.1. Programu ndogo ya Uratibu wa Udhibiti wa Usafirishaji na Usambazaji wa dawa za kulevya

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuzuia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya pamoja na kuzuia usambazaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa 46programu hii ndogo yatapimwa kutokana na kuwepo muongozo wa utoaji taarifa; idadi ya mikutano ya kuhamasisha jamii; na idadi ya operesheni zitakazofanyika na maeneo yanayofanyiwa biashara ya dawa za kulevya yatakayosambaratishwa.

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 57,814,000/- kutoka serikalini.

D.2. Programu ndogo ya Kinga ya msingi ya Mahitaji na Matumizi ya Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, 46programu hii ndogo ina lengo kuu la kupunguza tatizo la utegemezi wa dawa za kulevya katika jamii ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni uhamasishaji wa jamii juu ya athari ya dawa za kulevya pamoja na kuzijengea uwezo nyumba za upatajji nafuu.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na idadi ya skuli, taasisi za binafsi na za Serikali zilizofikiwa; idadi ya nyumba zilizosaidiwa na idadi ya waliofaidika na programu za ujasiriamali.

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 33,250,000/- kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya utaratibiwa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya TZS TZS 91,064,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii ya Udhibiti wa dawa za kulevya.

E. PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA WA TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, programu hii itatekelezwa kuititia programu ndogo mbili (2) na matarajio yake ya muda mrefu ni kuwezesha mazingira bora ya kazi ndani Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

E.1. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuongeza uwezo wa kufanya kazi na kuweka mazingira mazuri ya kazi ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kujenga uwezo wa wafanyakazi katika uratibu wa mapambano ya dawa za kulevya.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na asilimia ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Tume; idadi ya wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ndani ya kazi pamoja na asilimia ya bajeti ya utekelezaji wa mipango ya Tume.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo utafanywa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mhe. Spika, programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 304,690,000/- kutoka Serikalini.

E.2. Programu ndogo ya Uratibu wa masuala ya Dawa za kulevya Pemba

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuongeza uwezo wa kufanya kazi na kuweka mazingira mazuri ya kazi, ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni uratibu wa shughuli za Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo utafanywa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Ofisi Kuu ya Pemba na inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 71,346,000/- kutoka serikalini.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya TZS 376,036,000/- kwa ajili utekelezaji wa Programu hii ya Mipango na Utawala wa Tume Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

PROGRAMU YA KURATIBU MUITIKO WA TAIFA WA UKIMWI

Mhe. Spika, programu hii itatekelezwa kuititia programu ndogo mbili (2) na matarajio yake ya muda mrefu ni kuwezesha kupungua kwa maambukizi mapya ya *VVU* katika jamii.

F.1. Programu ndogo ya Mawasiliano na Utetezi.

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuimarisha utekelezaji wa mipango ya utetezi na uhamasishaji ili kupunguza maambukizi mapya ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni uhamasishaji na utetezi ili kupunguza mazingira ya hatari ya kuambukizwa *VVU* na kuchochea mabadiliko ya tabia kwa makundi maalum na jamii.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na idadi ya shehia zitakazofikiwa kwa njia ya sanaa za maonyesho; idadi ya programu za jamii zitakazofanyika kwa makundi maalum; idadi ya watu wa makundi maalum watakoafikiwa; idadi ya vipeperushi na majarida yatakayochapishwa na kusambazwa kwa walengwa; idadi ya vipindi vya redio na *TV* vitakavyorushwa; idadi ya mikoa itakayohamasishwa na kuchukua hatua za kupunguza mazingira hatarishi; idadi ya mikutano ya kuziratibu taasisi zinazotekeleza shughuli za uratibu na utetezi wa uhamasishaji; idadi ya taasisi zitakazojengewa uwezo; na asilimia ya fedha zitakazotolewa kwa utekelezaji wa programu ya stadi za maisha na afya ya uzazi kwa vijana nje ya skuli.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo utafanywa na Tume ya UKIMWI, na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 1,034,381,000/- zikiwemo TZS 51,981,000/- kutoka serikalini, TZS 932,400,000/- kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 50,000,000/- ikiwa ni mchango wa serikali katika kazi za maendeleo.

F.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa UKIMWI.

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuongoza, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miongozo ya kitaifa, sera na sheria ya kukinga na kusimamia masuala ya UKIMWI ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya muitiko wa UKIMWI; kuelimisha jamii juu ya Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2014; kuandaa Mkakati wa Tatoo wa Taifa wa UKIMWI; kuongeza uwezo wa Tume, jamii, wizara na sekte binafsi kupambana na UKIMWI; na kufanya ufuatiliaji na mikutano ya kuratibu shughuli za UKIMWI kwa sekte za serikali, wilaya, sekte binafsi, asasi za kiraia na shehia.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ndogo yatapimwa kutokana na kuwepo kwa Mfuko wa Taifa wa UKIMWI;

- Idadi ya mapendekezo ya miradi;
- Idadi ya vipindi nya redio na *TV* vitakavyorushwa;
- Kuwepo Mkakati wa tatu wa Taifa wa UKIMWI;
- Idadi ya shehia zitakazowezeshwa na zitakazopatiwa mafunzo; idadi ya mikutano ya uhamasishaji kwa ABCZ;
- Idadi ya wizara zitakazopatiwa muongozo wa kufanya mapitio ya mipango ya UKIMWI;
- Kuwepo ripoti ya Tathmini ya hali halisi na mahitaji ya huduma za UKIMWI kwa maeneo ya masoko na usafiri wa daladala;
- Idadi ya mikutano ya uratibu; kuwepo kwa ripoti ya mwaka ya ufuatiliaji;
- Idadi ya mikutano ya Kamati ya Kitaalamu ya Ufuatiliaji; kuwepo kwa mpango wa utafiti wa Tume; na
- Idadi ya wadau wanaotekeleza shughuli za UKIMWI watakaofuatiliwa.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo utafanywa na Tume ya UKIMWI, na unakadirwa kutumia jumla ya TZS 100,833,000/- kutoka serikalini.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya TZS 1,135,214,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI, zikiwemo TZS 152,914,000/- kutoka serikalini, TZS 932,400,000/- kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 50,000,000/- ikiwa ni mchango wa serikali katika kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA WA TUME YA UKIMWI

Mhe. Spika, programu hii itatekelezwa kupitia Programu ndogo mbili (2), na matarajio yake ya muda mrefu ni kuwezesha mazingira bora ya kazi ndani ya Tume ya UKIMWI Unguja na Pemba.

G.1. Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo kuu la kuwa na mazingira wezeshi kwa Tume ya UKIMWI kutimiza majukumu yake, ambapo huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kuweka mazingira mazuri ya kazi; kujenga uwezo wa wafanyakazi; na kusimamia matumizi bora ya fedha, uwazi na uwajibikaji.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ndogo yatapimwa kutokana na asilimia za utekelezaji wa mpango wa manunuvi, na matengenezo ya ofisi

yaliyofanyika; idadi ya wafanyakazi watakaopatiwa mafunzo pamoja na idadi ya wafanyakazi na familia zao watakaoshiriki Siku ya Afya (*wellness programme*).

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo utafanywa na Tume ya UKIMWI na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 383,386,000/-.

G.2.Programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya UKIMWI Pemba.

Mhe. Spika, programu hii ndogo lengo lake kuu ni kuratibu shughuli za UKIMWI Pemba kwa wadau wote.

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ndogo yatapimwa kutohana na idadi ya mikutano ya uratibu kwa Taasisi za Serikali, taasisi binafsi na Shehia itakayofanyika, na idadi ya wafanyakazi watakaopatiwa mafunzo.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Programu hii ndogo utafanywa na Tume ya UKIMWI Ofisi ya Pemba na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 184,900,000/-.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya TZS 568,286,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii ya Mipango na Utawala wa Tume ya UKIMWI.

SHUKURANI

Mhe. Spika, naomba kukushukuru tena, pamoja na wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu. Ni dhahiri kwamba mashirikiano yenu, umoja, upendo na nidhamu ndio siri kubwa ya mafanikio tuliyoyapata.

Mhe. Spika, naomba kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Makatibu wote wa Baraza wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwa umakini wao katika kulisaidia Baraza, Kamati za Baraza na Wajumbe wa Baraza katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, naomba niwashukuru waandishi wote wa habari waliopata nafasi ya kushuhudia yale yaliyofanyika hapa Barazani kwa vipindi tofauti vya mwaka, lakini na wale tuliokuwa pamoja nje ya Baraza kwa safari na mikutano mbali mbali katika jamii. Wote wamekuwa na mchango adhimu wa kuwafikishia wananchi taarifa na miongozo mbali mbali ya masuala yanayohusu nchi yao.

Mhe. Spika, naomba pia kwa namna ya pekee kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugezi, Afisa

Mdhamini pamoja na Maafisa wa ngazi zote kwa kufanya kazi bila kuchoka, zilizotuwezesha kutekeleza malengo na majukumu yetu kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, natoa shukrani za dhati kwa nchi marafiki, mashirika ya Kimataifa na watu binafsi, kwa kuendelea kutusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nchi hizo ni pamoja na Marekani, Finland, Norway, Uingereza, Uhlanzi, Australia, China, Brazil, India na Falme za nchi za Kiarabu na Oman. Pia, mashirika ya kimataifa yakiwemo *UNDP, UNICEF, UNFPA, UNAIDS, UNEP, UNODC, UNFCCC, WHO, World Bank, CDC, THPS, IOC, UNESCO, DFID, IIED, Save the Children International*, pamoja na nchi na mashirika mengine ambayo sikuyataja. Lakini kwa njia moja au nyengine yanatuunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo. Juhudi na michango yao tunaithamini sana.

Mhe. Spika, shukurani za pekee ziwaendee wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mwisho, napenda kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla, kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru sana familia yangu, kwa ustahamilivu wao na msaada mkubwa wanaonipa katika kunijengea utulivu, ili niweze kutekeleza majukumu yangu, nawaombea heri na baraka katika maisha yao.

Mhe. Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla, kwa kudumisha amani katika kipindi hichi chote cha miaka mitano chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sote tunaelewa amani ni nyenzo muhimu ya kutufikisha katika maendeleo endelevu na ustawi wa jamii yetu. Nawaomba wanasiasa na wananchi wote kwa ujumla, kuhakikisha tunadumisha amani katika kipindi hichi cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu hadi kufikia kukamilisha uchaguzi kwa salama na amani. Namuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuitunza amani ndani ya nchi yetu. *Amin.*

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sasa nachukuwa nafasi hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako waipokee, waijadili, washauri, waelekeze na hatimae kuidhinisha matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ya jumla ya shilingi Bilioni tatu, milioni mia tatu na sabini na tatu na laki nne (T.Shs. 3,373,400,000/-) kwa mwaka wa fedha 2015/2016, zikiwemo shilingi Bilioni mbili, milioni mia tisa na ishirini na tatu na laki nne (TZS 2,923,400,000/-) kutoka Serikalini na shilingi

Milioni mia nne na hamsini (T.Shs. 450,000,000/-) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Kati ya fedha hizo, shilingi Milioni mia moja na sabini na nne, na elfu sabini na sita (T. Shs. 174,076,000/-) kutoka Serikalini pamoja na shilingi Milioni mia nne na hamsini (T.Shs. 450,000,000/-) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zitakuwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya tabianchi. Shilingi Milioni mia moja na hamsini na tano, laki nne na elfu sitini (T. Shs. 155,460,000/-) kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu na shilingi Bilioni mbili, milioni mia tano na tisini na tatu, laki nane na elfu sitini na nne (T. Shs. 2,593,864,000/-) kutoka serikalini, kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Mipango na Utawala (Angalia **Kiambatanisho Nam. 10**).

Mhe. Spika, aidha, naliomba Baraza lako liidhinishie Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhhibit wa Dawa za Kulevyaa matumizi ya jumla ya shilingi milioni mia nne na sitini na saba na laki moja (T.Shs 467,100,000/-) kutoka serikalini, kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni tisini na moja na elfu sitini na nne (T.Shs 91,064,000/-) kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Udhhibit wa Dawa za Kulevyaa na shilingi milioni mia tatu na sabini na sita na elfu thelathini na sita (TShs. 376,036,000/-), kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Mipango na Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevyaa. (Angalia **Kiambatanisho Nam. 10**).

Mhe. Spika, aidha, naliomba Baraza lako liidhinishie Tume ya UKIMWI, matumizi ya jumla ya shilingi Milioni mia saba na ishirini na moja na laki moja (T.Shs. 721,100,000/-) kutoka serikalini, shilingi milioni mia tisa na thelathini na mbili na laki nne (T.Shs. 932,400,000/- kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, na shilingi milioni hamsini (T. Shs. 50,000,000/-) ikiwa ni mchango wa serikali katika kazi za maendeleo, zitakuwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya UKIMWI, na shilingi milioni mia tano na sitini na nane, laki mbili na elfu themanini na sita (TShs 568,286,000/-) kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Mipango na Utawala wa Tume ya UKIMWI.

Kati ya fedha hizo, shilingi milioni mia moja na hamsini na mbili, laki tisa na elfu kumi na nne (T.Shs. 152,914,000/-) kutoka serikalini, shilingi milioni mia tisa na thelathini na mbili na laki nne (T.Shs. 932,400,000/- kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, na shilingi milioni hamsini (T. Shs. 50,000,000/-) ikiwa ni mchango wa serikali katika kazi za maendeleo, zitakuwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI; na shilingi milioni mia tano na sitini na nane, laki mbili na elfu themanini na sita (TShs 568,286,000/-) kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Mipango na Utawala wa Tume ya UKIMWI (Angalia **Kiambatanisho Nam. 10**).

Mhe. Spika, aidha, naliomba Baraza lako likubali mchango wa jumla ya TShs.34,712,000/-, ikiwa ni mapato yaliyokadiriwa kukusanywa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Namshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwa kuunga mkono hoja. Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na mjadala, naomba nikumbushe tu kwamba mtiririko wa *activities* kwa maeneo mbali mbali ndani ya programu na programu ndogo, tuangalie kitabu cha Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, ambacho Dkt. Mwinyihaji alikigawa mapema, kimeandikwa mapitio ya utekelezaji wa mwaka 2014/2015 na mwelekeo wa mwaka 2015/2016, huo mpango wa maendeleo wa Zanzibar.

Kitabu hiki ukiangalia katika ukurasa wa 133 hadi ukurasa wa 165 utakuta huo mtiririko wa *list* ya mambo ya kazi, yaani *activities* ambazo zimepangwa kwa mambo mbali mbali kwenye programu na programu ndogo hizo, zitasaidia katika kujua huo mnyambuliko wa kazi zenyewe, yaani *activities* katika maeneo mbali mbali. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe.

Basi baada ya hayo sasa mjadala uanze na nitangulize kumwita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya kamati kuhusiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, katika bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, nianze kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuwezesha siku hii ya leo kuweza kutufikisha hapa tukiwa wazima kabisa na wenye afya njema.

Pia, Mhe. Spika, nikushukuru wewe mwenyewe binafsi, kwa kuweza kuliongoza Baraza lako hili tukufu la Nane la wananchi wa Zanzibar, kwa kipindi chote cha uhai huu wa Baraza hili la Nane la miaka mitano, kwa umahiri mkubwa na kwa kushirikiana na wasaidizi wako bila ya matatizo yoyote na wala bila ya kuonesha upendeleo wa aina yoyote.

Vle vile, nachukua nafasi nyengine ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake za mvua aliyatupa nchini mwetu, ambapo bila ya kutuneemesha neema hii

basi maisha yetu hayatoweza kuendelea. Aidha, kwa kuwa mvua zinazoendelea kunyesha, zimeleta maafa kwa baadhi ya wananchi wetu. Pia, nachukua nafasi hii kwa niaba ya kamati kuwapa pole wale wote ambaao wameathirika na mvua hizo. Tunaomba wawe na subra na tunamuomba Mwenyezi Mungu kile ambacho wamekipoteza, basi kwa njia nyengine Mwenyezi Mungu aweze kuwarejeshea. Lakini pia waendelee kuiamini serikali yao, kwani imeonesha moyo mkubwa wa mashirikiano kwa kuwasaidia katika maafa haya. Vile vile, tunaamini serikali yetu itajitahidi katika mengine yatakayotokeza katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pia, katika hili tunaendelea tena kuwapongeza viongozi wetu wote wakuu wa nchi kwa kuonyesha moyo wa kuwafariji wananchi wetu walipatwa na maafa ya mafuriko ya mvua kubwa ya masika iliyonyesha hivi karibuni, kwa kweli tuliwaona viongozi wetu hawa walitoka maofisini mwao na kuwemo mitaani kuwafariji watu wetu mbali mbali hawa kwa niaba yao tunawashukuru na tunawaomba waendelee na moyo huo huo wa kuwa karibu na wananchi wetu katika hali au kwa hali na mali.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kamati yangu inampongeza sana Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuendelea kuiongoza Afisi yake ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa umahiri mkubwa na pia kuendelea kumshauri vizuri Mhe. Rais wa Zanzibar katika kuiongoza nchi yetu. Sote tunaamini mafanikio yote tunayoyapata ya maendeleo hapa Zanzibar basi ni mashauriano ya pamoja baina ya viongozi wetu ambaye ni Mhe. Rais wa Zanzibar, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kukaa pamoja na kuangalia mustakbal wa nchi yetu katika kuwaletaa maendeleo hapa Zanzibar. Tunawaomba viongozi wetu hao waendelee kukaa pamoja kwa kushauriana na tumuombe Mwenyenzi Mungu awajaalie waendelee kuelewana kwani wakielewana wao ndipo nchi yetu itakapopata baraka na neema ili wananchi wetu kufaidika na matunda ya nchi yao.

Mhe. Spika, pia, kamati yangu inampongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kwa kumsaidia Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais katika shughuli zake, Mhe. Spika, Waziri huyu ni mwanamke shupavu asiyeyumba wala kuterereka katika kutekeleza majukumu yake, na ndio maana ameweza kubeba sifa nydingi ndani na nje ya nchi yetu.

Kamati yangu katika kipindi chote cha miaka mitano imeweza kupata mshirikiano makubwa kutoka kwa Waziri huyu, kwani pia hakusita kutaka msaada wetu pale alipokua akikwazwa na utekelezaji wa shughuli zake na bila kusita kamati yetu iliweza kutoa msaada mkubwa ili kuweza kufanikisha majukumu yake. Ndio maana leo tunajivunia alau kusema tumeweza kupata eneo la kujenga nyumba za

kurekebisha tabia katika vijana wetu walioathirika na madawa ya kulevyta (*Rehabilitation Centre*) huko kidimni Mkoa wa Kusini Wilaya ya Kati Unguja. Hayo ni baadhi tu kati ya mafanikio ambayo yamepatikana baina ya mashirikiano baina ya Mhe. Waziri wetu pamoja na Kamati.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri yeye ni (*Hajat*) na katika hotuba yake ametuombea Dua sote turudi tena hapa Barazani ili kuliendeleza gurudumu letu hili tuliloliacha, basi tumuombe Mwenenzi Mungu na hasa kwa Ijumaa ya leo basi aweze kuibali dua yake ili tuweze kuwa pamoja mwakani kuja kuisimamia vizuri bajeti yake. *Amin.*

Mhe. Spika, pia, kamati yangu inaungana na Mhe. Waziri kutoa mkono wa pole kwa familia ya aliye kua mjumbe mwenzetu Marehem Salmin Awaadh Salmin. Sote basi tumumbe Mwenyenzi Mungu aiweke roho yake peponi. *Amin.*

Mhe. Spika, Kamati yangu inatoa shukrani zetu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Afisi hii, kamati yangu pamoja na kuisimamia Afisi hii lakini na sisi vile vile tumeweza kuchota mengi kutoka kwa Katibu Mkuu huyu *Senior* katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini pia shukurani za dhati kwa Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hii, Wakurugenzi, Makamishna pamoja na watendaji wote wa Afisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mashirikiano makubwa waliokuwa wakitupatia wakati wote tulipokuwa katika kazi zetu kwa pamoja.

Nichukue tena nafasi hii vile kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi, lililoanza uhai wake kuanzia 2010, kwa Mashirikiano makubwa kufanya kazi kwa pamoja baina ya Wajumbe bila ya kujali tofauti zao za kisiasa na kwa kweli mimi mwenyewe binafsi pamoja na kamati umetupa faraja kubwa sana ya kuweza ku jiamini na kusimama leo hii katika kikao cha mwisho cha Bajeti ya Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Niendelee kuwaomba Wajumbe kudumisha mapenzi na mashirikiano ya pamoja katika kujenga nchi yetu hii ya Zanzibar, ambayo ni utegemezi wake, ni nguvu za pamoja za watu wake, ambao ndio sisi ambao walituleta kutoka katika Majimbo mbali mbali.

Mhe. Spika, baada ya shukrani zote hizo za watu mbali mbali tumeshirikiana nao, sasa naomba niingie katika kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kama hivi ifuatavyo; -

Mhe. Spika, kwa kweli kwa niaba ya kamati tumpa pole sana Mhe. Waziri, kwani majukumu aliyopewa kuyasimamia katika Ofisi yake ni masuala magumu ambayo yanachangamoto nyingi kwani karibu yote wao hawana uwezo wa kuyashughulikia moja kwa moja isipokua inabidi yashughulikiwe na taasisi nyingine chini ya isimamizi wao. Inawezekana wakati mwingine Mhe. Waziri pengine walikuwa

hawaridhiki kwa uharaka au kwa kasi waliokuwa wakiitarajia lakini walikuwa wanabakia wanasisitika na kusononeka. Lakini pamoja na hayo tunawapongeza kwa kuweza kuwasimamia kwa karibu na kutoa ushauri pale ilipobidi ili kuhakikisha kwamba yale malengo yao yanaweza kufikiwa.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Idara ya Uratibu ya shughuli kwa kuweza kusimamia shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kwa kuweza kuratibu shughuli zake mbali mbali za kitaifa pamoja na kimataifa zinahusu masuala yote katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini bado kamati yangu inaungana na Mhe. Waziri kwa idara hii kuendelea kukabiliana na changamoto nyingi ya ukosefu nyumba ya makaazi kwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwa hapa Unguja, kwamba mpaka leo bado tunaendelea kukodi nyumba na vile vile Pemba tunaendelea kukodi nyumba, lakini kwa upande wa Dar-es-Salaam ndio kabisa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais anafikia Hotelini.

Mhe. Spika, Kamati yangu kwa kweli hairidhiki kabisa na hali hii kwani huyu ni kiongozi mkubwa katika nchi yetu, lakini pia inaigharimu Serikali kutumia pesa nyingi sana kulipia majengo hayo pesa ambazo zingeliweza kuwahudumia wananchi wetu kwa shughuli zao mbali mbali za kijamii na kimaendeleo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali katika muhula ujao kupitia Tume ya Mipango tunaitaka Serikali kuhakikisha inampatia Makamu wa Kwanza wa Rais Makaazi ya kudumu Unguja, Pemba na Dar-es-Salaam, ili awe na utulivu lakini vile vigeo tuweze kuokoa pesa za wananchi.

Mhe. Spika, jukumu jingine ambalo Afisi hii ya Makamu wa Kwanza ni usimamizi wa Mazingira, kama nilivyoleza hapo mwanzo mionganoni mwa changamoto kubwa zilizopo katika eneo hili la uharibifu wa Mazingira kwa kweli hali yetu sio nzuri na usimamizi wa jambo hili. Kwani ukizingatia nchi yetu ni visiwa lakini bado uelewa wa wananchi wengi katika uhifadhi wa Mazingira hapa Zanzibar ni mdogo sana kwani ukiangalia kuanzia katika miradi mikubwa mingi hapa Zanzibar huwa haifanyiwi tathmini ya kimazingira kabla ya kuanzisha miradi hiyo jambo ambalo hasa katika fukwe zote za Zanzibar.

Kuna uharibifu mkubwa wa Mazingira na wakati mwingine sisi viongozi ndio tunaowingkingia vifua watu hao bila ya kujuu kuwa tunaliangamiza Taifa letu, na Waswahili wanamsemo wao kua; "Hili gogo tulilokalia ndio tunalolikata" yaani visiwa vya Unguja na Pemba. Hali hii kwa kweli inasikitisha sana kwani athari kubwa tumeanza kuziona, leo hii tusije kushangaa siku moja tikiamka Kisiwa cha Kisiwa Panza kikiwa kimezama chote kwa maji ya Bahari. Mwenyenzi Mungu atuepushie mbali.

Mhe. Spika, leo hii wananchi wengi hasa katika kisiwa cha Pemba wameingia katika umaskini mkubwa waliokua hawakutarajia katika maisha yetu kwani yale maeneo waliyokua wakilima mpunga na mazao mengine tangu enzi za mababu zao hivi sasa yamevamiwa na maji ya Bahari na hawawezi tena kuyatumia maeneo kwa ajili ya kilimo, jambo ambalo kilimo kilikuwa ndio tegemea lao kubwa kwa chakula, kusomesha watoto wao, pamoja na mahitaji mengine katika familia zao. Hii yote inatokana na uharibifu wa mazingira hasa kwenye maeneo ya fukwe unayofanywa na katika maeneo mengine. Kwa hiyo, nitoe wito kwa sisi sote tuungane katika kupiga vita uharibifu wa mazingira kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kutokana na kuokoa muda nimetoa mfano mmoja tu katika uharibifu wa mazingira katika eneo hili na kwa sababu katika eneo hili ndilo linaloongoza katika uharibifu wa mazingira na kuwatia umaskini wananchi wetu wengi. Kwa hiyo, nawaachia wajumbe wa Baraza lako hili tukufu ili waendelee kuendelee kuongelea katika maeneo mengine ambayo yana uharibifu mkubwa wa Mazingira.

Mhe. Spika, pamoja na hayo lakini kamati yangu inatoa pongezi kwa Serikali kwa kusikia kilio chetu cha muda mrefu kwenye eneo hili la uharibifu wa mazingira kwa kuleta sheria itakayoanzisha taasisi maalum itakayosimamia masuala mazima ya mazingira. Tunaamini taasisi hii ikiweza kusimamia vizuri basi athari ambazo zilizokuwa zikitokezea haitoweza kuendelea kuendelea kuwa mbaya zaidi na kuweza kutoa miongozo ya kudhibiti pale panapotokezea uharibifu.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Serikali kupitia Idara ya watu wenye Ulemavu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuratibu masuala yote yanayohusu watu wenye ulemavu na pia kuweza kukamilisha *data base* ya kuweza kuwatambua watu wote wenye ulemavu hapa Zanzibar. Kwani hii itaweza kusaidia kuwatambua pahala walipo ili kuweza kurahisisha Serikali kwa upatakanaji wa mahitaji yao muhimu, lakini vile vile kwa huduma muhimu kwa watu hao.

Lakini pia nitoe pongezi maalum kwa Mkurugenzi wa Idara hii kwa kazi kubwa anayoifanya katika kupigania haki za watu wenye ulemavu, kwa hiyo, tunawaomba waendelee na utendaji huo na Mwenyezi Mungu atamsaidia.

Mhe. Spika, kwa hivyo, natoa wito kwa Mkurugenzi wa Idara hii kuanza mikakati ya kutafuta Wawakilishi na Wabunge wao wenyewe watakaokuja kuwawakilisha katika chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi pamoja na Bunge ili kuja kuweza kutetea wao wenyewe maslahi yao na fursa zao pamoja na kudai huduma bora katika kundi lao ndani ya vyombo vya kutunga Sheria baada ya Katiba Mpya kupitishwa. Pia, tunawapongeza kwa kuanzisha mfuko wa watu wenye ulemavu mfuko ambao utaweza kusaidia shughuli zao mbali mbali za kujiongezea kipato na kuwaleta maendeleo.

Mhe. Spika, kama nilivyoleza hapo mwanzo Mhe. Waziri amekabidhiwa mambo mazito mingoni mwao ni mapambano dhidi ya maradhi thakili ya UKIMWI ambayo yanangamiza wananchi wetu wengi. Tunampungeza Mkurugenzi wa Tume ya UKIMWI kwa kazi kubwa ya kueleimisha jamii katika mapambano dhidi ya maradhi haya thakili ya UKIMWI, lakini kamati yangu inasikitika sana pale inaposikia kuwa washirika wa Maendeleo wameanza kupunguza misaada yao katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Kwa hiyo kamati yangu inaitaka Serikali pamoja na kuongeza fungu katika mapambano au katika Idara hii, lakini bado fungu hilo ni dogo halitoshi kwa kulingana na gonjwa lenyewe. Pia, kamati yangu inawapongeza viongozi wa ZAPHA + kwa jitihada zao za kujikusanya na kuweza kutoa misaada mbali mbali kwa wale waliopata maambukizi ya maradhi hayo pia na kwa wale ambao tayari wameathirika, kwani bila ya jitihada zao basi hali ingelikua mbaya zaidi.

Kutokana na elimu wanayoendelea kuitoa kwa jamii basi hata hali ya unyanyapaa kwa kiasi fulani imeanza kupungua hapa Zanzibar ingawa bado kuna baadhi ya maeneo mengine unyanyapaa bado upo. Kwa hivyo, bado jitihada ya kuwafikia watu katika maeneo hasa ya vijijini iendelee na kwa hivyo, iko haja kwa Serikali kuandaa utaratibu wa kuisaidia fungu la fedha ZAPHA+ hasa baada ya wahisani kuanza kupunguza misaada kama nilivyosema hapo mwanzo.

Mhe. Spika, Kamati yangu imeendelea kujadili na kutafakari kwa kina bajeti za Wizara tatu inazozismamia, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kamati yetu imepokea bajeti za Wizara zote hizo katika mfumo mpya wa Programu, ambayo inaitwa *Programme Based Budget (PBB)*. Mfumo huu kama alivyokwisha kuelezea na Mhe. Waziri katika hotuba yake na kama Wajumbe wako tulivyopata mafunzo vile vile kuititia Semina ya tarehe 13-14 Mwezi huu. Mfumo huu kwa kweli ni mfum oambao unatofautiana sana na ule ambao wajumbe tulioweza kuuzoea na kwa sababu tulikuwa tukijadili katika mafungu lakini sasaunalazimika kujadili programu kubwa na zile programu ndogo pamoja na kufatilia zile *activities* kama alivyoziitaja Mhe. Spika.

Mhe. Spika, pamoja na kutolewa semina kwa wajumbe wako wote katika tarehe hizo ambazo nilizozitaja hapo mwanzo na pamoja na ukweli kuwa mabadiliko haya yalianza kuelezwka kwa wajumbe kupata maelezo yake takriban miaka miwili nyuma, utakubaliana na mimi kuwa, kabla ya Kamati zetu kuititia bajeti za Wizara husika, ama kabla ya Kamati ya Wenyevit kuititia Bajeti Kuu ya Serikali, ilipaswa kwanza Wajumbe wote wawe na uelewa mpana zaidi na hasa kwa namna kuwasilisha katika vitabu vyaa bajeti.

Kwa hiyo, kamati yangu inaenedelea kuitaka Serikali kwa kushirikiana na Afisi yako ya Baraza la Wawakilishi mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu kutoa tena mafunzo upya kwa Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu la Wawakilishi ili kuweza kuisimamia vizuri Bajeti hii ambayo tunaipitisha katika mwezi huu unaokuja.

Mhe. Spika, Kamati yangu ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, pamoja na kukosa elimu ya matendo kabla ya bajeti hiyo na ililazimika kujifunza haraka sana msaada mkubwa wa Katibu Mkuu wakati huo wa upitishaji wa bajeti. Katika kuipitia bajeti hiyo, Kamati yangu itaizungumzia Ofisi hii katika maeneo matatu makuu kama ifuatavyo:

OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ZANZIBAR:

Mhe. Spika, bado Ofisi hii inaendelea na makusanyo yake kama alivyosema Mhe. Waziri, kupitia Idara ya Mazingira, ambayo inategemea kupata mapato hayo kupitia ada ya hifadhi ya mazingira ambayo kwa mwaka uliopita ilikadiriwa kukusanya karibu Tsh. 10,500,000. Hadi kufikia Machi, 2015 kama alivyoeleza Mhe. Waziri, Idara ilifanikiwa kukusanya karibu Tsh. 8,700,000, sawa na asilimia 83 ya makadirio.

Sasa Idara hii kwa mwaka huu wa 2015/2016 imekadiriwa kukusanya Tsh. 23,100,000, kwa nyongeza ya Tsh. 12,600,000, ambayo ni sawa na asilimia 220 ya makadirio ya mwaka uliopita, fedha ambayo kwa namna ambavyo haikuweza kukusanywa kikaamilifu kwa miaka iliyopita ambapo Idara hii kwa mfano mwaka 2012/2013 ilikadiriwa kukusanya Tsh. 8,130,000 na ulipotimia mwaka iliweza kukusanya Tsh. 7,618,000 sawa na asilimia 94 ya makadirio. Ni wazi kuwa, kwa mwaka huu pamoja na ukweli kuwa Idara na Wizara kwa ujumla wanategemea kupata mafanikio makubwa baada ya kusainiwa kwa Sheria Mpya kama alivyoeleza Mhe. Waziri, bado kuna changamoto kubwa ya kupatikana makusanyo kamili hasa yanayokadirwa.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira, kama alivyosema Mhe. Waziri, imekusudia kukusanya kiasi ya Tsh. 11,612,000 kupitia chanzo kipywa cha ada ya ukaguzi wa mazingira. Chanzo hiki kimeelezwa kwa Kamati kuwa kinatokana na Sheria mpya ya usimamizi wa Mazingira na itaipa Idara ya Mazingira ruhusa kamili ya kukagua miradi kwa kufatilia utathmini wa mazingira katika taasisi husika za ukaguzi za mazingira ili kuweza kupitia miradi yao mbali mbali ambayo watatakiwa kufanya ukaguzi huo, chanzo hiki kinaifanya Ofisi hii kuwa na dhima ya makusanyo karibu Tsh. 34,000,000.

Hata hivyo, Kamati haina pingamizi na chanzo hicho wala kima kilicho kisiwa kukusanywa, kwani kama tulivyoeleza hapo mwanzo kitu kikubwa ambacho tunachowaomba kuweza kuhakikisha kwamba wanasimamia vizuri hizo fedha ambazo zilizokadiriwa. Mbali na kuelezwa kwenye vitabu vingi nya bajeti. Ni lazima Idara ya Mazingira kwa muongozo wa Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ikifanya juhudhi kubwa katika kukusanya fedha hizo, ili mwaka ujao iweze kupatiwa kima cha juu zaidi katika makusanyo yake.

Kamati yangu inaamini kuwa ikiwa Mamlaka hii ya Usimamizi ya Mazingira itafanya kazi yake ipasavyo basi wataseza kukusanya fedha zaidi kuliko hata hicho kiwango ambacho kilichowekwa. Kwani adhabu nyingi kwa wale watakaokiuka sheria na kukiuka sheria ya Mazingira jambo ambalo limekua ni utamaduni wa watu wengi wa hapa Zanzibar kuweza kukiuka taratibu za mazingira.

Mhe. Spika, Ofisi hii sasa inatambuliwa na matumizi yake kuititia fungu kuu la B01, ambapo jumla ya fedha zinazohitajika kwa matumizi ya kazi za kawaida kama alivyoeleza Mhe.Waziri, ni Tsh. Bilioni, 2,923,400,000 kwa fedha zinazohitajika kwa matumizi ya maendeleo ambazo ni karibu Tsh. 450,000,000. Fedha hizo ambazo zinatarajiwa kutumika kwa program kuu tatu pamoja na program ndogo sita kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama tulivyoelezwa bajeti ya mwaka huu kwa kuwa itakuwa inaendana na programu, kwa hivyo, nitaomba nichukuwe muda wako kidogo ili niweze kutoa ufanuzi katika hizo programu ambazo zitasimamiwa kama tulivyoelezwa.

Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi ambayo ina programu ndogo mbili ambazo ni usimamizi wa Mazingira na Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi.

Programu Kuu ya Pili ni Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu ambayo ina programu ndogo moja ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu, na Programu Kuu ya Tatu ni Mipango na Utawala yenye programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi, Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa masuala ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Pemba.

Mhe. Spika, programu kuu zote hizi zimeelezwa huduma zake na zinazotarajiwa kutolewa pamoja na viashiria nya mafanikio vinavyotarajiwa kufikiwa katika mwaka wa 2015/2016. Aidha, kwa programu ndogo ya usimamizi wa mazingira inatarajiwa kutumia karibu milioni 174,076,000 ambapo Tsh. 161,376,000 zinatarajiwa kutumika kwa kuendeleza mazingira endelevu kwa jamii, lakini vile vile Tsh. 12,700,000 zitatumika kwa kukuza uelewa wa kimazingira kwa jaimii.

Mhe. Spika, jumla ya Tsh. 155,460,000 zinahitajika kwa matumizi kati ya Tsh. 73,060,000 zinazotarajiwa kutumiwa kwa ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu, Tsh. 2,400,000 zinahitaji kwa kukuza uelewa kwa jamii juu ya masuala ya watu wenye ulemavu, huku Tsh. 80,000,000 zitahitajika kwa uwezeshaji wa watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, kamati yetu pia iliridhika kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuidhinishiwa Tsh. 2,593,864,000 kwa Tsh. 2,051,997,000 kutumika kwa kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi za uongozi na kusaidia jamii katika kazi za maendeleo na kuongeza uelewa kwa jamii juu ya masuala yanyaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, kamati imeelezwa na kuridhika kuwa Tsh. 53,744,000 zitumike kwa kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa na kuwasambazia wadau, Tsh. 17,527,000 zitumike kwa kuratibu masuala mtambuka yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, huku utayarishaji wa sera na mipango ya maendeleo utumie Tsh. 22,448,000.

Mhe. Spika, programu ndogo za uratibu wa masuala ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kama alivyooleza Mhe. Waziri, unahitaji fedha za kutosha, hali iliyoifanya Kamati yangu kuridhishwa na kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 448,148,000 ambapo jumla ya Tsh. 426,480,000 zitumike kwa kuimarisha ufanisi wa utendaji wa kazi za uongozi na Tsh. 21,668,000 zitumike kwa kuratibu, kufuatilia na kukuza mashirikiano kwa masuala ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, jumla ya Tsh. 450,000,000 kama alivyooleza Mhe. Waziri zimekadiriwa kukusanywa kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa miradi ya maendeleo chini ya programu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, ambapo programu hii kubwa chini ya programu ndogo ya Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi inakusudiwa kuratibu na kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi ambapo kazi kuu ni kutayarisha nyenzo na mipango ya usimamizi, kuratibu mikutano ya usimamizi na kujenga uwezo wa wadau na kukuza uelewa juu ya athari ya mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuzisaidia jamii katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Spika, fedha hizo za maendeleo zinazoombwu zitasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais chini ya Idara ya Mazingira na Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Kwa mfano, kuna Tsh. 37,000,000 zimekadiriwa kutumiwa kwa kuimarisha mazingira wezeshi kwa kuongeza matumizi mbadala ya misitu Zanzibar. Aidha, utekelezaji wa programu ndogo hii ya Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi utafanywa kwa mashirikiano

na Wizara ya Fedha kuititia Idara ya Fedha za Nje. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuititia Idara ya Nishati na Madini na Jumuiya ya *CODECOZ* na kuratibiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Spika, fedha hizo zote hizo Tsh. 450,000,000 zinakadiriwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo amba ni *UNDP* huku fedha hizo ama zikiwa ni ruzuku, fedha za nje pamoja na za ndani. Aidha, pamoja na ukweli kuwa, katika vitabu vya bajeti viliviyowasilishwa kwa Kamati, serikali haikuonekana kutoa mchango wowote katika eneo hili waziri tunamuomba labda Mhe. Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho aje kuteleza basi zile shilingi milioni 174,076,000 kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii. Kwa hiyo, katika eneo hili kamati yangu itaomba tu ufanuzi hadi kufikia leo je fedha hizo kama SMZ iliweza kuchangia.

TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya Zanzibar inakadiriwa kutumia Tsh. 166,091,000 kwa ajili ya mishahara, pamoja na Tsh. 134,680,000 kwa matumizi ya maposhon na Tsh. 166,329,000 zitatumika kwa matumizi ya uendeshaji wa ofisi kama alivyoelezea Mhe. Waziri, kwenye kitabu na kama tulivyooleza kwenye kamati ambapo fedha zote hizo zimeombwa chini ya programu kuu mbili. Programu ya Dawa za Kulevya yenye programu ndogo mbili ya Udhibiti wa usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya na programu ndogo ya Kinga ya Msingi ya Mahitaji ya Dawa za Kulevya. Na programu kuu ya pili ni Utawala, Uendeshaji na Tume ya Dawa za Kulevya ambayo programu yake ndogo ni hiyo hiyo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya.

Mhe. Spika, bado tukumbuke kuwa Zanzibar tunaeendelea kuwa ni sehemu hatarishi ya uingizaji na usambazaji wa madawa za kulevya na vijana wetu wanaendelea kuathirika na matumizi haya ya dawa za kulevya, hali inayolipelekea Taifa hili kukosa nguvu kazi na kurudi nyuma kimaendeleo. Hivyo, ili kuweza kukabiliana na tatizo hilo sugu la dawa za kulevya, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuititia Tume hii imeweka programu ndogo ya kudhibiti usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya Zanzibar, ambapo jumla ya Tsh. 30,908,000 zinahitajika kwa ajili ya kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya na Tsh. 26,906,000 zinahitajika kwa kuzuia usambazaji wa madawa hayo.

Mhe. Spika, pamoja na kima hicho kilichotengwa na kuombwa kwa shughuli hizo za udhibiti na usambazaji wa dawa za kulevya, kama iliyyokuwa malalamiko makubwa ka wananchi dhidi ya matumizi ya madawa ya kulevya yanalegwa katika uingizwaji na usambazaji wa dawa hizo kwa watumiaji mbali mbali kwa

kuzingatia ukweli kuwa serikali hufanikiwa zaidi kuwashughulikia watumiaji kuliko waletaji na wauzaji wa dawa hizo. Fedha zilizotengwa katika kutekeleza porgramu ndogo hii ni chache sana na inaonesha bado serikali kwa ujumla inahitajika waangalie kwa umakini mkubwa jukumu hili zito ambalo chanzo chake ni matumizi ya madawa ya kulevyta Zanzibar.

Mhe. Spika, jumla ya Tsh. 376,036,000 zinahitajika kwa programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevyta kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi katika uratibu wa mapambano ya dawa za kulevyta ambapo jumla ya Tsh. 304,690,000 zinahitajika na kwa ajili ya Uratibu wa Shughuli Tume ya Dawa za Kulevyta Pemba, fedha zinazohitajika ni Tsh. 71,346,000. Aidha, kwa ujumla utekelezaji wa programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevyta unaoratibiwa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta unakadiriwa kutumia Tsh. 91,064,000/- kama tulivyoelezwa hapo mwanzo.

TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kama alivyoeleza Mhe. Waziri, Tume ya UKIMWI inahitaji kupatiwa Tsh. Bilioni. 1,703,600,000, ambazo fedha zitakazotumika kwa kazi za kawaida na Tsh. Milioni. 721,200,000 kwa fedha za maendeleo ni Tsh. Milioni 982,400,000. Fedha hizo kama walivyosema zinatarajiwta kutumika chini ya programu kuu mbili, programu ya Kuratibu Mfuko wa Taifa wa UKIMWI ina programu ndogo mbili ya Mawasiliano na utetezi wa masuala ya UKIMWI na Uratibu wa muitikio wa Taifa wa UKIMWI, na programu kuu ya pili ni Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI ambayo programu yake ndogo ni Utumishi na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuitia Tume ya UKIMWI, imeahidi mbele ya Kamati kuwa kwa kutekeleza programu zote mbili na programu ndogo zilizomo itakapofika June 30 ya mwaka 2016 Mwenyezi Mungu atuweke hai itakuwa imeshatekeleza mambo haya yafuatayo:

- Kuzifikia Shehia 20 kwa maonesho.
- Kufanya programu 150 kwa makundi maalum.
- Kuwafikia watu 1400 kwa makundi maalum.
- Kuchapisha na kusambaza vipeperushi, vijarida 5000 kwa walengwa.
- Kutoa vipindi 36 vya TV na radio.
- Kuhamasisha Mikoa mitano kwa kuitaka kuchukua hatua za kupunguza mazingira hatarishi ya UKIMWI.
- Kufanya mikutano 16 ya kuziratibu taasisi zinazotekeliza shughuli za utetezi na uhamasishaji wa masuala ya UKIMWI.

- Kuzijengea uwezo taasisi 30 zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI, na
- Kutoa asilimia 100 ya fedha kwa utekelezaji wa programu ya maisha na afya ya uzazi kwa vijana nje ya Skuli.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu serikali yetu tumekuwa tukisema katika ikiwa ni pamoja na kuna haja ya kuleta mabadiliko ya mfumo wa kibajeti katika kipaumbele cha programu katika kila taasisi zake kwa kuwaacha wananchi wake waje waipime na kuzipima taasisi hizo katika utekelezaji wa programu hizo na viashiria vyake. Leo hii tunaisifu kwa vitendo matendo waliyoyasema kwa muda mrefu huko nyuma. Hata hivyo, hatua hii bado hajidhi shida na maneno ya wananchi na dhiki kubwa wanayoipata inayoipa taasisi zake ambayo ni kupatiwa uingizwaji wa fedha kwa muda muafaka ili kuweza kukidhi matumizi yaliyokadiria mbele na kuombwa mbele ya Baraza hili katika mikutano mbali mbali.

Mhe. Spika, serikali yetu pamoja na ahadi nyingi za mfumo huo mpya wa bajeti iwapo tutashindwa kukusanya vyema kama tulivyopanga ikiwa itaachia kufanya matendo ya kuziingiza fedha inazoahidi leo katika asilimia iliyopo, katika kikao hiki cha bajeti kwa wizara na taasisi zake, basi itazidi kuendelea kutoa mzigo mkubwa kwa taasisi zetu au kwa taasisi za serikali na hatimae mzigo mkubwa kwa wananchi.

Mhe Spika, kwa upande wa mambo ya kiujumla naomba kuishauri serikali kuangalia matatizo yanayowakabili hasa wananchi katika Kisiwa cha Pemba kwa kuvamiwa na maji ya bahari kwenye maeneo yao ya kilimo ambayo wanayategemea kwa kuendeshea maisha yao kama nilivyosema hapo awali. Kwa hiyo, uvamizi huo umewaaacha wananchi hao katika umasikini mkubwa kwani hawana njia nyingine yoyote ya kuendesha maisha yao. Kwa hiyo, ni vyema serikali kuandaa mradi maalum kwa kuyahami maeneo hayo lakini vile vile kuangalia na maisha ya watu hao ambao wameathirika na kuvamiwa na maji ya bahari ambayo kila siku yanaongezeka na bila ya kuweka utaratibu maalum basi umasikini utakua unaongezeka siku hadi siku na baadae utakua ni mzigo mkubwa kwa serikali yetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa wa hotuba yangu hii fupi, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe pamoja na Wajumbe wako bila ya kuwasahau Wajumbe wa Kamati yangu pamoja na Makatibu Kamati. Aidha, naomba kwa ruhusa yako kwa haraka haraka niweze kuwatambua Wajumbe hao.

Mhe. Spika, kamati yangu ilikuwa ikiongozwa na mimi mwenyewe hapa naitwa:

- | | |
|---|-------------------|
| 1. Mhe Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Saleh Nassor Juma | Makamu Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Ali Mzee Ali | Mjumbe |
| 4. Mhe. Ashura Sharif Ali | Mjumbe |
| 5. Mhe. Shadaya Mohammed Suleiman | Mjumbe |
| 6. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Mjumbe |
| 7. Mhe. Subeit Khamis Faki | Mjumbe |
| 8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu Kamati |
| 9. Ndg. Othman Ali Haji ambaye alikuwa akikaimu nafasi ya Katibu wetu ndugu Makame. | |

Mhe. Spika, niendelea kumshukuru tena kwa mara nyengine Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote waliokuwepo chini ofisi yake kwa kuweza kutoa mashirikiano makubwa katika kamati yetu hii.

Mhe. Spika, kama sitakosea kutoa nasaha zangu kwa Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake, huku nikijua kuwa sisi viongozi wa siasa huongoza taasisi hizi kwa muda maalum lakini wao ni waajiriwa wa kudumu. Niendelee kuwaeleza kuwa wao ndio roho ya Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kutekeleza kwao kwa majukumu yao kwa kuzingatia Katiba na Sheria ni matarajio makubwa sana ya wananchi wa nchi hii. Aidha, na wao ndio wataalamu na ndio wajuzi wa mambo mbali mbali, lakini wenye dhamana ya kuwaleta maendeleo ya kuimarisha ustawi wa wananchi wa Zanzibar kupitia ofisi yao hii.

Mhe. Spika, tuendelee kuwanasihi watendaji hawa waendelee kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu mkubwa kama walivyoweza kuonesha katika kipindi chote cha miaka mitano.

Mhe. Spika, sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi waanze kuvitumia vipawa vyao na uwezo wao mkubwa katika kuijadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambapo kama nilivyo sema ina changamoto nyingi ambazo nyingi zao ziko nje ya utendaji wa shughuli zao kwa kutegemea taasisi nyengine. Watumie elimu yao na uzoefu wao walioupata katika miaka yote mitano na zaidi ya mitano ambao tuliokuwepo hapa Barazani ili kuweza kuishauri serikali yetu kuweza kutatua matatizo haya ya wananchi.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naendelea tena kutoa shukurani za dhati, sasa nataka kidogo nizungumzie ikiwa kwa maoni binafsi kama Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Spika, kutohana na makofii hayo inaonesha muda kwa maoni ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kwa leo hayatoweza kutoka moja kwa moja, lakini naaminii nitawenza kumpelekeea Mhe. Waziri, kwa maandishi. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nakushukuru sana na umeutumia muda vizuri kiasi cha kwamba hakuna nafasi tena yakumwita Mhe. Mjumbe ye yeyote ili kuweza kuchangia katika kipindi hiki.

Waheshimiwa Wajumbe, muda umefikia nadhani sasa tukapumzike ila tu nakumbusha kwamba ule mtiririko wa *activities* mbali mbali tuangalie kitabu kile cha mwelekeo wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2015/2016 kuanzia ukurasa wa 133 hadi 165 yapo mambo mbali mbali ambayo yatasaidia kujua mambo gani ambayo yalikusudiwa kufanywa katika programu na programu ndogo. Basi Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(*Saa 5:54 Mchana Baraza lilahirishwa mpaka saa 11:00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea huku nina jina la mtu mmoja tu Mwenyekiti wa Kamati na keshachangia. Kwa hivyo, sina mchangiaji. Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu jioni hii kuwa mtu wa kwanza kuweza kutoa michango yangu miwili, mitatu katika Makadirio haya ya Bajeti ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimpongeze sana waziri kwa kupata Sheria mpya ya mazingira. Nataka nimpongeze kwa sababu moja katika changamoto kubwa tuliyonayo katika nchi yetu ni uchafuzi wa mazingira na uchafuzi wa mazingira umegawika makundi mawili; Kwanza kutoka na tabianchi ambalo hili sisi hatuna uwezo nalo sana, maana yake sio la kwetu pekeyetu. Ingawa tukiwa na mikakati mizuri, tukiwa *serious* tunaweza tukapunguza athari yake, lakini kwa sasa tunaweza kusema haliko katika uwezo wetu moja kwa moja. Lakini kuna uchafuzi wa mazingira ambao uko ndani ya uwezo wetu, kwa sababu kukata misitu oyoyo hili limo ndani ya uwezo wetu na tunalifanya kwa kiwango cha kutisha sana.

Sasa Mhe. Waziri, alikuwa anapata tabu kwa sababu sheria aliyokuwanayo ilikuwa haina meno sana, lakini kwa sababu sasa kapata sheria ambayo imempa mamlaka makubwa zaidi namuombea dua sana aitumie vizuri hiyo sheria ili kupunguza athari za mazingira ambazo zinatokana na sisi wenywewe wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mazingira yetu tunayaharibu sana bila ya kuzingatia udogo wa ardhi yetu tuliyonayo, bila ya kuzingatia umasikini wetu tulionao; tunachafua mazingira katika kiwango cha kutisha sana kiasi ambacho hata mvua zimeanza kupungua baadhi ya maeneo kwa sababu ya kumaliza misitu tulioanyo aliyoitujaalia Mwenyezi Mungu. Sasa namuomba sana waziri katika suala hili awe mkali kidogo.

Nadhani mionganoni mwa changamoto ambazo waziri anazo pia ni kutokuwa waaminifu watendaji wake wengine. Kwa sababu kuna wakati niliona uchungu sana nikamwambia waziri kuna tatizo pahali naomba ulifuatilie. Kulikuwa na mtu alimaliza mikoko yote anapiga tanu za chokaa na tanu za mkaa, yaani kama mtu alikuwa analijua lile eneo lilivyokuwa na sasa lilivyo akienda atatoka machoz. Nilimwambia waziri kuna tatizo hili, nashukuru sana waziri alikusudia kulifuatilia na alilifuatilia, lakini bahati mbaya sana watendaji wake walimuangusha.

Kwa sababu walivujisha taarifa kwamba bwana mkubwa wee waziri anakuja hamisha huko, chokaa ilihamishwa siku moja yote, magogo ya mikoko waliyyoyakata usiku wa kucha magari yalifanya kazi kuhamisha alipokwenda waziri asubuhi hakuna kitu kama kwamba mimi nimempa taarifa za uongo. Hii nawalaamu moja kwa moja watendaji wake ndio waliyosababisha hivyo na haya ni mazingira ya rushwa, nina hakika huyo jamaa wasingempendelea katika kiwango hiki isipokuwa wanawapa rushwa, sasa rushwa ni adui wa haki tutamaliza yetu kwa sababu ya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi sasa baada ya kumpungeza waziri nataka nimpe pole, nimpe pole kwa sababu kazi aliyopewa ya kusimamia ni ngumu mno. Kuna mambo matatu magumu na yote kabebeshwa kichwani; moja ni liho mazingira. Mazingira ni changamoto kubwa katika nchi yetu. Lakini la pili, madawa ya kulevyaa nayo ni changamoto moja kubwa sana ambayo inatumalizia nguvu kazi ya nchi yetu, mtandao wake mkubwa unahitaji utaalamu, unahitaji uaminifu wa kutosha ndio tunaweza tukakabiliana na madawa ya kulevyaa. Lakini kitu cha tatu nacho ni UKIMWI na UKIMWI nalo ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, mamba matatu haya ni mazito na mimi nadhani nilitaka kuona ile *collective responsibility*. Kwa sababu kwa kumuachia waziri na ofisi yake moja tu na kibajeti hiki kidogo anachopewa hawezu kupata mafanikio ya kutosha. Kwa

hivyo, naomba sana serikali wajitahidi sana kuwa pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais niliposema matatu haya maana yake ni adui sana wa nchi yetu.

Pole nyengine kwa Mhe. Waziri nilipokuwa napitia hiki kitabu chake nilikaribia kuona machozi, kwa sababu pesa alizoomba za mwaka huu unaomalizika nafikiri kama kuna pahali angalau kafika 50% idara moja tu, lakini idara nyengine zote ziko asilimia 35 na naomba ili hao wanaogawa pesa waone haya nizitaje hasa.

Kwanza Ofisi ya Faragha. Hii iliidhinishiwa shilingi 411,150,000; hadi kufikia mwezi wa Machi walikuwa wamepata shilingi 143,902,500 hii ni asilimia 35 Mhe. Naibu Spika. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti walidhinishiwa shilingi 146,065,000; hadi kufikia mwezi wa Machi wamepata shilingi 51,819,000 ni asilimia 35. Idara ya Mazingira ambayo ndio sugu walidhinishiwa shilingi 113,284,000 lakini pesa walizopewa ni shilingi 44,274,500 asilimia 39. Idara ya Watu wenye Ulemavu iliidhinishiwa shilingi 278,442,000 kilichopatikana ni shilingi 100,724,500 asilimia 39. Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa OC 210,000,000 walichopata ni shilingi 77,100,000; asilimia 48. Tukija kwenye miradi walidhinishiwa shilingi 1,400,000,000 kilichopatikana ni shilingi 250,000,000 sawa sawa na asilimia 18.

Mhe. Naibu Spika, sasa ikiwa hii ndio *trend* ya pesa ambazo Mhe. Waziri anapewa na makazi ya magumu kama haya aliyokabidhiwa, hivyo tufikirie huo ufanisi utakuwa namna gani labda afanye miujiza. Kwa hivyo, naomba sana serikali ambayo humu ndani imeadimika sana haimo lakini salamu zitafika maana yake *Hansard* zipo, ili kuweza kupunguza ukali wa matatizo haya makubwa ambayo yamo katika wizara hii, lazima waone umuhimu wa kuipa pesa hii Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, vyenginevyo tutakuwa tukiimba kila siku hapa hakuna ambalo litaendelea.

Jambo jengine ambalo nilisema nilitaje kidogo ukiangalia *paragraph* ya 99 ukurasa wa 27 kuna taasisi pale ambazo zinahusika moja kwa moja, maana suala la madawa ya kulevyta ni suala mtambuka halipo kwenye wizara hii peke yake ni suala ambalo linagusa taasisi nyngi sana na hapa zimetajwa. Polisi wanahusika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inahusika, Mahakama inahusika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inahusika, Bandari inahusika, Mamlaka ya Mapato Tanzania inahusika, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali inahusika, Bodi ya Mapato Zanzibar inahusika na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa inahusika.

Sasa hoja yangu iko wapi, hivi vyombo viko katika kila kona ya nchi yetu na kila kimoja kina mamlaka yake na madaraka yake. Mhe. Naibu Spika, nashangaa sana kuwa mpaka leo madawa ya kulevyta yanaingizwa hapa nchini na vijana wetu wanaendelea kuathirika na vyombo hivi viro. Hii inamaanisha ama hatuko *serious*

kama ambavyo Dokta Mshimba huwa anasema hatuko *serious*, au tumeshikwa na ubinafsí wa kupokea rushwa lazima tuseme wazi, haiwezekani vyombo vyote hivi vishughulikie dawa za kulevyá na ziweze kuingia nchini. Mimi naviomba sana hivi vyombo kila kimoja kina *role* yake katika kupambana na madawa ya kulevyá na waone kama ubinafsí ukiendelea kuwatawala basi tutakuwa tunaimaliza nchi yetu wenyewe, tusije tukatafuta mchawi baadae nani aliyemaliza hii jamii kumbe ni sisi wenyewe.

Siku moja katika ziara zetu za kusimamia serikali tulitembelea Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka akatupa mazingira ya kesi moja, kuna mtu alikamatwa na madawa ya kulevyá *airport* hapo yalikuwa yameingia sasa ye ye anatokanayo anakwenda nayo nchi nyengine, lakini hii ni *transit* akakamatwa. Sasa walijitahidi sana kufuatilia, lakini ushahidi ulivyopotoshwa yaani zile *documents* ambazo walizifanya hata mimi nisiyekuwa mwanasheria basi moja kwa moja namkamata yule ana kosa, lakini ajabu ya Mahakama ilifika pahali ikamuona hana hatia, kiasi ambacho hata yule Mkurugenzi wa Mashtaka mwenyewe alikuwa *disappointed* kweli kweli, maana yake juhudí aliyoifanya lakini hatimaye wenzake wakamuangusha.

Mhe. Naibu Spika, sasa mazingira haya yanatia uchungu kweli, nikasema lazima tuwe *serious*, lazima tuhakikishe kwamba kila mtu anatekeleza wajibu wake. Kwa sababu kuna mambo hayapaswi kufumbiwa macho. Kuna kesi kila mwaka naitaja humu, kuna mtu anauza majani ambayo kwa mujibu wa taarifa za Mkemia Mkuu wa Serikali yamesadikiwa kuwa ni bangi, anapelekwa Mahakamani na kuna mrundiko wa kesi hazipungui tatu, nne kule kwa mtu huyo huyo mmoja na bado Mahakama haimpati na hatia, kwa nini? Matokea yake anaendelea kuwauzia vijana wetu bangi wanavuta bangi wanaharibu mali za watu.

Mhe. Naibu Spika, wala mimi sitaki sana kulaumu Mahakama kwa sababu Mahakama ni muhimili tafauti kabisa na sisi hapa na tulipaswa tusiutazame hata kidogo, lakini kwa mwenendo huu tunalazimia tuweke kando kanuni zetu za kiutawala tulaumu kidogo. Mimi nafikiri wanapaswa Mahakama wawe *serious* sana katika masuala haya sio masuala ya mchezo, masuala yakiendelea kuachwa yanaweza yakaimaliza jamii yetu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya mchango wangu huu mfupi sana, naomba niishie hapa, ila nisisitize tu kwamba serikali ijitahidi kutoa pesa za kutosha kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hasa kuzingatia na mambao ambayo ni *priority* katika nchi yetu. Mambo ya mazingira na mambo ya kiutafiti yanahitaji kufanywa ni miradi mikubwa ambayo imo katika Ofisi ya Kamau wa Kwanza wa Rais. Kwa sababu hata ukiangalia Idara ya Mazingira sasa hivi ilitakiwa itoe mwelekeo kwa vile nchi yetu visiwa na visiwa kila siku, visiwa vyetu vinaendelea

kumegwa athari za kimazingira zinapungua, kilomita zake za mraba zinapungua kila uchao.

Kwa hivyo, tunadhania Idara ya Mazingira ingefanya utafiti wa kina halafu wakaishauri serikali. Katika hali kama hii basi, hata mwelekeo wetu wa mipango miji uweje, majengo yetu ya kuishi yaweje ni mambo yanayohitaji utafiti na utafiti unahitaji gharama kama serikali haiweki pesa hapa tutakuwa tunakwenda ovyo sana. Kwa hivyo, naiomba sana serikali ione umuhimu wa kutia pesa za kutosha na ikiwezekana hata pesa za ziada ilimradi tuweze kwenda kwa uhakika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chonga naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kutujaalia Alaasiri hii kukutana hapa kwa ajili ya kujadili maendeleo ya nchi yetu na mustakabali mwema wa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikupongeze kwa kunipa nafasi ili na mimi kuchangia mawili matatu katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini vile vile nisiwe mchache wa fadhila nimpongeze Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa jinsi alivyotuwasilishia ripoti yake kwa ufasaha na kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, nikikiangalia kitabu hiki cha hotuba hapa nikifungua tu kwenye jalada hili utakuta pana ujumbe wa picha, kuna ujumbe ambaa unaonesha watu mbali mbali akiwemo ye ye waziri mwenyewe na baadhi ya wafanyakazi wake, lakini kuna watu wenye mahitaji maalum wengi hapa wakiwemo walemovu wa viugo, walemovu wa ngozi na kadhalika. Picha hii inatupa taswira ya kwamba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imejipanga vyema kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum wakiwemo walemovu, tunasema kwamba picha hii isiwe ni picha tu, bali iwe ni picha kwa ajili ya utekelezaji wa mambo mbali mbali yaliyokusudiwa na ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchangano wangu katika ukurasa wa nne kwenye malengo makuu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Hapa pameelezwu malengo makuu sita ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini nataka nizungumzie lengo la tatu na la nne na hapa naombaa ninukuu. Lengo la tatu waziri amesema kwamba;

"Ni kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira na kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi".

Mhe. Naibu Spika, kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira ni jambo muhimu sana. Hivi sasa nchi yetu imekabiliwa na mambo tofauti yanayohusiana na mazingira. Kwanza kuna uharibifu wa mazingira, lakini pia kuna uchafuzi wa mazingira. Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo mbali mbali hivi sasa mazingira yetu yanachaguliwa vibaya sana na kama serikali haikuwa makini basi maeneo haya yapo katika hatari. Yaani wananchi wa maeneo haya wapo katika hali ya hatari. Mfano katika maeneo hayo moja kwa moja neende katika jimbo langu la Chambani.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri katika Afisi ya Kwanza wa Rais ana taarifa gani ya uharibifu wa mazingira katika eneo la Giningi pale Chambani. Mheshimiwa, eneo lile nalitaja naona baadhi ya Waheshimiwa hapa wanacheka, sio makao makuu ya Giningi pale pahali ambapo panachotwa mchanga kwa wingi sana. Mhe. Naibu Spika, eneo hili ni eneo hatarishi sana hivi sasa. Sijui Mhe. Waziri, ni mara ngapi umefika katika eneo lile na kutoa taaluma kwa watu Wachambani ambao wanazunguka eneo lile.

Mhe. Naibu Spika, eneo hili limechimbwa mchanga sana kiasi ambacho hivi sasa kuna mabwawa ya maji ni hatari hata kwa watoto wanaopita kwenda skuli, ni hatari hata kwa wanyama, ni hata kwa watu wanaokwenda katika shughuli zao za kilimo. Namuomba Waziri suala hili aliangalie kwa umakini sana na anambie kwamba ni mipango gani endelevu, kama alivyoitaja katika kitabu hichi ataliimarisha eneo lile na atatoa elimu ya kutosha juu ya athari ambazo zinapatikana pale.

Mhe. Naibu Spika, moja katika athari ambayo inapelekea kuchotwa mchanga kwa wingi eneo lile, kuna sehemu maarufu ambayo ilikuwa na chemchem tunaiita Jimbi Kutini, wanansikia watu wa eneo hili. Sehemu ile ilikuwa ina chemchem inatoa maji kwa wingi sana, lakini kwa athari ya kuchimbwa mchanga kwa wingi eneo hili chemchem zile zimekauka kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, hili aliangalie kwa kina na kwa kweli atoe ushauri endelevu na atoe taaluma endelevu ili eneo lile linusurike na wanusurike wananchi ambao wamekaribia eneo lile wakiwa watoto wadogo, mifugo na hata watu wazima.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika lengo la nne ambalo Mhe. Waziri, amesema ni kuimarisha na kutetea uzingatiaji wa haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu ndani ya jamii. Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu wanapaswa sana kulelewa kwa huruma ya hali ya juu kabisa. Kwa sababu sisi sote tunaojiona tuko salama hatuko salama, sote ni walemauvu watarajiwa. Watu wangapi wanatoka majumbani kwao wakiwa wazima, wakiwa salama lakini wanakutana na mitihani kadhaa wanakuwa walemauvu. Kwa hivyo,

nimuombe sana Mhe. Waziri, suala hili la walemauvu aliangalie vyema na sio tu aliangalie katika kitabu bali aliangalie katika uhalisia wake.

Mhe. Naibu Spika, ningemuuliza Mhe. Waziri, alisema kwamba kuna walemauvu kadhaa ambaao wamepewa visaidizi pamoja na dawa katika mwaka uliopita. Je, ni watu wangapi wenye ulemavu kiujumla wake ambaao wamepewa visaidizi hivi na katika jimbo langu kuna walemauvu ni wangapi ambaao amewapa visaidizi hivi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu kuhusiana na watu wenye ulemavu. Kuna watu wengi wenye ulemavu hivi sasa wanajie ndeleza kimasoma katika elimu ya juu. Miongoni mwa watu hawa wameshaomba misaada kadhaa katika Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, je, ni misaada gani ya kuwaendeleza kusoma watu hawa wenye ulemavu ambaao wameomba msaada katika Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 6 kifungu cha 20 kinasema hivi;

"Pamoja na mafaniko hayo Afisi ya Faragha imekuwa na changamoto ya msingi iliyodumu ndani ya kipindi cha miaka mitano ambayo ni kukosekana kwa makaazi rasmi ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais huko Dar-es-Salaam, halii hiyo imemlazimika kufikia hotelini, jambo ambalo limepelekea kuwa na gharama zaidi".

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo, viongozi wakubwa wa Kitaifa wana hadhi yao na wanapaswa kupewa hadhi kama ilivyo. Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Rais, hawapaswi kukosa kuwa na makaazi maalum katika safari za za Dar-es-Salaam. Kwa hivyo, nimuombe Waziri pamoja na changamoto hii kwamba imedumu kwa muda mrefu, malengo yao ni yepi ili kuitatua changamoto hii ambayo kwa kweli ni tatizo. Kwa kweli kiongozi mkubwa wa nchi kukaa hoteli kila inapotokea safari ya kwenda Dar-es-Salaam ni tatizo. Kwa hivyo, naomba serikali iliangalie hili viongozi hawa wetu wakubwa waekewe mazingira mazuri na wewe na makaazi ya serikali maalum ambayo yatakuwa yanawaenzi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 8 wa kitabu cha Mhe. Waziri kifungu cha 26, naomba ninukuu;

"Katika masuala ya watu wenye ulemavu Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeweza kufanya usajili wa watu wenye ulemavu katika Mikoa yote mitano ambaao utaiwezesha serikali kuwatambua walipo pamoja na kuzingatia mahitaji yao katika mipango ya maendeleo. Aidha Afisi ya Makamu wa Kwanza

wa Rais imeanzisha mfuko wa watu wenye ulemavu kwa lengo la kuhudumisha utoaji wa huduma kwa watu hao, mpaka wa mwisho wa aya hii."

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, ni fedha ngapi ambazo amekusanya na wana utaratibu gani wa kuzigawa ili watu hawa kufaidika na mfuko huo. Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 36 kwenye masuala ya Programu.

Amesema kwamba Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2015/16 inakusudia kufanikisha utekelezaji wa majumu yake kuitia Programu kuu 7.

(a) Programu ya kwanza ni Programu ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Hapa nataka nizungimzie kuhusiana na masuala ya mabadiliko ya tabianchi, kama tunavyoolewa Mhe. Naibu Spika, kwamba nchi yetu ni kisiwa na kisiwa kimezungukwa na bahari kila upande. Mhe. Naibu Spika, visiwa vidogo vidogo hivi sasa takribani kama vile Kisiwapanza vinaanza kuathirika na tabianchi. Mhe. Naibu Spika, tatizo hili linapelekea watu wa visiwa hivi kupata ghofu kubwa. Sasa basi ni utaratibu gani ambao afisi hii imejipanga kutoa taaluma tosha ya watu wa visiwa hivi katika kuimairisha mazingira vizuri ili huu uingiaji wa bahari katika miji kuweza kudhibiti angalau kwa kupanda miti au serikali kujenga matuta makubwa yenye uwezo kwa ajili ya kuzuia huu muingio wa bahari katika visiwa hivi.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo mengi ambayo yalikuwa hayafiki maji ya bahari hivi sasa maji ya bahari yanafika na kuna maeneo ambayo watu walikuwa wanalima yameshindikana kulima hivi kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo, ofisi na serikali kwa jumla inapaswa kwa kiasi kikubwa sana kuliangalia hili kwa kitaalamu kabisa ili kupunguza huu muingio wa maji ya bahari katika visiwa hivi vidogo vidogo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli jengine ambalo nitalizungumza kwa uchache sana ni kuhusiana na masuala ya madawa ya kulevyta. Katika Programu imeelezwa kwamba kutatumika fedha nyangi tu kwa ajili ya kudhibiti madawa ya kulevyta. Lakini tunaona katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba bado uingiaji wa madawa ya kulevyta unaendelea na vijana wetu wengi wanapiga madawa ya kulevyta, lakini kila siku hatusikii ni watu wangapi au watu gani wamekamatwa na kupelekwa Mahakamani na hukumu gani zimetolewa kwa watu hawa. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, atueleze katika kipindi cha mwaka 2014/15 ni watu wangapi wamekamatwa na madawa ya kulevyta na wamepewa hukumu gani.

Mhe. Naibu Spika, vijana wanaumia na wanateketea kwa madawa ya kulevy ya nchi inategemea vijana wenyne nguvu pamoja na madawa ya kulevy vijana watakosa nguvu, akili na tutakosa nguvu kazi ya baadae ya kuijenga na kuiendeleza nchi hii. Suala la madawa ya kulevy ni janga na kama serikali haikusimama kifua mbele kulikemea na kulitetea na kuchukuwa hatua endelevu hatua za kutosha juu ya madawa ya kulevy, tutawakosa vijana imara ambao tunawategemea kulijenga Taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana serikali isilifumbie macho wala isiwafumbie macho watu ambao wanaleta madawa ya kulevy kwa makusudi. Mimi naamini serikali ina mkono mrefu, nguvu na vyombo vyenye nguvu, uwezo wa kuwakamata watu wenyne madawa ya kulevy upo.

Lakini sijui kwa sababu gani kila siku tunasema kupunguza madawa ya kulevy, hayapungui na watu wanaendelea kuleta madawa ya kulevy. Naiomba serikali hili ilipe nafasi kubwa ili kuwalea vijana wetu wawe imara katika kuitetea nchi yetu pamoja na kuendelea na shughuli za ujenzi wa Taifa, bila ya kuwa na vijana makini basi shughuli za ujenzi wa Taifa ya nchi yao kwa kweli tunawenza tukawakosa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mchango wangu huu niseme kwamba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. (*Makofî*)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kuweza kunipa nafasi jioni hii ya leo kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na hasa imesomwa na Mhe. Waziri, ambaye ni mwanamke.

Kwanza nimpe pongezi sana, nimemsikia sana alivyokuwa akiongea katika hotuba yake hii. Niwapongeze kwa jumla pamoja na Katibu, Naibu Katibu pamoja na Wakurugenzi na Afisa wao mara nyingi nilikuwa nao karibu sana. Mhe. Naibu Spika, ni watu wasikivu sana na siku zote mimi nasema panapo haki ipeleke haki. Nashukuru sana tulikuwa na mjadala mkubwa sana katika hii Programu ya Mradi ya wa *PBB* ya Bajeti mpya na tulianza kupata taaluma kabla ya kwenda kwenye semina Mhe. Naibu. Katika watu ambao tulikataa ilikuwa irudi ni moja katika sisi. Lakini nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara hii alijitolea, ni kitu ambacho cha maajabu makubwa sana, lakini yeze siku hiyo alijitolea akawa mwali muu wa kutuelimisha sisi na sisi pamoja na kuitwa Waheshimiwa tulikubali taaluma yake.

Mhe. Naibu Spika, hilo tumeshukuru sana na tumeendelea kupata taaluma tena ilivyokuja hii semina tumeepigwa *brash*, tumeondoshwa tu na hakuwa na posho lakini alifanya kazi ya watu ya ziada. Alikuwa na yeze apewe posho lakini amepata

mafunzo tangu enzi hizo za Umoja wa Vijana mpaka leo na ukipita Umoja wa Vijana inasaidia sana, hilo niseme ukweli.

Mhe. Naibu Spika, mimi huwa mtaratibu sana naogopa sana kikiingia sana hichi kitabu kwa sababu kina mahiri mtu ambaye amesema sana kabisa. Mhe. Naibu Spika, ukurasa huu nichangie na mimi katika masuala ya dawa za kulevyta. Hapa mimi nataka nitowe ushauri wangu mkubwa sana katika hizi programu zetu ambazo mlozipanga ninaamini hiyo itakuwa ni *New Programme* kwenu nyie nitakayoisema mimi hapa kabisa. Lakini ndio mkombozi wa hili *target* wa hii mliyokwenda nayo.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo na hili mimi naliseMEA sana lakini watu hawaoni nini faida kwa sababu mimi nikisema kitu kina faida, sisemi kitu ambacho kilikuwa kina hasara, sitoona haya kulisema kwa sababu ni jambo ambalo litawenza kutufikisha pahali pazuri sana na Mhe. Waziri, akaweza kufika.

Kwanza nimpongeze kwa kupita, ninaamini akirudi kesho kutwa atakuwa tena Waziri wa Afisi hii. Kwa hiyo, nimpongeze na yeze vile vile nisimnyime haki yake, atawenza kukumbuka wakati mimi niko nyumbani nimekaa kitako. Kwa hiyo, nimegundua jinsi gani ambalo tatizo hili halishi, watu mitaani wanaelewana, hakuna mtu katika mtaa asimjue mwenzake tabia. Lakini kuna kitu kimetuletea miujiza, kimekuja miujiza na watu wamekipokea kwa shangwe zote ni Polisi Jamii.

Mhe. Naibu Spika, ukiikatama Polisi Jamii sidhani kama kesho kutwa utanambia hapa bado unazungumzia neno la madawa ya kulevyta. Polisi Jamii imo ndani ya Shehia, Polisi Jamii imo ndani ya eneo, tunajuana ukweli tuseme. Kwa sababu Polisi Jamii inamjua Juma ndio wale wale ambao kwenye nyumba hakukosi mtu mmoja kumjua mwenzake. Lakini hatujawa makini, mimi naomba sana suluhisho ni Polisi Jamii jamani. Kwaza kuwa-*train*, lazima *training* iwe kubwa, kuwa-*train* jinsi gani ya kuweza kudhibiti na kukamata, *wallah* utakula raha Mhe. Waziri toa *Programme* yako mpya Mhe. Waziri, wala usiwe na wasi wasi wowote, tena hii itakuwekea sifa kubwa sana. Kwa sababu ume-*train* kitu ambacho unawaambia.

Mhe. Naibu Spika, nimeona mfano pale Kwahani kuna Polisi Jamii ilikuwa nzuri sana, walikomesha masuala haya, ikawa Kwahani sio Jamaica tena, ikawa Kwahani sio Pakstani na Kwahani ilikuwa ni hatari, sio mchezo, hakuna mtu asiojua Kwahani. Ilikuwa pale unaliwa unga kama njungu, vitoto vidogo kabisa, hivi kina mama ukipita pale unajikamata kama unaumwa na baridi kumbe unaficha kidani chake kisichukuliwe, vijana walifanyakazi sana.

Mhe. Naibu Spika, walifanya kazi kubwa sana, waliondoa kama ukiuza unga Kwahani wakati ule ilipokuwa Polisi Jamii ilivyojishamiri hata ukiweza kuuza Mhe. Waziri, basi ujue ni jambo kubwa sana, umeuza basi kwa siri kubwa tu, ilikuwa si kitu rahisi. Walikuwa jamaa wanafanya kazi usiku na mchana wale vijana. Lakini ninashukuru Serikali imeweka ulinzi katika kiwanda chetu hichi; Kiwanja cha Watoto wamepata ajira nao pale. Sasa imeondoka haiko tena mitaani imeingizwa kwenye viwanja.

Sasa hilo moja nalo ni koseo. Lakini Mhe. Naibu Spika, tatizo letu hatuna *centre* ya ile sheria ile tukaweka, kwa sababu ukiwaweka *centre* fulani, sasa wao wanakuwa tayari macho mengi wana upeo wa kuangalia wakajua kama sasa hivi kaingiza unga na nani anataka kununua au kuuvuta unga. Hiyo moja inakosekana.

Kwa hivyo mimi Mhe. Naibu Spika, naomba sana Wizara hii tusingoje tukasema si Wizara yangu, hili ni suala la Polisi, si la Polisi, tumetia jamii na jamii mionganoni mwa sisi, tunatafuta tiba, tiba mkombozi. Vijana wanateketea Mhe. Naibu Spika, tena kwa sababu vijana haujulikani usiku wala mchana, wao wanalala tu. Kwa sababu unga unalaza tu *full time*, utakaa naye masaa machache mwenzako anakoroma eeh! hayupo. Maisha gani haya ya kuishi.

Sasa mimi ninakuomba sana Mhe. Waziri wangu tiba ipo, shauriana na Katibu wako ye ye atafanya *modification* ya mambo ili tuweze kupata jambo lenye uhakika na kuweza kulinda. Mhe. Naibu Spika, hali inaumiza sana kwa sababu unga *wana-frame* kitu ambacho wao mambo mawili; *kwanza wana-frame* wapo ndani ya Marekani, *wana-frame* wamo ndani ya Uingereza na ukitaka uudhike, kamuudhi pale umshiture atakuua, haoni tabu kuua. Wako tayari hata kuua mtu kwa kete moja, maisha gani.

Sasa mimi ninafikiria jamani hatupo *serious* na masuala kama haya ambayo ni masuala ambayo Mhe. Naibu Spika, yanatekelezeka, yapo mepesi kabisa. Kama tutakuwa na mfumo huo, tutaujenga hasa, tuwe *strong*. Mimi ninaamini *wallahi* ninaamini sana. Hii leo nimesema nichangie kwa *style* yake kwa sababu niseme na ndani nina huruma ndani yake. Nina huruma kwa sababu *population* inaendelea, tena watoto wadogo tu na ule unaumiza kwa sababu unamuumiza hupati chafya hata kidogo, ni sumu kabisa ambayo inayotumika kwa mtu yule aliyelazwa hospitali kwenda kufanya operesheni. Sasa *imagine* wewe mtu unafanyiwa operesheni unatumiwa kile kitu, halafu mwili wote unakufa ganzi wala huhisi, niambie ye ye anayekula, hata uzazi watakuwa hawana.

Sasa kweli mtoto anatakiwa wewe uzae, unazaliwa na wewe uzae ili ukoo uendelee. Pia athari hizo zinaendelea Mhe. Naibu Spika, kitu kama hicho. Sasa

mimi naomba sana lazima tufanye *combination* nzuri kati ya Polisi yenewe na Kitengo husika cha Madawa ya Kulevy ili tufike pahali tuseme sasa basi inatosha.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana hilo nilisema kuwa nilichangie na kulichukulia muda kwa kulitengeneza. Sasa tena hiyo hiyari yenu Serikali mukisikia sawa. Lakini mimi hukaa, unajua Mhe. Naibu Spika, sasa nyengine mimi hukaa tu mwenyewe basi sina kazi ninakaa kwenye *lab* yangu; huwa ninakaa ninajifikiria, ninafanya *assessment*, akija mtu kutoka Marekani atasema jambo ambalo lile lile kalisema Mhe. Mshimba, lakini ye ye anachukuliwa anaonekana *yes*, inaonekana kafanya jambo la ajabu na linakubaliwa, watu wanakwenda mbio kwa sababu kasema huyu katoka Marekani, lakini Mshimba Mkaskazini hapa linaonekana aah! si porojo tu yule.

Sasa hapo Mhe. Naibu Spika, huwa ninajiuliza *why*, tatizo ni nini. Yule kasema Kiingereza, mimi nimesema kwa Kiswahili lakini ndiyo lile lile moja tu. Sasa mimi Mhe. Naibu Spika, naomba sana tusingojee tukasemewa. Hii ni hasara kubwa Mhe. Naibu Spika, tujitahidi sana kujisemea wenyewe, na ndiyo maana ingelikuwa tunakubalika kusema wenyewe, baadhi ya mambo mimi nime-refer nimeona kweli.

Mhe. Rais wa Zanzibar ana-*take action* mambo mengi nimeyajaribu kama matatu manne, nimefurahi sana ameyaunga mkono na akayatolea ufanuzi, ameyakubali na kayatolea maamuzi.

Kisakina nilisema hapa Mhe. Rais kakubali. Rais wetu wanapanda visakina vya *benz*, na nimesikia gari za visakina vyengine vinakuja tayari vya Muscat ijapokuwa vya *left hand*, si tumepata. Sisi hatutaki upande gani lakini tumevipata itakuwa, tunafurahi navyo. *Radio call* walikuwa *traffic* hawana ya kuongezea Marais njiani lakini wamepata.

Sasa na hili suala naomba Mhe. Rais hii Polisi Jamii jamani tuitilie mkazo katika kuondosha maovu. Asikwambie mtu Mhe. Naibu Spika, tunujuana kwenye mitaa. Na wale watoto tena Polisi Jamii wameikubali vijana kabisa. Siku hizi kuna *show*. Tena nitoe mfano wa kuona uhakika lile jambo.

Tizameni yaliyotokeza njia ya Mwanakwerekwe, vijana wamejitlea, ni *free* kabisa, na mavazi yao wamekuwa *traffic* wao. Tizama maana yake nikupeni uhakika wa jambo kama inawezekana bila ya kutoa fedha kwa vijana, walikuwa wanasesaidia *traffic* pale, wanasihamisha gari kuondoa msongamano, *wallahi* wanakesha, maana yake niseme mpaka saa tano au saa sita utawakuta wale vijana wanahangaika pale. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wanastahili kupewa pongezi sana. Sasa huo mfano mdogo tu tizameni wanavyotusaidia vijana.

Sasa leo munawapa madaraka wakuu waambieni jamani Shehia hii tunataka unga usiingie, Shehia tunataka unga watu wasielewe. *Wallahi* hamutawaona vijana kama watakula unga, amini Mwenyezi Mungu ninakwambia. Useme jambo hilo uwaambie hasa, leo njooni askari jamii.

Mhe. Waziri nenda kule na Tume yako waambie hao; nenda na Tume yako katika Shehia musingoje mukaona lazima aje muhusika zaidi baada ya nyinyi, hapana, nenda kuwaambie wale, jamani eeh! tunasema tumekuja hapa kuna hili na hili, tunataka *one week*. Muone *wallahi* kama nimekuwa nitilieni *fat-ha* mara mia kwa sababu nitakuwa nimeliokoa jambo kwenye janga.

Mhe. Naibu Spika, uone kama watu wataendelea kufanya hivyo, kama watu wataingiza, siyo mchezo. Lakini hatupo *serious*. *Wallahi* Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana, tunaleta matakwimu kibao hapa, tutajenga *sober houses* zaidi ya mia haikusaidii kitu Mhe. Waziri amini kabisa, wala asikudanganye mtu. Lakini kama hatukuangalia kwenye Shehia utajidanganya tu Mhe. Waziri, *wallahi* utajenga *sober houses*, utajenga nyumba kubwa ya kufanya nini, akitoka pale anarudi wapi. Sasa wewe jiulize.

Huyu umeshamtia *sober house*, na kweli wengine wanapona *alhamdulillah rabil alamina* Mwenyezi Mungu anawaongoa moja kwa moja, lakini anarudi kwenye Shehia. Yupo huyu muuzaji huyu.

Lakini leo unamtoa kule *fresh*, anajua duu! hawa watwana Polisi Jamii watanipiga mimi hawa. Na huyu jamaa anasema duuh! mimi siyo wananijua bwana siku hizi maendeleo yangu kila siku ninang'ara. Kwa hivyo jamaa sasa hivi mimi watanidhibiti. Tayari wewe mwenyewe unajitisha.

Naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana hebu nikubalieni hii rai. Ni rai tiba peke yake. Leo nenda hospitali wateja kibao, zamani walikuwa wakienda hospitali wateja kuwadhalilisha akinamama wanaolala, wanaiba na kufanya kila mambo. Lakini leo nishukuru kwa kuwa kampuni ile ipo, *security* ile ya *private* kidogo masuala hayo yameondokana na mambo kama hayo.

Sasa hivi dawa ambazo zinawapunguza makali wa kuwepo *mental*. Mutawalisha mpaka mtawavimbisha wale isipokuwa ni bure tu, atanyweshwa watavimbishwa anarudi tena kwenye Shehia.

Sasa niliona mimi Mhe. Naibu Spika, nimalizie hapo kwa kuendelea kwengine, ninaomba sana jambo zuri jipe mwenyewe, usingoje ukapewa kwa sababu ukingoja utapewa na mtu akasifu utakaa miaka mungi. Hasa Zanzibar, hakupi mtu sifa hapa, ama majungu utachoka. Majungu utapewa mengi sana tu kila aina, hiyo

ndiyo kawaida yetu lakini suala la kukusifia wewe mtu haiji. Sasa nenda kule chini kamwite Sheha nioneshe kikosi chako cha Polisi Jamii na Tume yako ya Madawa ya Kulevy, weka mikakati yako twende zetu mbele kwa mbele, tutashinda tu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Mimi sina wasi wasi kwa jambo hili, unaweza ukashinda tu.

Mhe. Naibu Spika, ninaingia suala la ukurasa wa 39 la walemavu. Mhe.Naibu Spika, na mimi nina ushauri mmoja mzuri sana. Mara nydingi sana hata sheria hizi zimeanza kutoka huko Ulaya zikaja huku Afrika. Hili tukitaka tusitake tubadilike.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu sasa hivi Ulaya wana sheria kali sana zinazowajenga wenzetu walemavu. Lakini ninasema ninaona kulitumia hilo jina, niseme kuwa ni wapungufu wa viungo labda niseme kitu kama hicho. Tena wana sheria kali Mhe. Naibu Spika, tena wanahifadhika sana, lakini sisi hapa kwa nini hatufanyi hivyo, kwa vipi basi, nitaanza kutoa vitu.

Mhe.Naibu Spika, tusione tabu, kuna tabu ya kurahisisha ndugu zetu kwa sababu nikasema tusione tabu. Wenzetu sasa hivi wana *system* zile za vigari. *Automatically* vile vigari vinavyotiwa *charge*, tuwarahisishie hata kimoja kimoja sana. Tutampa mtu kigari cha *wheel chair* mpaka lini Mhe. Naibu Spika. Tuondokane na suala la *wheel chair*.

Hapa nimeona kwenye picha yako umewapa Mhe. Waziri *wheel chair*. Ni sawa unawapenda Mhe. Waziri na wala sikatai, ndiyo mwanzo tunaanzia hapa, lakini tugeuke Mhe. Naibu Spika, suala tena la kuwapa *wheel chair* halifai, tuondokane na wakati.

Sasa hivi wenzetu Ulaya huko wametengeneza vile vidubwana wala havitumii petroli, aah! nenda tu pale tia *charge* yako kwa muda fulani anajua masafa fulani kitanifikisha weka vitu nenda zake, wapeni hivyo musione tabu na twende na wakati. Leo tutawapa *wheel chair* mtu anakwenda munamtoa vijimbi, kwani analima yule.

Mhe. Naibu Spika, hili suala linasikitisha sana. Mimi ningeomba sana bado hatujawasaidia sana. Ninaomba sana Mhe. Rais anisikilize hasa katika jamii. Umoja ni ngao kwa sababu katika familia lazima wapate watu wa aina hawa, wewe jione kama kwenye familia yako mtu kama yule yupo unamuensi vipi. Lakini watu wengine wanawadharau, wakati mwengine wana shida watu na sheria hizi. Mwanasheria ninaomba sana hebu tutafute sheria ambazo sasa hivi hawa wanaopita kuwadhalilisha. Unajua kuna sheria nyengine zinatisha, kwanza mbadiliko wa sheria tuliokuwa nazo zipo nyepesi sana. Mtu anafika anamdhalihsa mlemavu anamnyanyasa, hamuhudumii ipasavyo anamfunga

minyonyoro. Halafu leo tunajua Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kucheka maana yake huyu mkali. Wewe ulifungwa mnyonyoro.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri weka sheria kali, wala usifanye mchezo. Jamani hizi sheria nyinyi hamuziangalii. Nenda Ulaya, nimekwenda Spain siku moja jamaa alitaka gari mlemavu mmoja mwenye kigari kidogo, *wallahi* nijilize kwa nini yule kashuka mbio kwenye gari anakwenda kuangukia, maana yake mzungu anaangukia kavaa vizuri anapiga magoti anakwenda kumuangukia kwa kuwa nini, kamkosea tu hakumponda. Nikauliza pale, nikaambiwa duuh! yule angemuenzi maisha.

Angemlipa maana yake angemuenzi mpaka kufa kwake, sheria wenzetu inavyofanya kazi. Sisi tupo *simple*, wanapondwa na gari na baiskeli zao maskini ya Mungu, basi mtu akienda anaambiwa aah! kwa kuwa sisi hatuna hapa hatuna mapana, mmoja alisema Mheshimiwa hatujaangalia kuweka programu mapema au ramani zetu mapema za mipango miji, lakini kule wenzetu wanazo. Kwa sababu utakuta vile vigari vyao vinapita njia maalum. Lakini basi ikiwa ni hivyo tumekosea, tena ndiyo tuwadhalilishe. Sheria ninaona tuiangalie upya.

Wanawake wanazalishwa ovyo ovyo haki ya Mungu. Mungu atunusuru rabi salama yarabi Mwenyezi Mungu atuokoe na jambo hili. Maana yake leo wewe unakwenda kumdhalilisha. Nimeoneshwa jimboni huko mlemavu kaza, sasa ninajiuliza huyu wanamchukua saa ngapi. Huwezi kuamini Mhe. Naibu Spika, huyo mtu aliyezalishwa, watu ninakwambia sijui namna gani.

Sasa kungekuwa na sheria na wakati yule mtu keshajulikana kamzalisha bila ya kumuo, kwa sababu na ye ye anayo haki ya kuolewa yule, muoe hakuna tatizo. Kwani hakuna watu wameoa watu wa aina hiyo, mbona wapo watu wengi na wanastarehe vizuri *alhamdullahi*, tena wanapata thawabu kubwa sana. Tena wanaume tuwaoeni hawa tusione tatizo eeh! lakini tukienda hivi hivi. Mhe. Naibu Spika, naomba sana sheria iweze kufuata mkondo wake. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi kuna *designs* za *stick*. Zamani nyinyi mumezoea ile *stick* refu *white*, siku hizi ina-*indicator*. Hawa waliokuwa hawaoni *automatically* ukiona kile kitu kinawaka na wengine kuna kitu ukigonga kinalia *automatically* kinamwambia hapo kuna kitu ambacho sicho, twendeni na wakati.

Leo Zanzibar lazima twende na wakati. Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ambayo nao tuwape faraja kabisa. Tuzitafute hizo *stickers* zenye kuonesha *indicator automatically*, kwa sababu ile siku unamuona yule, duu! yule mtu ana tatizo fulani, unaanza kumu-*orange* kumkwepa kabla ya kumfikia pale.

Sasa nimeona Mhe. Naibu Spika, hizi *tools* za kizamani tuziondoe, tuwape haki zao na wao tuwafurahishe. Majengo yawepo ya kuwawezesha kupanda, twendeni na wakati sasa hivi jamani, tugeuke Zanzibar hiyo ya zamani tuondokane nayo. Mhe. Naibu Spika, hilo ni jambo ambalo litakuwa ni faraja sana.

Halafu *population* ya kazi na wao vile vile twende nao sambamba, tena wapo wasomi wazuri sana. Kuna mtoto kule kwetu Kwahani mzuri msomi huyo hatari kabisa. Nimesema huyo kama hakupata kazi mimi nitapigana. Ni mtoto kasoma vizuri sana, hana mguu maskini ni mwanamme. Sasa mimi ninasema Mhe. Naibu Spika, nao tuwe Mwanasheria tuangalie sheria za kazi, tuwaone vipi na wao *advantage* ya kuweza kupata nao asilimia zao kwenye kazi.

Sasa tugeuke, hata kwenye Baraza la Wawakilishi tuwaangalie na wao tuwaingize humu, wakiingia humu Mhe. Naibu Spika, kwa asilimia na wao wana akili nzuri, wanapungua baadhi ya mambo tu, lakini *brain* zinafanya kazi, wataweza kutoa ushauri mzuri kwenye Serikali na kuweza kupigania haki zao ili twende nao sawa.

Mimi ninaamini patakuwa hapatoshi hapa, waingizeni watano sita, saba, hapatoshi, watatusaidia vizuri katika kujenga hali halisi ya sehemu yao.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi ninasema kuwa sheria ya Zanzibar tuiangalie mapitio yake yakoje ili tuweze kuwasaidia hawa ndugu zetu wenye mapungufu kwenye sheria ya ajira, ili aingalie jinsi gani ambavyo tunawa-*favour* vipi, hata katika masomo Mheshimiwa Katika mgao huo wa masomo tusiwaweke nyuma, tuwape mikopo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri au Mhe. Waziri ajitayarische aje kuniambia ni wangapi wenzetu wenye upungufu wa viungo wamepata mikopo ya kwenda kusoma, hilo aje kuniambia kabisa, wala asije kuniambia watatu au wanne, sio kweli wala sikubaliani nacho hicho kitu, ni lazima wapewe nafasi, kwa nini tunawanyima ni haki yao, ni Wazanzibari na ni Watanzania ni lazima wapewe haki yao.

Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, ni haki yao lazima tuwakabidhi. Ni hatari sana, tusifanye mchezo. Kwenye michezo *alhamdulillah* wanasaidiwa, wanatuletea medali, nyinyi hamuoni? Wanaitangaza Zanzibar katika michezo, tuwapongeze sana wanaleta medali za dhahabu, za fedha na kila kitu, halafu leo mnataka kuwabagua.

Mimi naona Mhe. Naibu Spika, sheria za kazi ziangaliwe na sheria za nchi ziangaliwe ni jinsi gani tunawenza tukawasaidia, mimi naamini linawezekana hili suala na likafanyika bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye mazingira. Mazingira *wallahi* tunaimba tu, hatujawa wakweli kufanya mazingira.

Mhe. Naibu Spika, tulisema sheria iwe elekezi vizuri, itoe vielekezo vizuri kwa mujibu wa sheria ya mtu akikutwa na matatizo basi sheria iweze kumuhukumu.

Kwanza nimuulize Mhe. Waziri katika sheria tuliyoipitisha juzi, waziri muhusika sijui keshachaguliwa au sijui imeshatiwa saini, kwanza niulize na kama hajitiwa saini basi naamini Mhe. Rais alivyokuwa msikivu *wallahi* ataitia saini kesho itakuwa tayari hapa na Mkurugenzi muhusika atawenza kuchaguliwa mara moja ili aweze kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, mazingira bado hatujawa tayari. Wenzetu hapo jirani sio mchezo nimeona mwenyewe. Nilikwenda kumtetea mtu fulani Mr. X sitaki kumtaja, na mimi nilikwenda. Nilisema kule labda Zanzibar tu, nikavaa suti yangu nikaenda kule buti inalia chuma chini utafikiri nini, jamaa wanangoja tu, nilipofika kule sio mchezo unajua kama ni sheria. Tumeharibu mazingira tunaambiwa, mumeharibu mazingira ya bahari, tizama hatari. Mumeharibu mazingira ya bahari, nyinyi mnahatarisha viumbe vya baharini, faini yake shilingi milioni 10. Mimi sikujiamini, nikasema labda anazungumzia yule Mwenyekiti kama hanioni, hanitizami wala haniiti Mheshimiwa tena hapo, hakuna mheshimiwa hapo kuna hukumu tu ya kesi.

Kwanza kikao kile unakiitisha wewe unalipa 1.5, halafu baadaye unakaa unahukumiwa kidonda na msumari wa moto ndani yake *5 millions* uweke pale. Basi tukalia huku na huku tukaambiwa *5 millions* zikatoka *cash* pale kwa suala la mazingira.

Leo Mhe. Naibu Spika, watu wanachimba mchanga hakuna hata mti mmoja. Nenda kesho Mhe. Waziri na jopo lako ukaangalie nani kapanda mti, katizame jangwa linavyoteketea huko.

Mumewaambia nyinyi watu jamani mkishachimba mchanga pandeni mti, hawapandi mti hatuko *serious*, ndio maana nikasema hatuko *serious*. Kamkamateni mchimba shimo kama hakupanda mti mpige faini mnangoja nini.

Mimi kitu kinachonisikitisha Mhe. Naibu Spika, siku hizi nitakuwa sichangii, naona napoteza nguvu zangu bure tu. Hapa wangkuwa wazungu mimi wangenihifadhi sana, wangesema huyu Muafrika ana akili kaipata wapi huyu, halikusoma, wangenihifadhi mimi, sio masihara Mheshimiwa, wangenihifadhi mimi wazungu (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini leo humu munanidharau kwa sababu kitu ambacho nawaambia ni cha uhakika. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, watu wanachimba vifusi, katizameni mahoba yanatuulia watoto wetu ndio hayo sasa mfano Kwerekwe kule, nini historia ya Kwerekwe pale, walichimba watu vifusi na michanga pale sasa yakaja kufanya mahoba pale. Lakini pale pangepandwa miti ungeona, kwa sababu rutuba mti ukiupanda ule basi unarutubisha wenyewe kama hamira umeutilia, unakuja zake na ile ardhi inapanda juu ndio maana yake mti kupanda, lakini watu wameachiwa kabisa na wanaendelea kuachiwa. Mhe. Naibu Spika, hili suala linasikitisha sana kusema kweli.

Mimi namuomba sana Mkurugenzi muhusika ashuke chini, mvua hizi ni lazima aende awatie watu kamba anaona tabu gani.

Leo Donge kule nenda haijulikani hii ardhi ya ngapi, mtu anachimba mpaka anakuta maji, hata ile *level* iliyowekwa kwa mujibu wa sheria ya uchimbaji mnaiacha kabisa, mtu anachimba mpaka anatoa maji sio kitu cha mchezoo hicho. Ardhi yetu mnajua hii tuko juu ya maji sisi hapa, sasa mtu anachimba mpaka kufika huko.

Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, Idara ya Misitu na Mazingira hebu shikamaneni vizuri, watieni adabu hao, mkiwatia adabu hao basi watakubaliana na sheria za mazingira.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Waziri kwa hili usilifumbie macho, kwa sababu mabadiliko ya nchi yanatokana na uharibifu wetu sisi wenyewe wananchi. Ndio maana tukasema Mheshimiwa, kwa sababu ukiangalia mtu siku za mvua ndio anapokwenda kumwaga taka, siku za mvua mtu ndipo anapochimba karo yake anaitoa uchafu anakwenda kumwaga nje.

Hebu Mhe. Naibu Spika, hupati maradhi hivyo au haupati msingi kujifunga hapo, basi mtu anatizamwa tu.

Sasa hizi sheria huwa najiuliza tunazitunga za nini Mhe. Naibu Spika, hebu tukubaliane na suala hili. Sheria hii sasa hivi haijapitwa na wakati kwa sababu tumeitunga juzi tu, kwa hivyo naomba sana msimamizi asimtizame nani.

Unajua ni kweli nakubali moja na sisi Waheshimiwa ndio tunaoharibu mazingira, hilo nakubali sana wala sina tatizo lolote. Maana yake leo nitamuendea bi Fatma pale nitalia wee Mhe. Waziri mtu wangu huyu, maana yake mimi ataninyima kura sijui nini na nini. Ninalomuombea ni hatari, na mimi baadae kwa kizazi changu.

Bi Fatma ananijua nampigia debe hapa bajeti yake ipite vizuri, watu wanaipitisha atatia wino tu kusaini, Katibu Mkuu mwalimu wangu atasema daa! mwanafunzi wangu, anatia saini huku anafumba macho lisilobudi daa! naliondoke. Tunasahau zile hatari. Baadae sasa ndio duuh!

Sasa kuna mambo mengine Mhe. Naibu Spika, lazima tuyaangalie. Ningombwa sana kuwa sasa tuwe na mikakati, twende na mikakati kwa mujibu wa sheria na utawala bora wa nchi yetu. Anayechimba mchanga ahakikishe amepanda miti, kama anavyoona raha ya kutanua eneo, maana yake wanaona raha Mhe. Naibu Spika, wanachimba tu, na yeze mumlazimishe apande miti kwa lile eneo alilolitanua, *wallahi* tutastarehe sana. Hilo moja.

La pili, wajengaji wa barabara. Mhe. Naibu Spika, ukilitaka jambo linakuwa, hapa kulikuwa na Uwanja wa Ndege, wakati ule mimi nilikuwa Mwenyekiti. Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na shimo ile nikiingia mimi basi naangalia juu huko. Leo kaliulize lile shimo liko wapi. Mimi ninayo historia nilipiga picha pale, mwenzangu Mhe. Subeit Khamis Faki pale anaitikia kwa kichwa kama anayepungwa, anafahamu ndio nilikuwa Mwenyekiti wake mimi.

Mhe. Naibu Spika, lile shimo sio mchezo, leo halipo wala huamini kabisa, kwa sababu gani pale sheria imefuatwa. Kwa sababu ni sehemu ya viwanja vyta ndege ni hatari. Tizama mule sehemu nyengine tunakwenda kutoa kipaumbele kama ile, lakini kule kwengine kunakofanya mabwawa wakafa watoto wetu.

Juzi mwananchi wangu mmoja maskini ya Mungu kapoteza maisha katika hayo mabwawa ya michanga huko sehemu za kwetu, kapoteza maisha. Jamani Mhe. Naibu Spika, mimi nimeona hili suala niliseme ili tuweze kufika pahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri na watendaji wake niwapongeze sana na hasa katika mfumo huu wa *PBB*, lakini niseme kitu kimoja tu, kuna malengo humu wamepanga mazuri.

Mhe. Naibu Spika: Hicho ni cha kumalizia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Namalizia, ndio nakwenda huko tena natoa taaluma kidogo.

Mhe. Naibu Spika, programu hii mimi naona Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tuulize, mimi niwaaulize tu kuwa katika hii miaka mitatu hizi programu mlizotupangia upatikanaji wake wa fedha, labda nichokoze kama hivyo tu, lakini siingii ndani sana, kwa sababu nimesema ni programu nzuri sana, kwa sababu tayari wametuonesha jinsi ya upangiliaji wa hizi *activities* ambazo zitakuja

kufanywa katika miaka mitatu. Tumeona hivi hivi wazi. Lazima wenzangu muwe wajanja katika kuuliza hizo fedha zenyewe zitatosheleza katika hizi programu tatu. Labda nikufundisheni ujanja mmoja. Tuwaalize hizi fedha walizozipangia katika hizi *activities* ambazo ni za miaka mitatu. Lakini sasa hivi tutakuwa na awamu moja tu nikwambieni ukweli. Awamu moja *very secret* tutaweza kuzipata tukaweza kutumia.

Waziri wa Fedha *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akujaalie na nimuombe sana Dkt. Shein kwa hili wala sio siri hapa. Haidhuru sehemu moja ulichukua kwangu mimi, maana yake mengine na wewe unisifu hutaki, kwa sababu hapa nilikuwa nasema sana tuwe na programu, tuwe na mpangilio katika bajeti zetu za miradi ya utekelezaji, tuone mradi gani tumefanikisha na mradi gani hatujafanikisha.

Hii umenkuu kutoka kwangu Mhe. Waziri ukweli nikwambie, lakini sio vibaya umetanua zaidi ujanja wa mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Rais *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akimjaalia akifanikisha basi aturejeshee Mhe. Waziri wetu, kwa sababu ana sifa moja kubwa sana, sio mdokozи. Sijasikia mimi hata siku moja pahala kuwa kala fedha, hilo hana Mheshimiwa *alhamdulillah*.

Halafu la pili nimshukuru sana Mhe. Waziri ni mtiifu, anasikiliza maneno ya Mzee Ali hapo ndio mshauri wake anamsikiliza anavyomwambia.

Mhe. Naibu Spika, mimi naikubali hii hotuba ya Mhe. Waziri bajeti yao, niwashukuru sana na naikubali, na hasa wa Katibu Mkuu wangu nayakubali kwa asilimia mia kwa mia. Niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe, ikubalini jamani, muitetee kwa kadiri mnavyoona kwa mujibu wa sheria ya muundo huu, msije mkatoka mtachekwa.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, jioni hii ya leo kunipa fursa na mimi nichangie hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi napenda niungane na wenzangu, kumpongeza sana Mhe. Waziri, kwanza kwa uwasilishaji wake.

Pili kwa utendaji wake na mimi nampongeza kwa sababu ni mwanamke lakini anaweza na anafanya kazi, anajituma, anafanya kazi kufa na kupona mwisho wa uwezo wake. Kwa hivyo, nampongeza kuwa ana juhudhi na anafanya kazi zake kwa umakini mkubwa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda nimpungeze Katibu Mkuu, pamoja na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wake wote. Kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Taifa.

Kwa hivyo, kwa kweli Mhe. Naibu Spika, Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni moja kati ya wizara ambazo tukienda pale katika ukaguzi wetu wa kamati, huwa wanatupa ripoti tunaridhika. Kwa kweli wanajitahidi kuyafanya kazi yale maagizo yetu tunayowaagiza, kwa hivyo nawapongeza sana na *Inshaallah* nawatachia waendelee kuwa na mafanikio mema.

Mhe. Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo sasa nataka nianze hapa kwenye watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu kama wenzangu walivyotangulia, ni watu muhimu sana na ni watu ambao wana haki ya kuenziwa.

Kwanza naomba tujipongeze sana Wazanzibari, sote kwa jumla tujipongeze sana. Kwa sababu wenzetu kule Tanzania Bara kuna wimbi ambalo limeibuka kwa hawa wenzetu wenye ulemavu ambao ni albino. Wenzetu wanawaua hawa ndugu zetu, wanawakata mikono na kuwafanya vitendo mbali mbali ambavyo sivyo, kwa upotevu na kwa dhamira tu eti ukipata kiungo cha albino utatajirika, hasa kwa hiki kipindi tulichonacho, au utapata mali au utakuwa mkubwa. Kwa hivyo, kwa kweli ni imani potofu.

Kwa bahati nzuri kwa kweli sisi visiwani haijawahi kutokea na ninaamini kwamba haitatokea. Kwa hivyo, sisi Wazanzibari tuna haki ya kujipongeza kwa hilo.

Baada ya kusema hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi napenda nimuulize Mhe. Waziri, kwa sababu kama alivyozungumza kwenye bajeti kwamba kuna mfuko ule wa watu wenye ulemavu, na mfuko huu ulianzishwa na nilimuona Naibu Katibu Mkuu wetu wa chama, Mhe. Ahmeid Mazrui alikuwa ni msimamizi wa mchango wa mfuko ule. Sasa napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri, je ule mfuko unaendelezwa, unachangiwa tena au baada ya michango ile iliyoendelezwa ndio imekoma. Je, ule mfuko kama unaendelezwa bado umeshafikia asilimia ngapi na umewekewa lini matumizi yake yataatumiwa. Hilo ni moja.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina masikitiko sana kwa sababu watu wenye ulemavu hatuwatendei haki, hasa mimi nailaumu serikali yetu kuwa kweli hatuwatendei haki. Kwa sababu mpaka leo hii miundombinu yetu sio rafiki kwa watu wenye ulemavu, barabara zetu hazijawekwa kama hii ni barabara ya kupita watu wenye ulemavu, hii ni ya magari na hii ni ya watu wenye balskeli.

Majumba yetu na maofisi yetu tunayojenga bado hatujawawezesha watu wenye ulemavu kufika katika maeneo ambayo yanakusudiwa.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa hili, sasa hivi awe na nguvu kubwa za kuwatetea watu wenye ulemavu, kwamba ofisi yoyote itakayojengwa basi lazima ijengwe ofisi hiyo ikiwa inamuwezesha mtu mwenye ulemavu kufika katika maofisi yote.

Mhe. Naibu Spika, suala hili tumeshalisema sana, lakini katika kulisema kwetu bado halijachukuliwa hatua.

Jengine katika bajeti iliyopita mimi nilisema hapa. Je, katika hii elimu kuna kipaumbele gani tunachowapa watu wenye ulemavu, ili na wao waweze kujumuika na wenzao ili kuona kwamba kuna kipaumbele wamepewa watu wenye ulemavu, lakini bahati mbaya sana sikupata jibu lolote la kuridhisha katika kipindi kilichopita.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ukienda kwenye elimu mjumuisho ni nzuri sana elimu hii, lakini sasa kuna watu wengine ni viziwi, kuna watu wengine ni vipofu, kuna watu wengine ni bubu hawasemi. Sasa kama atakwenda tu ile ile elimu mjumuisho, kunakuwa na ishara gani ya kumuonesha bubu ili aweze kuelewa katika masomo yale na aungane na wenzake. Maana ingekuwa kuna mtu ambaye anaashiria kama tunavyoashiriwa kwenye Baraza la Wawakilishi, basi tungekuwa tumewasaidia.

Elimu mjumuisho ni nzuri kweli kweli, lakini je tunawasaidia vipi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba na hili, wewe ndiye mwenye dhamana, kama wewe ndiye mwenye dhamana basi lazima uwe mtetezi mzuri wa kuwatetea hawa ndugu zetu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze, ni hili ambalo linazungumzwa na watu wote katika mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Spika, kwanza jana nilipata faraja alipokuwa akijibu maswali Mhe. Waziri kuhusu hili suala la mabadiliko ya tabia nchi kwenye maeneo ambayo yanaingia maji ya chumvi. Maeneo hayo ndugu zetu walikuwa wanalima sasa hivi hayalimiki tena kwa kuingia maji ya chumvi. Nilipata faraja baada ya Mhe. Waziri kusema kwamba kuna mradi ambao unajumuisha Tanzania Bara pamoja na Zanzibar, na akataja yale maeneo ambayo yatafaidika na miradi ile. Nilipata faraja sana na nilishukuru sana na nikaomba *Inshallah* kwa Uwezo wa Mwenyezi Mungu ipo faraja inakuja.

Namuomba Mhe. Waziri hiyo miradi itakapofika basi iwe na wasimamizi wazuri ili kuweza kutusaidia kuondoa matatizo yale.

Suala jengine ninalotaka nilizungumze ni suala la mazingira. Suala la mazingira pamezungumzwa mengi, rafiki yangu Mhe. Mshimba pale amesema sana. Amesema kwamba kuna maeneo ambayo yanatengwa kwa ajili ya utengenezaji wa barabara wanachimba fusi. Lakini maeneo yale yakishakuchimbwa ndio basi yameshachimbwa. Bahati nzuri sheria yetu tuliyokuwa nayo ilikuwa haina meno, Waziri alikuwa hawezi kumbana mkandarasi anayekuja.

Mhe. Spika, ndio maana sisi maeneo yetu kama maeneo ya Mhe. Hija Hassan, Mhe. Saleh Nassor, maeneo ya kwetu sisi na maeneo mengine ya hapa Unguja. Kwa sababu sheria yetu ilikuwa haina meno ya kuwabana wakandarasi, basi tulibakia baada ya kwisha kuchimbwa yale mashimo ndio yamebaki hivyo hivyo.

Mwisho walikuwa wanafanya ujanja wakandarasi wanakubaliana kwamba wakishakuchimba watarudisha lakini bahati mbaya mno hawarudishi wanaacha vile vile. Sasa kwa sababu sheria iliyopo sasa hivi itakuwa inabana, ina meno inauma, inambana mtu anatekeleza kabisa.

Nafarijika na *Inshallah* Mwenyezi Mungu aijaalie kama Rais hajaitia saini na mimi nasema kama anavyosema Mhe. Mshimba basi aitie saini sheria ile ili iweze kufanya kazi zake.

Lakini wakati huo huo mimi nimuombe Mhe. Waziri, sisi wengine hatujapata kutembea sana kwa wenzetu duniani huko, lakini nyinyi mnaotembea na sisi tunapofika pale padogo, mimi Mheshimiwa tulipokwenda China nilikuta siku moja linapita gari lina mjiti mzima na mashina yake yote, na mijiti inafika huko, nikiuliza naambiwa kule mjiti uking'olewa hapa basi unakwenda kupandwa sehemu nyengine, hakuna kukata mjiti ukapotezwa. Ule unang'olewa eneo hili unakwenda kuwekwa sehemu nyengine.

Kwa hiyo wenzetu wanatunza sana mazingira na wanayaheshimu sana mazingira. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri na sisi tuwe na utaratibu wa kupanda miti.

Huku nyuma kulikuwa na *kata mti panda mti*, lakini sasa hivi ule msemo unaosema *kata mti panda mti* haupo. Sasa namuomba Mhe. Waziri sana, watu wameitikia kwanza upandaji wa miti lakini wanapanda miti ya biashara, wanapanda minvinje, ikikuwa watu wanakata wanauzu, sio mbaya. Hata kule kwa wenzetu Tanzania Bara wanapanda miti wanauzu lakini wao wanapanda sana miti ya mbao wao. Sisi kwetu utaratibu ule wa kupanda miti ya mbao hakuna.

Namuomba Mheshimiwa kuwe na utaratibu wa yale maeneo wanayochimba kifusi iwe ni endelevu hasa, iwe ni sheria hasa kwamba ikishang'olewa wakishakuchimba fusi au wakishakuchimba mchanga iwe ni utaratibu na iwe ni sheria hasa ya kupanda miti, kwa sababu ile miti kidogo itarudisha ile haiba ya lile eneo, isiwe ni hiyari iwe ni lazima kupanda miti, kama ni Kampuni ilazimishwe ilipe fidia watu wapande miti warudishe eneo lao, kuliko kuacha mabaya kama vile. Kwa sababu inakuwa nchi inatisha ovyo ovyo, haionekani, kama vile wanavyochimba kule kwetu mashimo ya kutisha hasa.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri, na utaratibu huu wa kupanda miti uonekane kama ni utaratibu endelevu. Aidha iwekwe tarehe maalum kama ni wafanyakazi wa serikali au wafanyakazi wengineo, iwe ni siku ya kupanda miti.

Kuna siku ya kupanda miti duniani, itumiwe kwa ajili ya kupanda miti hasa kikamilifu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze kidogo ni suala la madawa ya kulevy. Suala hili Mheshimiwa ni sugu sana, na bahati nzuri hili suala linafanyiwa kazi lakini unayemfanyia kazi ni mwanadamu na mwanadamu siku zote tunasema ni mzito, ukipita huku ye ye anapita njia nyengine.

Kwa hiyo Mheshimiwa suala hili la madawa ya kulevy ya bado ni tatizo katika nchi yetu. Bahati nzuri kila siku mimi nasema madawa ya kulevy sio unga tu, kuna na madawa mengine ambayo tunayadharau lakini yana taathira kubwa kwa vijana wetu na tunapoteza nguvu kazi kubwa ya vijana wetu. Namuomba Mhe. Waziri bado namuomba Mhe. Waziri ashirikiane na vyombo vya ulinzi kuona kwamba suala la madawa ya kulevy linasimamiwa kikamilifu.

Mhe. Spika, pale tuliambiwa kama kulikuwa na choo ambacho kilijengwa Uwanja wa Ndege kwa ajili ya kuchunguza mtu kama katuhumiwa ili aende. Je, suala lile lilifikia hatua gani, lipo, ni endelevu au ndio likwama pale pale, hilo ni suala jengine ambalo nilikuwa namuuliza.

Suala jengine ambalo nataka nimalizie, Mheshimiwa sitaki niwe na mchango mkubwa kwa sababu mimi ni Mjumbe wa hii Kamati, mengi tumeyazungumza kule. Mheshimiwa ni suala la nyumba za viongozi wetu. Hili suala kwa kweli linatudhalilisha kidogo na linaidhalilisha na serikali. Naiomba sana serikali, haiwezekani Kiongozi Mkuu kama Makamu wa Kwanza au Makamu wa Pili, au Rais mwenyewe akodiwe hoteli, hata kiusalama haikai vizuri.

Leo Makamu wa Kwanza akienda Pemba ana nyumba kakodiwa, Makamu wa Pili akienda Pemba ana hoteli kakodiwa, Makamu wa Kwanza akienda Dar-es-Salaam

anakodiwa hoteli, Makamu wa Pili akienda Dar-es-Salaam ana nyumba kama nilivyo sema jana ni chakavu, chakavu, kwa sababu sisi tumekwenda tukaitizama. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa serikali ione kama kuna umuhimu mkubwa wa kuwapatia viongozi wetu hawa makaazi ambayo yatakuwa ni makaazi ya kudumu yenye usalama na yalikuwa sio nyumba za kukodi au hoteli za kukodi.

Hotelini ni hotelini, hotelini viongozi wetu waende wakakae wakiwa huko nje ya Tanzania ni haki yao wakae kwenye mahoteli, lakini ndani ya Tanzania hii yaani Zanzibar na hapo Tanzania Bara, wakodiwe hoteli, kusema kweli inakuwa haipendezi hata kidogo, na hata kihadhi haikai vizuri. Tunaliomba sana hili lisimamiwe na serikali ili viongozi wetu wapate makaazi mazuri ambayo yanastahiki na yana usalama kwao.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwambia mimi ni Mjumbe wa Kamati hii naunga mkono bajeti hii na hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais naiunga mkono mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kupata nafasi ambayo leo nina machache tu ya kuzungumza juu ya hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, huyu ni Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji ni hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii kwa bahati nzuri ni wizara iliyokuwa ina taasisi ngumu zinazowagusa wananchi moja kwa moja, na nyengine zikileta athari kwa Taifa, uharibifu wa mazingira, madawa ya kulevyia, Ukimwi na ulemavu; yote kuwekwa katika Wizara moja ni mambo mazito kabisa.

Lakini nitoe pongozi za kipekee kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na watendaji wake wote kwa namna walivyo jitahidi na kuonesha mabadiliko ya maendeleo kwa taasisi hizi tokea kuasi siwa kwa Ofisi hii.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa Idara ya Mazingira.

Bahati nzuri hivi karibuni nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC), tulifanya ziara Pemba na tuliona ni namna gani mazingira yanavyoharibika kutokana ama na tabia ya nchi au kwa kutafuta maisha kwa wananchi walioko kule Pemba.

Tuliona mfano Mhe. Naibu Spika, tulikwenda katika eneo la Uwandani ambapo kule ni eneo liliomo katika jimbo la Wawi Mwakilishi wake ni Mhe. Saleh Nassor Juma (Muasisi).

Vile vile tulikwenda Kiuyu Mbayuni na tukaangalia ni namna gani mazingira yanaathirika tena kikweli kweli, kutokana na utengenezaji wa matofali ya kuchonga, matofali yanayotokana na mwamba. Tulipohoji sana mwisho tuliondokea kuwa kwanza hawa watu wanaojishughulisha na kazi hii wanaathirika sana kiafya, lakini ni kwa sababu ya umasikini wanafanya hivyo, hawapendi, lakini kutokana na kuwa hawana kazi nyengine ya kufanya kwa mazingira yalivyo, kwa makusudi wanaona wajiajiri katika sehemu hii ya kutafuta maisha, lakini matokeo yake ikiwa ni yenze athari kubwa sana.

Kwa bahati mbaya au nzuri tulipokwenda Uwandani tulipata watu wakatupa maelezo kuwa wao wanajua kuwa mazingira kweli yanachafuka lakini hawana jengine la kufanya ili kuweza kujimudu katika maisha.

Nashukuru Uwandani huku Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na watendaji wao pamoja na wizara nyengine ambazo sikuzitaja hapa, walikwenda wakaiona ile hali na wakapata maelezo yote. Lakini kwa pamoja waliwaambia wananchi waliokuwepo kule na hili walilifurahia katika hali ya juu kabisa, kuwa waunde vikundi ya kwamba msaada utakapokuja badala ya kuijiendesha maisha kwa kukata mwamba na kuleta athari ya mazingira waweze kusaidiwa na kupata fedha za kuendeshea maisha yao katika njia nyengine.

Mhe. Spika, wale walilikubali suala hili wakaunda vikundi kama kumbukumbu zipo sahihi havipungui 80, ni watu wengi tu waliounda vikundi wanafika 1,200 na walikaa kwa tamaa sana, lakini mpaka tulipokwenda hakuna lolote lilofanywa. Kwa hivyo kwa sababu waliokwenda ni Viongozi Wakuu, na ahadi ilitoka na kwa sababu hili ni suala mtambuka, kwa hivyo kwa makusudi kabisa kwa kuititia Wizara hii naomba hili suala lifuatiliwe ili wale watu wasitafute maisha katika ile hali ngumu. Hawana jengine la kufanya lakini vikundi vyao viangaliwe kupatiwa misaada au kuelekezwa, lakini ilimradi waachane na kazi ile ambayo mwisho wake itakuwa ni athari kubwa kwetu.

Hapo hapo nichukue nafasi ya kuwapongeza wakaazi hawa au wananchi hawa katika jimbo hili wanaojihusisha na shughuli hii, kujitahidi sana kuyahami mazingira kwa mle sehemu zilizoharibika. Pia niiombe Wizara kwa kupeleka miche ya kutosha ili kufanya hivyo pamoja na kuwa bado miche mingi sana inahitajika.

Mhe. Naibu Spika, hili vile vile lilikuwepo sehemu ya Kiuyu Muyuni ambapo kule kazi ni kubwa zaidi, na kwa bahati mbaya ardhi yao ni ardhi ya jiwe, lakini kwa mashimo yalivyokuwa makubwa naamini muda wa siku chache huenda chumvi kwa sababu ipo karibu ikaingia na halafu mazingira yakazidi kufujika.

Mhe. Naibu tulikwenda bonde moja Ukele/Kilindini, lile ni bonde la mbali ilikuwa linapanda maji ya bahari.

Pamoja na juhudu ya kupanda mikoko kama tunavyoita lakini bado yale ni mambo ya maumbile ya tabia ya nchi na maji yanayoongezeka ni mengi. Kule kwa bahati nzuri kumejengwa tuta, lakini lile eneo la bonde ambalo linaokoa maisha ya watu 1200 hawapungui wanaotumia bonde lile na bado juhudu endelevu inahitajika.

Sehemu nyengine tulipokwenda kwa bahati mbaya jina nimelisahau lakini nafikiri ni Micheweni Mkadini maji yamepanda juu mpaka misikitini na minazi imeshaanza kufa.

Kwa hivyo aliyotwambia ni sehemu nyingi sana zinazoathirika kwa maji ya chumvi, hii ni tabia ya nchi na ni sehemu nyingi sana zinazoathirika kwa kujitafutia maisha sisi wenyewe. Sasa basi pamoja na elimu inayotolewa na juhudu inayochukuliwa, lakini bado misaada ya ziada inahitajika kifedha kutokana na maeneo yalivyo mengi sana ili Wizara hii iwe ni nia kabisa ya kuweka Zanzibar katika mazingira mazuri iweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na maelezo haya niliyoyaleta mimi, kwa sababu natoka jimbo la Mtambwe, kuna Kijiji cha Mtambwe Mkuu ni kisiwa chenye historia kubwa sana kweli kweli, na kinaathirika kwa mazingira na Mhe. Waziri alikuja na anaona iko haja ya ziada fedha kupatikana na kazi ya kitaalamu iliyokusudiwa kutekelezwa ili kijiji hichi kiweze kuokoka, kwa sababu ni kijiji cha historia na kinaliwa sana na bahari, na bahati mbaya sana ardhi yake ni ya mchanga.

Mhe. Naibu Spika, linalosikitisha Mheshimiwa ni kuwa tukiangalia ukurasa wa 21 wa kitabu chetu hapa Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 113, 284, kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 lakini hadi kufikia Machi ni asilimia, hii hesabu naona labda irekebishwe maana kuna milioni 442 ambayo sio sahihi. Lakini ni asilimia ndogo tu ya fedha iliyotolewa kwa shughuli hizi, ambapo suala hili linasikitisha. Yaani wamepata asilimia 39 tu, lakini hii hesabu iliyoadikwa hapa haikubaliani kuwa ni asilimia 39 naomba irekebishwe. Sasa ikiwa kazi ngumu inayofanywa ni kama hii na fedha zinazotolewa ni kidogo kiasi hiki, hii ni kuifanya Wizara ioneokane kuwa haifanyi kazi, kumbe ni uwezo wa kufanya kazi kifedha

haupo, kwa sababu kwa mujibu wa mazingira yake ni lazima zipatatikane fedha za kutosha ndio kazi itaweza kufanyika.

Jengine Mhe. Naibu Spika, twende ukurasa wa 34 na 35 ambapo hapa pana fedha za Washirika wa Maendeleo imetajwa ambayo fedha hii ni fedha ambayo imekusudiwa kwa utekelezaji wa kazi zilizofadhiliwa na *UNICEF* na ni fedha inayohusikana na Ukimwi.

Ukimwi ni janga kubwa sana tulilonalo katika visiwa vyetu, na vile vile katika Tanzania lakini kwa mazingira yalivyo na kwa maana ya neno Ukimwi, na kwa sababu Zanzibar ni visiwa, na kwa sababu Mtanzania anayo haki ya kwenda popote anapotaka, watanzania kwa bahati katika sehemu mbili za Muungano tumetafautiana kimila, silka desturi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Uhuru huu wa nia safi na kimazingira yalivyo na sote ni mashahidi, ni kuwa kuna mambo na hayawezi kuchukuliwa hatua kwa bahati mbaya, lakini huu ujio wa atakaye aje na kufufurika kwa watu, na wengi wakiwa ni vijana wanawake katika nchi hii, na kwa sababu hawakuja hapa kujenga kwa viwanda na kadhalika kuokoa maisha ya wananchi, wanajitafutia maisha katika hali ambayo wanayoijua wenyewe na moja naamini tukataka tusitake inasababisha kuongezeka kwa Ukimwi katika nchi hii. Ninamsikitikia sana Mhe. Waziri kapewa jambo alitekeleze ambalo Serikali hajatafuta njia ya kumsaidia.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoona kuwa Zanzibar imeingiliwa na kila siku tukitaka tusitake Ukimwi unaongezeka, sijui Serikali itachukua hatua gani kutokana na athari ya Ukimwi, kwa sababu ni maradhi mabaya sana ili Mheshimiwa tuweze kumsaidia, siwezi nikatoa ushauri wowote, kwa sababu kuna sheria za kiserikali tukiziingilia hapa bila ya kufanya marekebisho itakuwa tunafanya kosa.

Hivi mimi Mhe. Waziri ninamsikitikia sana kwa kupewa Wizara hii ambayo kwa mujibu wa Katiba hakuna sababu hata moja ya kujitetea, na wala yeye hana la kufanya likaonekana kuwa kweli Ukimwi unaweza ukaondoka katika nchi hii. Sisi Wazanzibari tumeambiwa katika Qur-an Tukufu kuwa bora nizungumze kama alivyofundisha sheikh Rufai, tumeambiwa binadamu sote tumeambiwa "*walaa takrabu zzinna innahu kaana faahishatan wasaa sabiila*". Lakini tunaletewa hiyo na vijana wetu tunawajua silka zetu, mila, desturi zetu na wao ni tofauti wenzetu wanajihami lakini matokeo yake ni kuwa Ukimwi unaongezeka.

Tuendelee na utaratibu lakini sina imani kuondoka mpaka tubadilishe mfumo, mfumo wenyewe Serikali yenye inajua siwezi nikaishauri kwa hilo kwa sababu sio kazi yangu.

Vile vile hajachoka Mhe. Waziri katika programu zake kaelekeza vizuri tu namna atakavyopambana na Ukimwi na vile vile ameomba fedha naomba kwa vyovyote vile itakavyokuwa asaidiwe, kwa sababu tunajua Ukimwi ukikupata huna pa kwenda isipokuwa ni akhera. Halafu ingeliwu maradhi yaliyokuwa hayaambukizi ingeliwu *well and good* lakini yanaambukiza vibaya sana.

Masikitiko yangu kwa hapa ni kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume ya Ukimwi iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni moja na milioni mia tatu na sitini na tisa (1,369,000,000) fedha ya Tanzania hii ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa bahati mbaya hadi kufikia Machi, mwaka huu 2015 Tume hii ya Ukimwi ililingiziwa milioni mia sita na thalathini na tatu, laki nne na ishirini na saba na mia tano (633,427,500) ikiwa ni sawa na asilimia 46. Hii ni fedha kidogo sana kupambana na jambo ambalo kuna viashiria vinaongezeka kila siku.

La kusikitisha zaidi Serikali inajua umuhimu wa kupambana na Ukimwi, inajua sana lakini Wizara hii kwa upande wa fedha zinazotoka kwenye Serikali ilikuwa Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 50 kuwa ni mfuko wa Serikali lakini mchango huu wa Serikali haukutoka hata senti. Ni jambo la kusikitisha tena sana, kwa hivyo maslahi ya wananchi wetu hasa vijana wetu naomba Serikali iweke kipaumbele, umuhimu wa kuitupia jicho Wizara kwa fedha zinazoidhinishiwa kutumika japokuwa hazitosh, *at least* waweze kuifanya kazi yao ipasavyo, kutotoa hata senti moja hili ni jambo la kusikitisha sana.

Jengine ukienda kwa upande wa programu wameweka mipango mizuri tu ya kutekeleza na wameomba fedha ziingizwe kutoka kwa wahisani wa maendeleo pamoja na Serikali, haya yaliyotokea na hasa kwa upande wa Serikali katika kipindi hiki kinachomaliza naomba kisitokee tena huko mbele, kwa sababu itaharibu programu yote.

Halafu tuliamiwi tu kuwa safari hii tunajitegemea zaidi kwa sababu hakuna uwazi wa kupata fedha kutoka kwa wahisani wa maendeleo, sijui kule kumeingizwa kwa sababu gani kama mambo yamegeuka ninamuomba nipewe maelezo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni jambo bayaa sana, tukizungumza madawa ya kulevya na ulevi wetu wa kawaida ni mambo tofauti, madawa haya ya kulevya tunajua hayatengenezwi hapa Zanzibar, yanaingizwa kutoka nchi za nje. Tumefanyiwa masemina na tumeona namna gani *communication* ya watu hawa inakwenda mpaka madawa ya kulevya yakafika kule kunakotarajiwa.

Imani yangu ni kuwa bila ya kuingia mkono wa mtu mwenye uwezo Zanzibar kusingeliweza kuletwa madawa ya kulevyta, kwa sababu ni kitu kibaya sana lakini madawa ya kulevyta kwa mujibu wa kitabu hiki, Mhe. Waziri kazungumza maneno mazuri tu kuwa atajitahidi kupunguza idadi ya watu wanaotumia madawa ya kulevyta, kwa mikakati aliyoiweka yeye mwenyewe. Lakini Zanzibar kama kweli tutaaamua tusilette madawa ya kulevyta, basi ninahakikisha hayatofika na Mhe. Waziri tutamsaidia sana, kwa suala hili kwa sababu kila mzanzibari anajua kuwa hakuna kitu kibaya kama ulevi, ukishalewa unaweza ukafanya lolote si zuri wala halitakiwi kufanya kwa muislamu yejote au binaadamu yejote.

Na haya madawa zaidi ya hayo kuna mengine yanapunguza nguvu, yanapunguza nguvu kazi, watu wanakuwa wabovu, tunapata Taifa lenye vijana ambao tunawategemea ambao hawawezi kufanya lolote, hata kusema vizuri kama wanaume hawawezi, achilia mbali wanawake.

Mhe. Naibu Spika, vyote ya hivyo watu wanapoteza pesa nyingi sana kwa kutumia ulevi huu uliokuwa hauna maana, na hakuna njia hata moja ambayo itasaidia hapa madawa ya kulevyta yasiingizwe isipokuwa Serikali kuweka adhabu kali kweli kweli, na kufanya utafiti wa hali ya juu.

Tuna askari wa kutosha tu, wala hawana idadi kuona kuwa hili linashughulikiwa ipasavyo, na baada ya kushughulikiwa ipasavyo tuone kuwa madawa ya kulevyta hayaingii, na kama madawa ya kulevyta hayaingii ninahakikisha mambo haya yataondoka.

Naipongeza Wizara, tena ninaipongeza sana kwa kuwaona wenzetu walivyo haribikiwa kwa madawa haya ya kulevyta, wakawaweka katika nyumba maalum zinaitwa *Sober Houses*, kule kuwapa taaluma na wao wenyewe kupeana taaluma na wengine wakawenza kuachana na kazi hii, hii ni kazi kubwa sana. Kwa sababu Wizara inakerekwa sana sana na tabia hii ya madawa ya kulevyta, na badala yake kunahitajika kutumia fedha nyingi kwa kutoa huu ushauri nasaha ambao umesaidia, ninaloomba Mhe. Naibu Spika, katika programu Wizara imeomba fedha ya kutosha ili kupambana na mambo haya. Hapa ninaombwa mambo mawili.

Jambo la mwanzo Serikali itafute njia ya kuisaidia Wizara kuona kuwa kama kuna watu wanahusika kwa hivyo madawa haya yapigwe marufuku na pakitokea ishara ndogo pasiwe na huruma wala pasiwe na kuoneana haya, kwa sababu rushwa ya kuoneana haya ndio rushwa mbaya sana, tuwasaidie wenzetu na tulioke Taifa letu.

La mwisho kwa sababu ya wakati ni kuwa Mhe. Naibu Spika, imezungumzwa hapa na mimi ninatilia mkazo, Waheshimiwa hii Zanzibar ni nchi ina Katiba yake,

ina Serikali yake, ina viongozi wake wakuu na watendaji wengine tofauti. Inasikitisha ikiwa leo tumefikia miaka 51 ya Mapinduzi na tunamaliza miaka 5 kama sikosei kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na tunajua maana ya Kiongozi Mkuu wa Serikali ni jambo la aibu kwa Makamu wa Pili wa Rais ikiwa ni Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali kwa kusikia kumbe ana jumba bovu kule Dar es Salaam, na ndio linafanyiwa matengenezo na mwenzake Makamu wa Kwanza yeye ndio kabisa analala hoteli. Hii ni aibu, hii ni kielelezo tosha *we are not serious with our leaders.*

Mhe. Naibu Spika, naiomba Serikali ilione hili, tufanye marekebisho tena ya dharura wasitutilie aibu viongozi wetu kwa kukosa hata hapa pa kukaa, ndio aibu ya nchi yetu, ndio kielelezo cha nchi yetu ilivyo.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, ninaomba kukaa kitako.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia machache katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Fatma Fereji.

Awali ya yote nimshukuru mwingi wa rehma aliyetujaalia kufika hapa tukiwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zetu za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwanza kwa kutuwasilishia hotuba yake kwa ufasaha kabisa, lakini vile vile kwa kuweza kutuunesha hali halisi ya majukumu ambayo amepewa; nayo ni majukumu mazito, kwa sababu yanahusu jamii moja kwa moja.

Ni majukumu ambayo matokeo yake yanatakiwa yaonekane na sio matokeo ambayo unaweza kuyazungumza kama ni taarifa lakini ni matokeo ambayo yanatakiwa yawe wazi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme naunga mkono hutuba kwa asilimia 100 na ningewaomba wenzangu waichangie kadiri ya uwezo wao hotuba hii, kwa sababu ina manufaa sana katika Taifa letu, lakini vile vile tunapoweza kuishauri Serikali lakini na kumshauri Waziri ndio jambo ambalo linawenza kuleta manufaa mazuri au linawenza kusaidia katika utekelezaji wake wa shughuli hizi ambazo amekabidhiwa.

Vile vile nitoe pongezi na nishukuru sana Katibu wake Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wake wote ambao na wao wamemsaidia kwa kiasi kikubwa Mhe. Waziri kuweza kufanikisha yale ambayo wameyafanikisha kutokana na hali halisi ya uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze katika ukurasa wa 7. Niipongeze sana wizara kwa kuanza sasa tunayo sera ya mazingira lakini vile vile kujaribu kuandaa sheria za usimamizi wa mazingira, ambayo itasaidia sana katika kuweka mipango na mikakati itakayoweza kunusuru athari za mazingira katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba pamoja na yote, tumeona kuna hatua nyingi ambazo zimechukuliwa ikiwemo kupitia miradi mbali mbali inayoweza kusababisha athari za kimazingira, na tathmini zake zimeweza kusaidia katika kuona namna gani hatua zinaweza kuchukuliwa ili kupunguza athari za mazingira.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niipongeze sana Serikali kwa hatua ambayo wamefikia sasa hivi hasa kuhusiana na suala zima la watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, kuna changamoto nyingi sana katika kundi hili la watu wenye ulemavu na changamoto nyingi zinajitokeza ni suala zima sasa la kupata haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningewaomba sana, na ninafurahi sana kwamba Mwanasheria Mkuu yuko hapa ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu au makundi mengine yoyote madogo madogo yanapata haki zao. Hebu tujaribu kuzipitia tena sheria zetu zote na kuona kuna upungufu gani ambaio unasababisha kukosa haki zao kwa makundi haya, hasa ya wale mavu.

Tuzipitie sheria zetu, kwa sababu ninaamini kwamba kuna baadhi ya sheria bado zinamkandamiza mlema vu au makundi mengine haya madogo madogo. Kwa hivyo ningeomba sana hili na hususan kwenye suala zima la udhalilishwaji watu wenye ulemavu, tumeona kwamba sasa hivi kumezuka wimbi kubwa la wadhalilishaji ambaio zaidi wanakwenda kwa wale mavu, na kwa sababu wanakuwa hawaaminiwi sana katika ushahidi wao, matokeo yake wale mavu wanakosa haki zao.

Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba hili sasa hivi tulitilie maanani, tukijua kwamba na hawa wana haki sawa sawa na wanadamu wengine.

Mhe. Mwanasheria Mkuu tukikosea hapa na tukashindwa kulifanya hili basi tukakikishe kwamba wimbi sasa la kuanza kuharibu wale mavu litaongezeka.

Mhe. Waziri nilikuwa natizama katika kitabu chako nimegundua kwamba hivi sasa kuna mfuko maalum wa wale mavu, lakini mimi nimejiuliza, je, mfuko huu umeanzishwa kisheria? Na hofu yangu ni kwamba hatuteweza kujipanga vizuri kama mfuko huu hauko kisheria, kwa sababu kwanza lazima tujue lengo hasa la mfuko huu, lakini vile vile tujue vianzio vyta mapato ya mfuko huu, lakini je, mfuko huu utaendelezwa vipi? Hayo ni mambo ya msingi ambayo lazima tuyaangalie kwa sababu nakumbuka hapa, na Waheshimiwa wengi walichangia

mfuko huu lakini mpaka leo hii hatujui hasa mfuko huu uko katika sheria gani. Ningombma sana na mimi ningetoa wazo kubwa, kwa sababu Mhe. Waziri hivi sasa tayari nimeshafanya tathmini ya kujua walemaru wangapi wapo kwa upande wa Zanzibar na aina za ulemavu. Lakini hawa wanahitaji msaada mkubwa hususan kwa wale walemaru ambao wanahitaji msaada mkubwa kutoka kwa aidha wazazi au walezi wanaowalea.

Mfuko huu unaweza kutoa msaada wa kuwapa wale walezi ambao wanalea watoto walemaru, ambao kwa kweli wana kazi kubwa sana, na wanashindwa kufanya kazi zao nyengine za kiuchumi, kwa sababu ya hali pengine ya mtoto au ndugu yake ambaye anaishi naye.

Ningombma mfuko huu sasa ufanyiwe kazi na uwe mfuko endelevu ili uweze kusaidia familia ambazo zinaathirika katika masuala ya ulezi wa watoto walemaru.

Mhe. Naibu Spika, sasa nitaingia katika suala zima la madawa ya kulevyia. Mhe. Waziri mimi nikupe pole kubwa sana, kwa kweli suala hili ni suala zito na gumu sana kulitekeleza, na hata hayo Mataifa makubwa ambayo tunasema kwamba ni Mataifa yaliyoendelea katika suala hili wanashindwa kulitekeleza. Na mara nyingi sisi tunafikiria kwamba ambayo inawezekana ni moja katika tatizo ambalo linatufanya tatizo hili lisiondoke, ni kwamba tuna muhali wa kutoa taarifa, lakini ukweli hasa sio tu muhali lakini kuna uoga wa kutoa taarifa kutokana na mazingira hasa ya kesi kama hizi za masuala ya madawa ya kulevyia.

Tunaelewa sote kwamba madawa ya kulevyia mengi sana yanaingia, na mengi yao yanapita zaidi tunasema Zanzibar ni kama dirisha la madawa ya kulevyia, yanapita kuelekezwa sehemu nyengine kwa sababu kwa umasikini wetu sidhani kama biashara ya madawa ya kulevyia inaweza ikawa kubwa sana hapa, na kutokana na idadi ya wananchi waliokuwepo hapa. Lakini bado Zanzibar imekuwa ni sehemu ambayo inaathirika sana kwenye masuala ya madawa ya kulevyia. Lakini na mikakati yake ambayo inatumika katika kuhakikisha kuondoa tatizo hili hasa kwa uingizwaji wa madawa ya kulevyia bado imekuwa inaleta changamoto kubwa.

Mhe. Waziri ndio maana nakupa pole, kwa sababu najua kazi hii ni kazi nzito, na wizara yako peke yako haiwezi kufanya kazi, mukishirikiana na hizo taasisi nyengine, lakini taasisi nyengine pia zina vikwazo vingi ambalo moja ni suala zima la rushwa.

Suala la rushwa hapa linaingia sana, kwa sababu kesi nyingi zinazohusiana na usafirishwaji wa madawa ya kulevyia sisi wenyewe tunajua kwamba hazifiki pahala popote na hazichukuliwi hatua ya aina yoyote. Ina maana kwamba hili suala litaendelea kuwepo, hasa kwa sababu wale wanaohusika na mambo hayo bado

wako uraiani, wanaishi na wanaendelea na tena wanadunda, wanadunda zaidi ya wale raia ambao ni raia wema ambao hawafanyi biashara hiyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini tukiachia na hayo wanaotuumizia ni watoto wetu ni vijana wetu. Mimi nikupongeze sana Mheshimiwa, kwamba mumefanya jitihada tumesaidia, sasa hivi vijana wengi kutokana na masuala haya ya madawa ya kulevyta na elimu imeingia katika maeneo mengi, hususan katika maskuli yetu, tuipongeze sana.

Lakini vipindi nya redio na televisheni tumekuwa tukivisikia vikizungumzia suala hili la madawa ya kulevyta. Lakini bado tuna wengi ambao wanaanza, wanajifundisha na hili ndio rika hatari sana ambao wanajifundisha kuanza kutumia madawa ya kulevyta, na iko haja sasa ya *ku-concentrate* zaidi katika vijana hawa wenye rika hatarishi ambao wao imekuwa kama matumizi ya dawa ya kulevyta zaidi wanaigana zaidi, na kutaka kujuwa hasa ni kutokana na maumbile yao ya utundu wanataka kujuwa haya madawa ya kulevyta yanasaidia kitu gani.

Kwa hiyo, hili kundi ningeomba sana Mhe. Waziri tulifanyie kazi kubwa sana, kushirikiana na Wizara ya Elimu kuweza sasa kutoa mafunzo maalum hasa kwa vijana ambao kwa kweli wako kundi hatari la kupata maambukizi hayo.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine niseme tu kwamba sote tunafahamu suala zima la maambukizi ya Ukimwi ambayo yanatokana na matumizi ya dawa ya kulevyta.

Mimi niipongeze sana Wizara yako pamoja na Tume ya Ukimwi kwa kufanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba hili lisiwe tatizo la kuweza kuleta maambukizi ya Ukimwi kuongezeka kila siku.

Na kwa sababu hiyo tumeona kwamba kwa kweli elimu inayotolewa ni nzuri, na tunaona kwamba maambukizi ya Ukimwi katika kundi hili kidogo kidogo yanaanza kupungua kidogo sana. Kwa hiyo, niseme tu kwamba niipongeze sana Tume ya Ukimwi kwa kazi kubwa ambayo imefanya, lakini kuyafikia yale makundi mengine ambayo kwa kweli yako katika hatari ya kuambukizwa Ukimwi nayo ni makundi ya kina dada poa pamoja na kaka poa na wengine, yote haya kwa kweli yanaweza kusababisha kuongezeka kwa Ukimwi katika jamii yatu.

Kwa hiyo, nichukue fursa hii Mhe. Waziri kukupongeza sana, na niiombe sana wizara na hasa kwa sababu sasa hivi tunajua kwamba wenzetu Mashirika ya Kimaendeleo sasa hivi kasi ya kutusaidia imepungua sana, kwa hiyo ipo haja ya sisi serikali hivi kuweza kutia mkono wake kwa kiasi cha juu kabisa ili kuhakikisha tatizo hili linapungua.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kutoa miongozo pamoja na masuala mbali mbali ya elimu ambayo yanasaidia katika kuondosha unyanyapaa kwa wale ambao wamepata maambukizi ya Ukimwi.

Mimi niipongeze sana Tume ya Ukimwi wamefanya kazi nzuri kwenye suala hili, lakini vile vile wameweza hatia kuwasaidia wale ambao wameambukizika na virusi ya Ukimwi kuweza kuwashajihisha kufanya miradi mbali mbali ambayo imeweza kuwainua kiuchumi na kuweza kusaidia familia zao. Kwa hiyo, niipongeze sana Tume ya Ukimwi, Mhe. Waziri pamoja wizara yako.

Mhe. Naibu Spika, nitaingia katika suala la mabadiliko ya tabia nchi pamoja na mazingira. Mhe. Waziri suala hili ni suala mtambuka. Tunalielewa sote na tumeona kwamba wizara yako inalifanya kazi, lakini bidii kubwa zaidi inahitajika. Na mimi niseme tu kwamba nimeshukuru kwamba naona namna ya mipango ambayo imepangwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa suala hili tunaweza kulifanya kazi hasa katika suala la ufuatiliaji wa masuala mbali mbali na kuweza kufanya kazi pamoja na asasi za kiraia ambazo mumezihusisha moja kwa moja, lakini vile vile na kuweza kufanya kazi na taasisi mbali mbali zinazohusiana na masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, lazima wananchi waelewe, wafahamu kwamba mazingira yetu yanaharibiwa, na sisi ndio tunaoharibu mazingira yetu sio mtu mwengine, ni machache sana ambayo yanakuja kutokana na hali ya ulimwengu ulivyo, lakini mengi yanasaababishwa na sisi wenywewe.

Kwa hiyo, elimu ni kitu muhimu sana, lakini vile vile mimi niseme kwamba nimeshukuru kuona sasa hivi katika programu moja ndogo ya usimamizi wa mabadiliko ya tabia ya nchi yatatoa mwanya sasa yatatuonesha dhahiri hasa katika huu mpango tulionao wa *PBB*, yataweza kutuonesha kwa undani kabisa kitu gani kimefanyika lakini kitu gani kimetekelzeza na muda wa kutekeleza hilo jambo, lakini vile vile *impact* ambayo imepatikana katika mradi huo. Kwa hiyo, mimi nishukuru mipango iliyopangwa ndani ya *program* hizi, kwa kweli ni mipango mizuri sana itatupa nafasi kubwa sana sisi Waheshimiwa kuanza sasa kufuatilia, serikali imefanya jambo gani na imefanikiwa hata kama kuna changamoto zinazojitokeza.

Changamoto zimejitokeza wapi na hivi ili tukijua changamoto na tunaweza kujua vipi kuzifanya kazi changamoto ambazo zimetukibili. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba kwa kweli nimeona tumepiga hatua kubwa sana, hasa kwa kuzingatia kwamba sasa imeonekana kuwa suala la miradi ambayo hasa miradi kama hii inaweza kuonekana na kuweza kuleta tija yake ndai ya jamii.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumzia nafikiri nimemaliza yote, lakini ni suala lile ambalo nililisahau hili mwanzo kabisa nilipozungumzia suala la walemaavu.

Naomba Mheshimiwa kujua kwamba kwa sababu nakumbuka kwamba kulikuwa na Sera ya Watu Wenye Ulemavu ambayo ilikuwa inaandaliwa, na hii hatua sijui imefikia wapi na utekelezaji wa sera ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kujua hii imefikia wapi, nafikiri ilikuwa ni suala zaidi nilitaka kujua. Niseme baada ya kusema hayo machache sikuwa na mengi sana ya kuzungumza hii wizara ina sekta ambazo kwa kweli ni muhimu sana katika jamii yetu ambazo zinahitaji ufuatiliaji na utekelezaji wa makini sana.

Na mimi nishukuru kwamba Waziri ambaye amepewa jukumu hili ni waziri makini mimi namfahamu, na vile vile naamini kabisa kwamba anao uwezo mkubwa kwa sababu ni mwanamke, na ametudhihirishia kwamba uwezo wake wa kuweza kuendesha wizara hii kwa kweli ni mkubwa, na basi nimuombee Mwenyezi Mungu amjalie aweze kuendelea na kutujengea Taifa letu kwa pamoja ili tuweze kufanikiwa katika mambo yetu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo sikuwa na mengi ya kuzungumza, lakini mengi ambayo yamenigusa nimeweza kuyazungumza, na basi baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofî*)

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakupongeza kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa katuweka mpaka sasa hivi hapa ikawa tunachangia hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nitachangia ukurasa wa 19, ibara ya 69 Idara ya Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, mazingira ni mfumo mzima wa kimaisha au mpangilio wa nchi au mwanadamu.

Mhe. Naibu Spika, mazingira ni jambo linalohusu wizara zote za serikali; Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Biashara, Wizara ya Afya, Miundombinu zote zinajumlishwa na mazingira.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nikienda katika mazingira ya hali ya Mji wetu wa Zanzibar. Mazingira ya hali ya mji wetu bado kimazingira haujawa safi kuna

mitaro, takataka nyingi, kwa hivyo hiba ya mji kimazingira bado hatujafikia sehemu ambayo inaridhisha.

Katika Manispaa yetu hasa ukiingia katika eneo lile la Darajani utakuta hata vyoo vya kujisaidia wanadamu hamna. Kwa hivyo, ni moja katika mazingira yasiyopendeza katika mji kama ule.

Mhe. Naibu Spika, katika uchafuzi wa mazingira kuna sehemu ambazo zinamwaga taka au mitaro michafu. Hii ni moja katika uchafuzi wa mazingira, na hili jambo ambalo linahusu kila mwanadamu au kila wizara.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika sehemu za afya bado mazingira ya hospitali zetu hazijakuwa nzuri hasa ukiingia katika sehemu za kujisaidia wagonjwa mazingira yanakuwa machafu.

Mhe. Naibu Spika, ukienda katika sehemu ya kilimo bado mazingira ya kilimo yangali yanatatiza wakulima ili kupatiwa pembejeo, madawa na kulima kwa wakati pia ni moja katika mazingira ya wakulima kuwekewa mazingira safi ya kuweza kulima kilimo wakapata mahitaji yao mazuri, hiyo ni moja ya mazingira.

Mhe. Naibu Spika, kuna mazingira ya miundombinu. Leo ukienda katika sehemu zetu za barabara, barabara ni mbovu, hazijengwi kiutalamu, hazina kiwango, ni moja katika mazingira machafu.

Nchi za wenzetu barabara wanajenga katika mazingira safi, madaraja yao ni safi, mapana yanaweza yakapita gari tatu.

Leo kama utakwenda njia hii ya kutoka hapo Bububu, tuanzie Bububu tu tuelekee Chaani basi utaomba dua Mwenyezi Mungu hii gari isije ikatumbukia katika daraja, ni katika moja ya mazingira machafu ya kujenga madaraja mabovu.

Mhe. Naibu Spika, tunakwenda katika mazingira ya kibashara, wananchi wa Zanzibar bado hawajawekewa mfumo wa kufanya biashara, wenzetu zinajengwa *Super Markets*, tunatembea tunaona wanavyoensiwa wafanyabiashara. Bado mazingira ya biashara kwetu ni mabovu yote ni katika jumla ya mazingira.

Mhe. Naibu Spika, tunakwenda katika mazingira ya lishe, lishe pia ni moja katika mazingira sio kukata miti tu na kuweka miti, mazingira mpaka mwanadamu ana mazingira ya lishe. Mwanadamu anahitajika apate mlo angalau mara mbili kwa kutwa. Kwa hivyo, serikali ihalikishe kwamba bado mazingira ya wananchi wa Zanzibar ni machafu kutohana na hali ya kimaisha. Kwa hivyo, wizara zote za Zanzibar zinahusika na mazingira ya nchi na wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika hali ya mazingira ya kuweka biashara zetu au sehemu zetu za utalii.

Mheshimiwa tuna visiwa humu Zanzibar vya utalii ambavyo vinatupatia fedha sana, kule katika jimbo langu la Matemwe kuna kisiwa kinaitwa Mnemba. Mnemba sasa hivi kinaliwa na bahari sana, kisiwa ambacho ni tegemeo kubwa kwa serikali kwa utalii, kuna hoteli kubwa sana kule, lakini bado kutokana na hali ya mazingira kisiwa kile kinaliwa na bahari.

Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais anayeshughulika na mazingira namuomba afanye ziara kwa makusudi ya kwenda kuangalia kisiwa kile cha Mnemba.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika ukurasa wa 21 Idara ya Watu wenye Ulemavu. Zanzibar kuna walemovu, kuna walemovu vipofu, waliokatika miguu, walemovu wengi sana lakini bado serikali haiwawekei utaratibu mzuri wa kuwashifadhi walemovu. Kwa hivyo, naiomba serikali ihakikishe walemovu inawasaidia na inawaenzi.

Mhe. Naibu Spika, nije katika sehemu ya Uratibu wa Madawa ya Kulevy. Hivyo Mhe. Naibu Spika, tukijiuliza haya madawa ya kulevy yanayopiganiwa kila siku yanaletwa na nani? Tukikaa hapa mkamatwa na ndizi anahukumiwa, kuna mtu kaiba muhogo anakamatwa, wengine wanaiba ng'ombe wanakamatwa lakini mleta madawa ya kulevy hakamatwi ana siri gani. Sijasikia Mahakama imemuhukumu tajiri au mtu yejote mwene kuleta madawa ya kulevy akafungwa, sijasikia, lakini kaiba ndizi anapigwa faini anaambiwa ndio fundisho hili na miezi mitano au faini shilingi laki mbili, lakini sijamsikia tajiri au mtu yejote aliyeleta madawa ya kulevy akakamatwa, na madawa ya kulevy hayalimwi Matemwe, madawa ya kulevy yanapita Bandarini au Uwanja wa Ndege, lakini yanapita vipi mpaka yanatapakaa Zanzibar na mizigo huwa inaangaliwa. (*Makofi*)

Mimi nikipita pale Malindi gatini kuna jiti linapapasa hivi, papa papa. Sasa nashangaa madawa ya kulevy yanapita vipi?

Mhe. Naibu Spika, kwanza serikali ihakikishe haya madawa ya kulevy yanapitishwa na nani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia namuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais aje atueleze hasa madawa ya kulevy yanapita vipi, kwamba sisi tunapapaswa mpaka majivu pale.

Mimi nikichukua begi langu pale linaganda kama nimechukua kiwembe cha kujitoa hizi ndevu zangu nyeupe, basi inaganda ile. Sasa nashangaa madawa ya kulevyta yanapitaje, lile begi haligandi, lile jiti linalopapasa pale halizungumzi. Kwa hivyo, naiomba sana Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ijithahidi sana na haya madawa ya kulevyta. Nakushukuru, ahsante.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii, nafikiria itanitosha kwa kuzungumzia machache katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwanza nimshukuru Waziri kwa hotuba yake hii, na niwapongeze watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya mpaka kufikia mafanikio ya hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, kama walivyoendelea kusema wenzangu kuwa wizara hii ina malengo na majukumu mazito, hasa ukiona kwamba kuna ofisi na idara zake mbali mbali ambazo zote ni majukumu mazito sana.

Kwanza wana Ofisi ya Faragha, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mazingira, Idara ya Watu wenye Ulemavu, Ofisi ya Makamu wa Rais Pemba, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta na Tume ya UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli haya ni majukumu mazito na ni lazima serikali ione kwamba kuna haja ya kuisaidia wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, waziri wa ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni mwanamke, na ni mwanamke jasiri ambaye anatambulikana kitaifa na kimataifa, na niseme kwamba wanawake tunaweza.

Ofisi hii imeweza kuratibu kwa ufanisi mkubwa shughuli za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, pamoja na mafanikio hayo ofisi hii imetuonesha kwamba imekuwa na changamoto ya msingi iliyodumu kwa kipindi cha miaka mitano ambayo ni kukosekana kwa makaazi rasmi ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais huko Dar es Salaam.

Kwa kweli hili ni tatizo kubwa, kuwa mpaka leo hii miaka mitano toka kuanzishwa kwa ofisi hii kutokuwa na makaazi ya Makamu huko Dar es Salaam.

Wenzangu wameshalisemea sana lakini na mimi nimeona nichukue fursa hii ili niweze kusema machache kuhusu kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, tukizingatia kwamba bajeti ni mpango ambao unalenga kwenye matumizi na mapato, kwa hivyo ni lazima tunapoyapata yale mapato tuyatumie kwa vizuri sana. Nimeona kwamba ingawaje ofisi hii huwa inatengeneza bajeti na baadae sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunapitisha kwa kiwango ambacho tunasema kwa asilimia mia moja, tunategemea kwamba fedha zile zitapatikana, lakini baadae fedha zile zinakuwa hazipatikani kama wizara husika inavyoomba.

Kwa kweli hili ni tatizo ambalo linaweza kuleta athari za kibajeti. Kwa sababu wizara zinakuwa na malengo yake na iwapo fedha zile hazikupatikana basi yale malengo yanakuwa hayafikiwi. Hili ni tatizo na nimeona kwamba kitabu hiki kinaonesha mapungufu ya bajeti. Kuna mambo mbali mbali ambayo wamejiwekea lakini fedha inayopatikana ni ndogo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye masuala ya watu wenyе ulemavu. Kama walivyosema wenzangu kuna uanzishwaji wa Mfuko wa Watu wenyе Ulemavu. Lengo ni utoaji wa huduma kwa watu hao, kuandaa rasimu ya sera ya watu wenyе ulemavu ambayo inatarajiwa kuwasilishwa serikalini hivi karibuni. Kwa hivyo, hili ni jambo jema na nampongeza Waziri kwa jitihada hizo.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii vile vile ina jukumu kubwa hili katika Sekta ya UKIMWI ambayo vile vile Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imetayarisha mkakati wa pili wa Taifa wa UKIMWI Zanzibar. Kwa hivyo, hili vile vile ni suala kubwa sana ambalo wizara hii imejithahidi kwa mambo hayo hapo, tunajua UKIMWI ni hatari, UKIMWI mpaka leo haujapata dawa, hivyo hili ni jukumu la wizara hii na inajithahidi kufanya mikakati mbali mbali ili suala hili liweze kuondoa yale makali hasa ya uendelezaji wa masuala ya UKIMWI au ugonjwa wa UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna tatizo la dawa za kulevyta. Hili ni tatizo sugu na kwa kweli serikali naiomba iwe na *strategy* ya kuzuia haya madawa ya kulevyta. Mara nydingi huwa wanatafutwa wale watumiaji wa madawa ya kulevyta lakini wale wauzaji wa madawa ya kulevyta hawafuatwi wala hawatafutwi kusema kweli.

Mara nydingi anatafutwa yule anayetumia madawa ya kulevyta, kama serikali ilikuwa inatafuta hasa ingekuwa na jitihada kwa hawa wanaoleta madawa haya ingekuwa ni rahisi sana. Kwa sababu unapowapata hawa watumiaji wao ingekuwa ndio wapelekaji kwa hao wanaoleta madawa ya kulevyta, ingekuwa ni rahisi kwao wao kuwa-*direct* hawa wanaoshughulika na kutafuta watumiaji pamoja na hawa waletaji wa madawa ya kulevyta.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba, kwenye bajeti hii kunakuwa na mapungufu na nimeona ofisi hii na hasa hii Idara ya Faragha kuna asilimia kubwa ambayo imepatikana, sidhani kama kipindi hiki kilichobakia kitapatikana ili yale malengo yake iweze kutimiza.

Mhe. Naibu Spika, kitabu kimeeleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2014. Idara ya Mipango na Utafiti iliratibu utekelezaji wa miradi miwili ya maendeleo, na tumeona hapa mradi wa kujenga kituo cha tiba na marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevyta.

Kama walivyosema wenzangu kwamba bora kukinga kuliko kutibu, ni bora kufanya kinga lakini hata tukiawewka watumiaji wa madawa pahala ikiwa bado madawa ya kulevya yanaingia kwa kasi, basi tutakuwa hatujafanya jambo litakalotuondoshea matatizo haya.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema bado uingizwaji wa fedha hizi, kwa sababu mradi huu ulitegemewa fedha za SMZ kwa mwaka 2014/2015 kuwa uwe umekamilika. Lakini kutoptana na fedha hizi zilizopatikana inaonekaa bado lile lengo lilokusudiwa halijafikiwa.

Idara nyengine ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo hii nasema kwa upande mwengine ni idara mama ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji na utumishi zikiwemo sheria, kanuni za utumishi, mafunzo, maslahi na maendeleo ya wafanyakazi. Kama ni hivyo, basi nitegemee kwamba kwa sababu ina majukumu kama hayo, ni lazima bajeti yake itakuwa ni kubwa. Lakini kama kawaida fedha zake pia zinazopatikana mpaka sasa hivi haziridhishi.

Idara ya Mazingira. Kama walivyosema wenzangu ni kweli hii idara nayo inakumbwa na changamoto; kuna uchafuzi wa mazingira. Kama wenzangu walivyosema kamati yangu ya PAC hivi karibuni tulikuwa Pemba na tumeona uchafuzi wa mazingira yale ya tabianchi na mengine, kwa sababu ya ukali wa maisha watu wanazimika kuchimba michanga kwa kufanya matofali, vile vile kuchimba miamba kuikata kwa kufanya matofali. Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo linatuathiri, linaathiri kwa kiasi kikubwa na hata Mdhibiti ameona kwamba kuna tatizo la uchimbaji wa mchanga na kifusi kwa makampuni ya ujenzi wa barabara.

Uchimbaji wa mawe kwa wananchi, uchimbaji wa matofali ya kujengea na ukataji wa mikoko sehemu za pwani. Hii imepelekea sasa kuvamiwa visiwa hivi na maji ya bahari, na ukaguzi huo ilikuwa ni kuangalia kwa kiasi gani miradi hiyo inakidhi matakwa ya sheria juu ya utunzaji wa usimamizi wa mazingira.

Mkaguzi amesema katika ukaguzi uliofanyika ni kwamba miradi mingi wakati wa utekelezaji wake haizingatii matakwa ya sheria ya usimamizi wa mazingira kwa maendeleo endelevu ya mwaka, 1996.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii imeeleza ni hatua gani zinazopaswa kuchukuliwa kwa madhumuni ya kulinda na kuhifadhi mazingira, mambo ambayo yalipaswa kuzingatiwa yameelezwa.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono. (*Makofī*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa mashirikiano mlionipa na bahati nzuri wizara hii imepata wachangiaji 18, tisa tayari wamekwishachangia na tisa tutaendelea nao Jumatatu kipindi cha asubuhi baada ya maswali ili jioni tuweze kujumuisha.

Na naomba niwataje ili roho zikifika basi tuje mapema tuweze kuchangia. Kwanza atamalizia Mhe. Fatma Mbarouk Said, atafuatia Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Viwe Khamis Abdalla na wa mwisho Mhe. Zahra Naibu Waziri wa Elimu yeye atajibu hoja zilizomgusa katika wizara yake.

Baada ya maelezo hayo niahirishe kikao chetu hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 25/05/2015 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:42 usiku Baraza lilahirishwa hadi siku ya Jumatatu
tarehe 25/05/2015 saa 3:00 asubuhi)*

